

ATHARI ZA SHENG KATIKA DINI YA KIKRISTO: MTAAC WA UMOJA.

NA

ODHIAMBO GEORGE OGUTU

IDARA YA ISIMU NA LUGHA: CHUO KIKUU CHA NAIROBI

2013

ATHARI ZA SHENG KATIKA DINI YA KIKRISTO: MTAAC WA UMOJA

NA

ODHIAMBO GEORGE OGUTU

C50/69125/2011

**TASNIFU HII EMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA
SHAHADA YA UZAMILI**

KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.

OCTOBER, 2013.

IKIRARI

**TASNIFU HII NI KAZI YANGU MWENYEWE NA HAIJATOLEWA KWA MAHITAJI
YA SHAHADA KATIKA CHUO KIKUU KINGINE**

ODHIAMBO GEORGE OGUTO

**TASNIFU HII IMETOLEWA KUTAHINIWA KWA IDHINI YETU KAMA
WASIMAMIZI WALIOTEULIWA NA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

DKT. AYUB MUKHWANA

NA

BW. NDUGU BASISIO G. MUNGANI

TABARUKU

Kazi hii ninawatabarukia watoto wangu, Abigael, Easter na Christine kwa hali na maisha magumu waliyovumilia kwa muda mrefu nilipokuwa masomoni. Nawashukuru kwani wao ndio waliokuwa sinikizo langu kuu la kuipanda ngazi hii ya elimu ili nipate kuwa mfano mwema kwao katika Nyanja hii ya elimu.

Pia kwa heshima na taadhima kuu, ninawakumbuka wafadhili wangu Bi. Simon Vicky, SR. Margaret Wanjiru, na Father Miles Healey. Kama sio kwa hisani zao, kwa hakika nisingeliweza kuvipanda na kuvikamilisha vyema vidato hivi vya elimu. Wote hawa kwangu walikuwa mfano wa petroli katika chombo chochote kile cha usafiri. Bila wao chombo changu cha usafiri kwa hakika kisingetua salama katika bandari hii ya elimu. Nawavulia wote kofia.

SHUKRANI

Ama kwa kweli, kidole kimoja hakivunji chawa. Halingekuwa jambo la busara kuandika kazi kama hii bila ya kushirikiana na kupata mawaidha kutoka kwa wendani, wataalamu na wanataluma mbalimbali. wote hawa walinifaa kwa hali na mali. Orodha ya waja hawa wote walionifaa ni ndefu mno. Hivyo basi sitawataja wote ila baadhi yao tu.

Mcha Mungu si mtovu wa nidhamu. Hivyo ninamshukuru Mungu kwa mbele kwani ye ye ndiye aliyenijalia kwa pumzi, nguvu, ari, na maarifa ya kuifanikisha kazi hii. Pasi ye ye nisingeliweza kuukamilisha wajibu huu kwa jinsi ilivyostahiki.

Pili, ninaushukuru usimamizi mzima wa chuo kikuu cha Nairobi kwa busara yao ya kuendeleza shughuli ya masomo ya uzamili: kitengo cha isimu na lugha. Ni kutokana na usimamizi huu ambapo sisi kama wanafunzi wa isimu na lugha tuliweza kuwapata wahadhiri waliohitimu na wenye ari ya kuwaongza wanafunzi wao vyema hadi kufikia kilele cha malengo yao maishani hasa katika nyanja hii ya elimu.

Shukrani zangu chekwa pia ziwafikie wasimamizi wangu, Dkt. Ayub Mukhwana na Bw. Basilio G. Mungania hasa kwa hekima na ushauri wao wa busara kwangu. Nilipowauliza swali, kwa nilipokea zaidi ya jibu. Nilipotamauka, walinitia moyo. Nilipolaza damu walnikumbusha umuhimu wa kuimaliza safari hii kwa muda ufaao. Nilipokanya chechele walikuwa tayari kunirejesha njiani. Na kila nilipowapokeza faslu zangu za utafiti walizipokea kwa mikono mikunjufu kisha wakanirejeshea kwa muda uliofaa baada ya kuzitahini. Mungu na awazidishie pumzi ili muendelee kuwaffaa wengi wengine katika Nyanja hii ya elimu.

Vile vile nawashukuru wahadhiri wangu wote wa chuo kikuu cha Nairobi hasa katika idara ya isimu na lugha. Wote hawa walinfundisha katika vitengo mbalimbali vyta masomo yangu ya uzamili. Hawa ni pamoja na Dkt Iribi Mwangi, Prof. John Habwe, Dkt. Mwenda Mbatia, Dkt Zaja Omboga, Dkt Mweri Jefwa, Bw. Basilio G. Mungania, Dkt Mbuthia na wengine wengi. Na Mola awajalie siha njema ili kazi za mikono yenu ziendelee kuwa Baraka kwa wengine wengi hasa katika Nyanja hii ya elimu.

Naomba pia kuwashukuru wazamili wenzangu tuliozama nao pamoja katika bahari hii ya elimu. Katika kina cha upiga mbizi wetu, tuliweza kuyaafikia mengi kutokana na ushirikiano wetu wa bega kwa bega. Hawa ni pamoja na Owallah, Mureithi, Akeyo, Makange, Muniu , Abiero, Suakei, Katutu, Chacha, Kerubo, Otiende, Maundu, Onyonka, Grace, Koech, Njeri, Nguti, Mutuka, Florence, Kipng'etich na Keter, Mungu awape mbawazi njema ili waweze kushereheke matunda matamu ya jitihada zao kwa elimu tulioipokea. Kwa elimu hii, naomba mpate kuchangia pakubwa katika ustawi wa taifa letu na ulimwengu wote kwa jumla.

Nalipenda pia kuwashukuru marafiki na washiriki wangu katika utafiti huu, Bonface na Benson kwa msaada wao usio na mipaka nilioupokea kutoka kwao. Wote hawa wawili walinifaa sana katika kunakili na kuichapisha kazi yangu ya utafiti. Vile vile hawa wawili ndio waliokuwa nguzo na mhimili wangu mkuu katika ukusanyaji, uchanganuaji na utafsiri wa maneno ya Sheng katika Kiswahili sanifu. Nawavulieni kofia.

Kwa heshima na taadhima kuu naomba pia shukurani zangu ziwafikia walimu wote wa shule ya Msingi ya kihumbuini kwa ushauri wa busara niliopokea kutoka kwao. Kwao nilikuwa mnuna, hivyo basi walichukua jukumu la kunishauri ili niweze kujinyima kwa yote na kurejelea elimu. Ingawaje wote hawa walinifaa kwa hali na mali lakini ningelipenda kuwatambua hawa wafuatoa ambao kwa hakika walikuwa karibu sana na chemba cha moyo wangu: Bw. Ondari, Bi. Mugeni, Bi. Gachanja na Bi. Mary. Mungu na awabariki kwa ushauri wenu ili mwendelee kuwa mwanga kwa vizazi vyaya sasa na vijavyo hasa katika muktadha huu wa elimu.

Tamatini, ninawanyoshea mkono wa pongezi wale wote ambao wataisoma tasnifu hii kwa umakinifu na kuifanya uhakiki wa kina na haki. Pia nawapongeza wote watakaondeleza utafiti wa baadaye kuhusiana na mapendekezo ya utafiti wa ziada niliyopedekeza kuhusu athari za Sheng katika dini ya Kikristo.

YALIYOMO

Ukurasa

Ikirari-----	iii
Tabaruku-----	iv
Yaliyomo-----	v
Shukrani-----	vii
Muhtasari-----	-xi
Orodha ya vifupisho vilivyotumika.-----	xiv

SURA YA KWANZA;

1.0 Utangulizi-----	1
1.1 Tatizo la utafiti-----	1
1.2 Madhumuni ya utafit-----	3
1.3 Nadharia tete -----	4
1.4 Sababu za Kuchagua Mada Hii-----	4
1.5 Upeo na mipaka ya utafiti -----	5
1.6 Msingi wa kinadharia -----	9
1.7 Yalioandikwa kuhusu mada hii-----	13
1.8 Njia za utafiti-----	17
1.9 Umuhimu wa utafiti huu-----	18

SURA YA PILI;

2.0 UUNDAJI WA LEKSIMU ZA SHENG

Utangulizi-----	19
2.1 Ukopaji na utohozi -----	23
2.1.1 Ukopaji na utohozi: Maneno ya Kingereza-----	24
2.1.2 Ukopaji na utohozi : Maneno ya Kiswahili-----	25
2.1.3 Uokopaji na utohozi: Maneno ya Kikuyu -----	27
2.1.4 Ukopaji na utohozi: Maneno ya lugha nyinginez-----	28
2.2 Mbinu ya ukatizaji-----	30
2.3 Mbinu ya uambishaji-----	32
2.4 Mbinu ya ubadilishaji Silabi-----	33
2.5 Onomatopia -----	34
2.6 Upolisemia-----	36
2.7 Ubunifu wa leksimu-----	37
2.8 Akrониму -----	39
2.9 Kaleki:Tafsiri mkopo-----	40
2.10 Uhulutishaji-----	41
2.11 Uambatishaji-----	42
2.12 Unyumbuzi kapa -----	43
2.13 Ujenzi Ghairi-----	44
2.14 Hitimisho-----	45

SURA YA TATU:

3.0 VIFAHIIWA NA SENTENSI ZA SHENG

Utanguli-----	46
3.1 Haponimu-----	47
3.2 Sinonimu-----	50
3.3 Homonimu-----	53
3.3.1 Homografu-----	59
3.3.2 Homofoni-----	59
3.3.3 Heteronimu-----	60
3.3.4 Kapitonimu-----	60
3.4 Polisemia-----	61
3.5 Antonimu-----	65
3.6 Hitimisho-----	69

SURA YA NNE:

4.0 SHENG NA MAHUB IRI YA INJILI

Utangulizi-----	72
4.1 Sheng na injili: Kiwango cha Kanisani -----	78
4.1.1 Sheng na injili: Makanisa ya Zamani-----	79
4.1.1.1 Maoni ya wachungaji kuhusiana na matumizi ya Sheng kanisani-----	80
4.1.1.2 Maoni ya wafuasi wazima kuhusiana na matumizi ya Sheng kanisani-----	80
4.1.1.3 Maoni ya vijana kuhusiana na matumizi ya Sheng kanisani-----	81
4.1.2 Sheng na injili: makanisa ya kisasa-----	83

4.1.2.1	Maoni ya wachungaji kuhusiana na matumizi ya Sheng kanisani-----	84
4.1.2.2	Maoni ya watu wazima kuhusiana na matumizi ya Sheng kanisani-----	85
4.1.2.3	Maoni ya vijana kuhusiana na matumizi ya Sheng kanisani-----	85
4.2	Sheng na injili: kiwango cha redioni-----	86
4.2.1	Maoni ya watu wazima kuhusiana na matumizi ya Sheng redioni-----	86
4.2.2	Maoni ya vijana kuhusiana na matumizi ya Sheng redioni-----	86
4.3	Sheng na injili: kiwango cha televisheni-----	89
4.3.1	Maoni ya watu wazima kuhusiana na matumizi ya Sheng kwenye televisheni-----	89
4.3.2	Maoni ya vijana kuhusiana na matumizi ya Sheng kwenye televisheni-----	90
4.4	Sheng na injili: kiwango cha vijisahani vyta santuri(CD ROM)-----	93
4.4.1	Maoni ya watu wazima kuhusiana na vijisahani mseto vyta santuri-----	94
4.4.2	Maoni ya vijana kuhusiana na vijisahani mseto-----	95
4.5	Hitimisho-----	96

SURA YA TANO

5.0 MAHITIMISHO YA UTAFITI

Utangulizi-----	99	
5. 1	Mambo ibuka-----	104
5.2	Mapendekezo ya utafiti -----	105
	Hojaji -----	106
	Marejeleo-----	115

MUKHTASARI

Tasnifu hii ililenga kutathmini athari za Sheng katika dini ya Kikristo. Kwa jumla tasnifu hii ina sura tano. Katika kila sura, tumeshughulikia maswala na vipengele maalum ambavyo vinaingiliana na kukamilishana.

Katika sura ya kwanza tumeshughulikia usuli wa tasnifu hii. Tumetangulia kwa kutoa maana na chimbuko la lugha ya Sheng. Vile vile tumefafanua kwa upana tatizo la utafiti, swala la utafiti, nadharia tete, sababu za kuchagua mada husika, msingi wa kinadharia, upeo na mipaka ya utafiti, njia za utafiti pamoja na umuhimu wa utafiti huu katika nyanja ya elimu na utafiti.

Katika sura ya pili tumejadili mbinu mbalimbali za uundaji wa maneno ya Sheng. Mbinu hizi za uundaji wa maneno tumezichanganua kwa kukita katika kiwango cha isimu cha mofologia. Katika michakato yetu ya kuzichanganua mbinu hizi za uundaji wa maneno katika Sheng, tumeweza kabaini kwamba mengi ya maneno ya Sheng huwa yamekopwa kutoka katika lugha zingine hususan Kiingereza, Kiswahili na Kikuyu. Maneno haya yaliyokopwa aidha hutoholewa ili yachukue sauti na muundo wa kimofologia wa leksimu za Sheng (kibantu). pamoja na ukopaji na utohozi, maneno ya Sheng pia yameundwa kwa mbinu zingine za uundaji wa maneno, kama vile uambatishaji, uambishaji, upolisemia, onomatopia, uhulutishaji, ubunifu, kaleki, ujenzi ghairi, akronimu, ukatizaji, ubadilishaji silabi na unyumbuzi kapa. Maneno ya Sheng ambayo kiasili hayatokani na ukopaji ni maneno buniwa pekee. Mifano ya maneno haya asilia ya Sheng ni pamoja na:

Sheng	Tafsiri	
Ndai	=	Gari
Nganya	=	Daladala
Ukedi	=	Ukimwi
Uchiwa	=	Urembo
Mbus	=	Msichana

Dingo	=	Mwizi
Bonoko	=	Gushi
Deng'a	=	Chuma

Hii ndio mifano ya maneno ambayo kiasilia tuliweza kubaini kwamba ni leksimu za Sheng.

Katika sura ya tatu tumeweza kubaini kwamba Sheng huzitumia lekisu hizo ilizojiundia kwa mbinu mbalimbali za kimofologia ili kijiundia vifahiwa . Baadaye wanajamii lugha hii ya Sheng huvitumia vifahiwa hivyo katika kujitungia sentensi. Sentensi hizo huwa za viwango mbalimbali vya kisintaksia na kisemantiki na ndizo ambazo hufanikisha mawasiliano mionganini mwa wanajamii lugha hii ya Sheng. Mifano ya vifahiwa hivyo vya Sheng tumevijadili kwa kuvitolea tafsiri ya Kiswahili sanifu. Sentensi ambazo huundwa kutokana na vifahiwa hivi huwa hazieleweki bayana na watu wasioilewa Sheng au wasiolengwa. Mojawapo ya watu hawa ni Wakristo wenye umri wa juu kama vile wazazi pamoja na vijana wasioilewa Sheng. Kundi hili la watu wasioilewa Shenge huitwa “fala,” jina ambalo huwa na lengo la kuwadunisha na kuwafedhehesha watu hawa. Kwa kiwango kikubwa, sentenzi hizi za Sheng tumeweza kuzichanganua kwa vigezo vya kisintaksia ila kwa juujuu tu. Hii ilitokana na sababu kwamba tulilenga kukita katika semantiki wala sio katika sintaksia. Hata hivyo matawi haya mawili yote huingiliana na kukamilishana kwa ujumla na misingi ya isimu.

Katika sura ya nne tumepata kufahamu kwamba wanajamii lugha ya Sheng huzitumia sentensi ilizojiundia kutokana na vifahiwa mbalimbali kwa kujieleza hasa kuitopia sanaa ya uimbaji. Nyimbo ambazo tumeziangazia ni nyimbo za Kikristo wala sio za kidunia. Hii ilitokana na sababu kwamba utafiti wetu ulikita katika kutathmini athari za Sheng katika dini ya Kikristo. Hivyo tumepata kubaini kwamba Sheng ina athari zake katika asasi na taasisi mbalimbali za kijamii na kidini. Mifano ya taasisi na asasi hizi ni pamoja na makanisa (ya awali na ya kisasa nchini Kenya), na vyombo vya habari. Mifano ya makanisa ya awali tuliochangangua ni pamoja na kanisa la Katoliki, kanisa la SDA, kanisa la Anglikana, kanisa la PCEA, kanisa la A.C.K na kanisa la ‘Quakers. Mifano ya makanisa ya kisasa ambayo tumeangazia ni pamoja na “The Holy Ghost Fire Ministry”, “Jesus is Alive Ministry”, na “God’s Favour Ministry”

Kati ya aina hizi mbili za makanisa, tumepata kubaini kwamba makanisa ya kisasa ndiyo ambayo yamekubali matumizi ya Sheng kwa kiwango kikubwa katika kufanikisha taratibu za ibada. Athari za Sheng katika makanisa ya awali bado hazijaanza kuchipuza ingawaje dalili zipo. Taasisi nyngine ya kijamii ambayo tuliweza kubaini kwamba athari za Sheng hujithirihisha kwayo ni taasisi ya habari na mawasiliano. Mifano ya vyombo vya habari ambavyo tumeviangazia ni redio, televisheni na vijisahani vya santuri.

Katika sura ya tano, tumeweza kujadili hitimisho la tasnifu hii. Vile vile tumeweza kujadili mambo ibuka ambayo hatukuwa tumeyajumuisha katika malengo na haipothesia zetu. Mambo haya ibuka ni pamoja na Sheng kutumiwa kwa kuyabuni makundi maovu ya watoto ambayo yana lengo la kuwafundisha na kuwashimiza watoto wasiwatii wazazi wao na watu wazima. Mfano wa kundi la aina hii ambalo tuliweza kulibaini ni kundi linalojulikana kama “Gaza”. Pia katika sura hii ya tano tumengazia maswala ya kijumla hususan yanayohusu matokeo ya utafiti wetu. Aidha tumependekeza baadhi ya maswala ambayo watafiti wa baadaye wataweza kuyaangazia kwa kina katika tafiti za baadaye.

ORODHA YA VIFUPISHO VILIVYOTUMIWA

K.R.A-----Kenya Revenue Authority

T.S.C-----Teachers' Service Commission

Bi.-----Bibi

Bw.-----Bwana

Prof.-----Professor

Dkt.-----Daktari

K.m-----Kwa mfano

NATO-----North Allaiance Treaty Organization

NASA -----National Aeronaustic And Space Administration

UNESCO -----United Nations Education Scientific and Cultural Organization

UNEP -----United Nations Environmental Program

KANU-----Kenya African National Union

KARI -----Kenya Agricultural Research Institute

KEFRI-----Kenya Forestry Research Institute

KETRI-----Kenya Trypasonomius Research Institute

KEMRI-----Kenya Medical Research Institute

SURA YA KWANZA

1.0 Utangulizi.

Sura hii ya kwanza inatoa habari za kimsingi, zikiwemo habari kuhusu tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada hii, msingi wa kinadharia, mbinu za utafiti na umuhimu wa utafiti huu. Kimsingi, utafiti huu ulihusu athari za Sheng katika dini ya Kikristo. Utafiti huu ulifanyika katika maeneo ya eneo bunge la Embakasi, hususan katika mtaa wa Umoja. Eneo bunge hili linapatikana katika Kaunti ya Nairobi. Kama ilivyo kawaida na maeneo mengine ya miji au sehemu za miji nchini Kenya, eneo hili la Umoja linajulikana kwa kuwa mionganini mwa mitaa yenye vijana wengi wanaoenzi matumizi ya Sheng katika mawasiliano yao na pia katika kuwasilisha hisia, maoni na mitazamo yao kuhusiana na maisha, kupitia njia za usanii. Matumizi ya lugha hii hasa katika asasi mbalimbali za jamii yamezua maoni na mitazamo kadha, hasa mionganini mwa wanajamii husika. Mionganini mwa wanajamii hawa ni jamii ya Wakristo. Hivyo basi, utafiti huu ulilenga kutathmini kama zipo athari zozote zile zinazosababishwa na matumizi ya Sheng katika asasi ya dini ya Kikristo.

1.1 Tatizo la Utafiti.

Lugha huwa sehemu muhimu ya utamadumi wa jamiilugha husika. Upo huu wa uelewa vile vile unatudhihirishia hoja kuwa, lugha ndiyo huwa mhimili mkuu wa utamaduni wa jamii yoyote ile. Kama dira, lugha huwaongoza wazaliwa na walelewa wa jamii fulani katika kuzifuata taratibu za kutenda kaida za jamii hiyo. Katika tathmini hii, Sheng kama lugha haijaachwa wala kutengwa na utaratibu huu wa kimsingi. Lugha ya Sheng Inao utamaduni na kaida zake vilevile. Kibayana, haya ndiyo mambo yatakayochangia kuwepo kwa athari za lugha hii katika dini ya Kikristo. Sababu ni kwamba, dini ya Kikristo ina lugha yake; ina utamaduni wake na kaida zake vilevile. Hivyo basi, tamaduni mbili tofauti zinapajaribu kuoanishwa kwa pamoja kwa minajili ya kuafikia na kufanikisha lengo fulani, basi ni bayana kwamba athari kadhaa zitachipuka. Lugha ya dini ya Kikristo ni lugha bayana. Ni lugha ambayo inastahili kueleweka moja kwa moja na Wakristo wote, bila ya utata wowote ule. Na hii ndiyo maana wahubiri wa Kikristo

hukitumia Kiswahili sanifu mtaani humu katika mahubiri yao iwe ni kanisani au katika shughuli yoyote ile inayohusiana na kaida za Kikristo.

Kwa upande mwingine lugha ya Sheng (ambayo hutumiwa na vijana katika mahubiri) ni lugha ambayo inaeleweka tu na kikundi cha watu wachache katika jamii ya Wakristo mtaani humu. Mahubiri wayatoayo, mashairi wayakariryo na nyimbo waziimbazo katika muktadha wa dini, ni mambo ambayo huwa hayaeleweki bayana na wafuasi wote katika dini hii ya Kikristo. Tazama mfano huu wa sentensi jinsi unavyojithihirisha katika Sheng:

Mf 1

1. (a) **Sheng:** Saa Godi analaik tuwe maholijoo.

(b) **Tafsiri:** Mungu anapenda tuwe watakatifu.

Mazungumzo kama haya yanapotolewa kanisani au mbele za umma, hayataelewaka bayana na watu wote katika jamii ya dini ya Kikristo. Hivyo basi malengo na makusudio ya wafuasi wa dini hii yatakuwa hayajaafikiwa. Hii itatokana na sababu kwamba sio umma au Wakristo wote ambao wana ufahamu na uwelewa wa lugha ya Sheng. Na iwapo watu hawa watalazimika kushiriki ghafla zenyе mazungumzo wasiyoyaalewa moja kwa moja basi mnung'uniko fulani utatarajiwa kuibuka. Hili ndilo jambo ambalo utafiti huu unalenga kutafiti na kubainisha.

Kunao watu wanaodai kwamba Sheng si lugha kwa sababu haina utamaduni. Madai kama haya vile vile yana maana kwamba Sheng kama lugha bado haina uwezo wa kusababisha athari zozote zile katika jamii. Wazo kama hili si la kweli kwa sababu leo hii tunapolitaja neno utamaduni, inatubidi tufikirie tena kwa mara ya pili. Sababu ya kufikirikwa ni kwamba, utamaduni ni dhana ambayo inafifia kila uchao. Utamaduni walioujua, wakaufuata na kuutekeleza mababu zetu, sio utamaduni tunaoujua leo hii. Vipengele vingi vya tamaduni hizi vimesahaulika, vimerekebishwa au hata kukataliwa (labda kwa misingi ya sayansi, teknolojia na mabadiliko ya kiwakati katika jamii zetu) na jamii nyingi. Tazama mfano huu: Jamii ya Wajaluo ilijulikana kwa utamaduni wao wa kutotahiriwa, kung'olewa meno sita ya chini ya mdomo na hata kubomolewa kwa nyumba ya mfu ili ijengwe upya. Leo hii mambo haya hayatendwi tena na jamii hii. Na huu sio mwisho wa mabadiliko haya ya kitamaduni katika jamii hii. Jinsi nyakati zinavyozidi kusonga ndivyo jamii hii itakavyozidi kuupoteza utamaduni wake asilia. Sasa swali ni hili: je, Jamii hii itaupoteza

utamaduni wake asilia wote – na labda iige utamaduni mwingine mpya - itakoma kuitwa jamii ya Wajaluo? Jibu ni, “La” kwa sababu, kando na kuupoteza utamaduni wao asilia, bado wataizungumza na kujitambulisha kwa misingi ya lugha yao ya Kidholuo. Kwa hivyo, lugha ndicho kitambulishi muhali cha jamii wala sio vipengele hivyo vingine vyta kitamaduni vinavyoambatanishwa nayo. Kwa msingi huu, hatuna budi kukiri kwamba, Sheng ni lugha. Na kwa sababu Sheng ni lugha, basi inao uwezo wa kusababisha athari kama zilivyo lugha zingine hasa pale inapotumiwa katika kufanikisha majukumu katika asasi zote za jamii kama vile dini.

Ili kuziba pengo hili utafiti huu ulijikita katika nadharia ya kitambulishijamii (The Social Identity Theory). Nadharia hii ndiyo iliyo na vipengele muhimu vitakavyonifaa katika kufanikisha malengo na madhumuni ya utafiti huu wetu. Vipengele vyta nadharia hii ni pamoja na: kigezo cha ujainishaji, kigezo cha ujitalishaji, na kigezo cha ujilinganishaji.

1.2 Madhumuni ya Utafiti.

Utafiti huu uliongozwa na madhumuni yafuatayo:

- a. Kubainisha kama matumizi ya Sheng katika dini ya Kikristo yatazua leksimu zenye maana mpya yasiyoleweka na wafuasi wote katika dini ya Kikristo.
- b. Kutathmini kama matumizi ya Sheng katika sajili ya dini yatasababisha athari hasi na chanya katika dini ya Kikristo.
- c. Kubainisha kama swala la matumizi ya Sheng katika dini ya Kikristo litasababisha mgogoro baina ya wapenda Sheng na wasiopenda Sheng, na hivyo basi kuzua makundi mawili kinzani katika dini ya Kikristo.
- d. Kutathmini kama matumizi ya Sheng katika dini ya Kikristo yatafifilisha hadhi, malengo na makusudio ya dini hii, na hivyo basi kuioanisha dini ya Kikristo na taratibu za kidunia.

1.3 Nadharia Tete

- a. Matumizi ya Sheng katika dini ya Kikristo yatazua leksimu zenyenye maana mpya isiyoleweka na wafuasi wote katika dini ya Kikristo.
- b. Matumizi ya Sheng katika sajili ya dini yatasababisha athari hasi na chanya katika dini ya Kikristo.
- c. Swala la matumizi ya Sheng katika dini litasababisha mgogoro baina ya wapenda Sheng na wasiopenda Sheng na hivyo basi kuzua makundi mawili kinzani katika dini ya Kikrisrto.
- d. Matumizi ya Sheng katika dini ya Kikristio yatafifilisha hadhi, malengo na makusudio ya dini hii, na hivyo basi kuioanisha dini ya Kikristo na taratibu za kidunia.

1.4 Sababu za Kuchagua Mada Hii.

Ari yangu ya kuandika kuhusu swala hili la utafiti imechochewa hasa na kazi za wataalamu hawa wafuatao: Iribemwangi na Mukhwana (2011), na Juoni Philip Mahu (2009). Katika kitabu chao cha *Isimujamii*, Iribemwangi na Mukhwana wanadai kwamba Sheng ni lugha ya vijana. Madai haya ya wanataaluma hawa wawili nakubaliana nayo. Katika utafiti huu, tulipata pia kubaini kwamba Sheng ni lugha ya vijana. Vijana hawa hasa huwa wale waliozaliwa au kulelewa mijini, na walio na umri wa miaka kati ya 10 hadi 35.

Juoni Philip Mahu (2009) anadai kwamba Sheng inatumiwa hasa na vijana na ni sehemu ya utamaduni pendwa sana nchini Kenya. Mwanataaluma huyu anazidi kudai kwamba lugha hii hukua kwa haraka sana. Kukua huku kunachochewa na madai kwamba maneno huingizwa na kuondolewa katika leksimu za Sheng kizazi baada ya kizazi, na majira baada ya majira. Aliyoyasema Mahu pia tuliweza kukubaliana nayo. Katika uchanganuzi wa data yetu, tulipata kubaini kwamba lugha ya Sheng ina visawe vingi sana. Sababu inayochangia kuwepo kwa visawe hivi katika lugha hii, ni kwamba maneno mengi huingizwa au kutolewa katika matumizi ya lugha hii kulingana na mahitaji ibuka ya kizazi husika.

Mitchell na Anthony (2005), katika kazi yao ya *Aleet prime* nao wanasema kwamba Sheng ni istilahi mwiko katika hotuba za kawaida zinazojumuisha watu wa matabaka ya juu au watu wenye majukumu makubwa katika jamii. Hii ni kwa sababu, misamiati ya Sheng huchukua nafasi ya istilahi sanifu na muhimu zinazostahiki kutumika katika miktadha maalum. Madai haya

kwamba Sheng ni lugha ya vijana, ni sehemu ya utamaduni pendwa nchini Kenya na kwamba ni istilahi mwiko kimatumizi katika hotuba, ndiyo yalitusukuma kuifanyia mada hili utafiti. tulichagua mada hii ili kubainisha athari za lugha hii katika asasi za kijamii hususan dini ya Wakristo. Hili lilitokana na sababu kwamba vijana ndio wanaomiliki asilimia kubwa ya Wakenya hasa wale wanaoishi mijini. Asilimia hii kubwa ya vijana vile vile inajidhihirisha katika asasi mbalimbali za jamii kama vile dini ya Wakristo. Asilimia hii kubwa ya vijana ndiyo inayojulikana kwa kuipenda na kwa kuitumia lugha hii ya Sheng katika asasi mbalimbali za jamii. Sheng ni lugha yao; ndicho kitambulisho chao katika jamii, ndiyo utamaduni wao na ndiyo lugha ambayo wao huitumias kwa kujieleza. Bila shaka vijana hawa wakiubeba na kuuingiza utamaduni huu katika dini, Basi utata wa kiasi fulani utazuka. Utata huu utatokana na tofauti baina ya tamaduni mbili zitakazotumiwa katika taratibu za kuabudu na kuafikia kaida na malengo ya dini. Na iwapo jambo hili litatokea, swalni je, wengi watapewa na kuachiwa usukani au la?

Pamoja na kutaka kuzijua athari za lugha hii katika dini, vile vile tulitaka kubaini mitazamo na maoni ya jamii kuhusu matumizi ya Sheng katika ibada za dini.

1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti.

Utafiti huu ulijikita katika mipaka ya isimu jamii na jinsi ambavyo Sheng imezua athari zilizo chanya na hasi katika asasi hii muhimu ya dini katika jamii. Katika kulijadili na kulichanganua swala hili, tulizitathmini athari chanya na athari hasi za Sheng na jinsi zinavyojitokeza na kujidhihirisha katika dini ya Kikristo. Tuliamua kuitathmini Sheng kwa sababu Sheng ndiyo lugha ambayo inatumiwa na idadi kubwa sana ya vijana katika mtaa huu. Matumizi yake yameshuhudiwa katika asasi mbalimbali za kijamii. Mojawapo ya asasi hizi ni asasi ya dini ya Kikristo. Lugha hii inazidi kukua kila kuchao, nayo idadi ya vijana vile vile inazidi kuongezeka katika mtaa wa Umoja kila kuchao.

Vile vile tuliamua kuzitathmini athari zake katika misingi ya dini ya Kikristo kwa sababu hii ndiyo dini yenyeye wafuasi wengi katika mtaa huu na nchini Kenya kwa ujumla wake. Katika mtaa huu, vijana wanaenzi matumizi ya Sheng katika kuziendesha taratibu za kumuabudu Mungu iwe makanisani, shulenii, katika makongamano au kwenye vyombo vya habari. Kunao Wakristo wasiolipenda tendo hili la kutumia Sheng katika kufanikisha shughuli hizi katika jamii. Wao

wanaichukulia Sheng kama lugha chafu na isiyofaa kutumiwa katika taratibu za kumuabudia Mungu. Labda sababu yao kuu inatokana na dhana ya Durkheim (1921). Durkheim aliitazama dini katika muktadha mzima wa jamii. Alitambua nafasi ya dini katika kuchochea fikra na tabia za wanajamii. Mwananadharia huyu aligundua kwamba katika jamii watu hujaribu kutenganisha ishara, vifaa na kaida ambazo ni takatifu ,na ishara, vifaa na taratibu za maisha ya kila siku, zinazochukuliwa kuwa zenyе makufuru. Vifaa vitakatifu mara nyingi huaminika kuwa na utakatifu ambaо huvitenga na vifaa vya kidunia. Lugha ni kifaa cha mawasiliano; ni chombo kinachoensiwa sana na jamii katika kutekeleza taratibu na kaida zake.

Lugha hujumuisha maneno yanayofaa au yasiofaa kwa matumizi katika muktadha fulani. Iwapo maneno kadhaa ya lugha fulani yatabadili maana yazo awali na labda yachukue maana mpya yenye kuleta kinyaa mbele za umma, basi neno au maneno hayo huchujwa kutoka katika matumizi ya muktadha awali na kuingizwa katika matumizi ya muktadha mpya ambaо unayafaa. Mfano mzuri wa madai haya ni neno la Kiswahili “shoga.” Hapo awali neno hili lilikuwa na maana ya “rafiki wa kike wa mwanamke fulani.” Lakini leo hii maana msingi ya neno hili yanaelekea kubadili. Neno hili sasa linatumika kwa maana ya “mwanamume aliye na tabia ya kuwaingia wanaume wengine kwa nyuma.” Nchini Kenya maana msingi ya neno hili tayari yameshamishwa na kuingizwa katika muktadha mpya wa matumizi. Hivi ndivyo mambo yalivyo kulingana na matumizi ya Sheng katika jamii. Yaani kuna watu katika jamii wanaoichukulia Sheng kama lugha ya aibu na yenye kusababisha kinyaa mbele za umma. Hivyo basi, kwao Sheng ni lugha isiyofaa kwa matumizi kama vile ya kumuabudia Mungu.

Nadharia tuliyotumia ni nadharia ya kitambulishijamii kama ilivyopendekezwa na Taifel na John Turner (1979). Nadharia hii ina vipengele muhimu vitatu. Vipengele hivi ni pamoja na;

- a) Kipengele cha ujiainishaji.
- b) Kipengele cha ujitalishaji.
- c) Kipengele cha ujilinganishaji.

Tuliamua kuitumia nadharia hii na wala siyo nyingine kwa sababu nadharia hii ndiyo inayooana vyema na mada yetu ya utafiti. Mada ya utafiti ilihuathari za Sheng katika jamii; jamii mahususi ni jamii ya dini ya kikristo. Nadharia hii nayo ina msingi wake katika jamii. Inafafanua

kwamba katika jamii kuna michakato mitatu ya kiakili ambayo wanajamii huitumia ili kuwaainisha watu wengine kama watu waliondani ya makundi yao au walio nje ya makundi yao. Katika kuijadili mada hii, nitavitumia vipengele hivi vyote vitatu ili kuonyesha jinsi ambavyo vijana hujainisha, wakajitambulisha, na kisha wakajilinganisha na makundi mengine katika jamii; makundi ambayo hayatumii Sheng na yale ambayo yanatumia Sheng katika kumuabudu Mungu. Sheng ni lugha ambayo inaonyesha kuwapo kwa lahaja za kimaeneo, kijinsia na kiumri.

Kwa sababu hii nitashughulikia athari zake kama zinavyojidhihirisha katika dini kama inavyoshuhudiwa Mashariki mwa jiji la Nairobi, mtaa wa Umoja. Sifa za Sheng katika mtaa huu ni nyingi. Kwa mfano, Sheng ndiyo lugha ambayo hutumiwa na asilimia kubwa ya vijana katika mawasiliano yao ya kila siku. Vijana pia huitumia lugha hii katika kuwasilisha kazi zao za kisanaa kama vile: uimbaji, ushairi, uchoraji, uigizaji, na katika matangazo ya kibiashara. Nimechagua Umoja kimakusudi kwa kuwa wanataluma wengi wa Sheng wanadai kuwa lugha hii ina asili yake katika mitaa ya Mashariki mwa jiji la Nairobi. Madai haya hayana ukweli wa asilimia mia moja. Ifahamike kwamba kabla ya kiwango hiki - cha madai kwamba Sheng ni lugha iliyobuniwa na vijana Mashariki mwa jiji la Nairobi- kipo kiwango kingine awali. Kiwango hiki ni cha uigaji. Noam Chomsky (1962) anadai kwamba watoto hujifunza lugha kwa kuwaiga watu wazima. Kwa kuzingatia wazo la mtaalamu huyu, basi tunaweza tukasema kwamba wazo la kuzungumza kwa lugha ya Sheng lilianza mnamo miaka ya 1940 kuendelea mbele. Katika kipindi hiki wazo hili lilijitokeza kama ubadilishanaji msimbo wala sio kama lugha. Ni katika kipindi hiki ambapo juhudzi za kupigania uhuru nchini Kenya zilianza kuota mizizi. Katika miaka hii, viongozi walioongoza juhudzi za kupigania uhuru mara kadhaa waliongea kwa kuchanganya ndimi. Mara kadhaa, maneno mengi waliyoyasema yalijumuisha maneno ya lugha zao za mama na maneno ya Kiingereza, wakiwa na nia ya kuzisetiri siri za mazungumzo yao zisije zikaelewka bayana na mkoloni. Mifano ya mazunguzo ya viongozi wa Kenya yaliyokuwa na sifa hizi ni kama ifuatayo:

- a) Jaramogi Oginga Odinga aliwahi kusikika akisema hivi, “*Kenya is marwa and no body can tunya us.*” akiwa na maana kwamba, “*Kenya ni nchi yetu na hakuna anayeweza kutunyang’anya.*” Maneno haya yalimtatiza sana mkoloni hivi kwamba hakuweza kuuelewa ujumbe uliokusudiwa moja kwa moja.

- b) Mzee Jomo Kenyatta naye alipouliwa na mwingereza hivi, “*And you, where do you come from?*” aliwajibu hivi, “*Jomokete Kenya*,” akiwa na maana ya, “*ninatoka Kenya*.”
- c) Mkoloni hakuweza kuyaolewa maneno haya ya Kenyatta moja kwa moja, kiasi kwamba alidhani kuwa aliyeulizwa anakotoka, aliishia kulisema jina lake badala ya kulijibu swali aliloulizwa. Ni kutokana na kutolewana huku ambapo jina “Jomokenyatta” linaaminika kuzalika. Aliyelizaa jina hili alikuwa Mkoloni. Hata hivyo ipo kauli nyingine inayodai kwamba jina hili “Jomo Kenyatta” lilitokana na kirai cha kiingereza, “The Burning Spear.” Kulingana na kauli hii, rais huyu wa kwanza wa Kenya alipewa jina hili na Mbiu Koinange. La msingi kueleweka hapa ni kwamba binadamu huwa na uwezo wa kuibadili historia yake kutoka kwenye kidato cha imani anachokiona kwamba kinaathiri kwa kuizusha hadhi yake na akaiweka kwenye kidato cha imani kinachoienzi na kuidumisha hadhi yake katika jamii. Yaliyoandikwa huaminika kuliko yaliyosemwa tu. Huenda ikawa kwamba hili ndilo lililotendwa na rais huyu wa kwanza wa Kenya. Yaani aliibadili historia ya chanzo cha jina lake kasha akaihifadhi historia hiyo katika maandishi ili ipate kuaminika zaidi.
- d) Wapiganiaji uhuru nchini Kenya walijulikana kama “*mau mau*.” Jina hili lilitokana na ujenzi ghairi wa neno la Kikuyu “*uma uma*,” Lenya maana ya, “*toka toka*.” Maneno haya ya viongozi hawa wetu yaliwatatiza Waingereza hivi kwamba hawakuweza kuyaolewa bayana. Wapo Waingereza ambao walikuwa wameishi na Wakikuyu kwa muda mrefu hivi kwamba waliweza kukielewa kikikuyu kwa kiwango fulani cha kuridhisha, kiasi kwamba waliweza hata kuwasiliana na wenyeji hao wao kwa kuitumia lugha hii. Lakini ujenzi ghairi huu wa neno hili “*uma uma*” uliwatatiza Waingereza kiasi kwamba hawakuweza kuelewa maana bayana ya neno hilo.

Mbinu hii ya maongezi ilizua ucheshi kwa kiwango fulani mionganini mwa jamii ya Wakenya, na hivyo basi ikazua mvuto wa aina fulani hasa mionganini mwa vijana. Vijana walivumbua kwamba, kwa kuyatumia maneno ya lugha yao au ya jamii nyingine, wao wanaweza wakaunda au wakazifinyanga leksimu ambazo huenda zikakosa kueleweka bayana na watu wa jamii fulani na hivyo basi wakawasiliana wao kwa wao bila ya jamii au watu wasiolengwa kuyaolewa mazungumzo yao. Uzungumzaji huu ultia fora sana mionganini mwa vijana katika maeneo ya Nairobi kama vile: mashariki, magharibi, kusini na kaskazini mwa jiji hilo (Nairobi) hasa

mnamo miaka ya 1980. Hata hivyo mawasiliano haya yaliishia kukita mizizi yake katika maeneo ya Mashariki mwa jiji la Nairobi kwa sababu kadhaa hasa zile zilizoegemea hali za kiuchumi za wakati huo. Hali hizi ni kama jinsi zinavyodaiwa na wataalamu kama vile Iribemwangi na Mukhwana (2011) mionganoni mwa wanataluma wengine. Kwa vile hii haikuwa mada yetu ya utafiti hatukujikita kwayo ila kwa kuigusia tu.

Athari za Sheng katika dini ya Kikristo hususan katika maeneo haya ya Umoja huenda zikawa tofauti na maeneo mengine kama vile magharibi, kusini, au kaskazini mwa jiji hili la Nairobi. Hii ni kutokana na sababu kwamba Umoja - pamoja na maeneo jirani kama vile Komarock, Kayole, na Manyanja - ni mtaa unaopatikana Mashariki mwa jiji la Nairobi, eneo linaloaminika kuwa kitovu na asili ya lugha hii ya Sheng. Hivyo basi athari za Sheng katika eneo hili huenda zikawa za kiwango cha juu au cha chini ikilinganishwa na maeneo mengine hususan ya jiji la Nairobi.

1.6 Msingi wa Kinadharia

Ili kuyaafiki malengo ya utafiti huu tulikita utafiti wetu katika misingi ya nadharia ya kitambulishijamii. Nadharia hii ilianzishwa nao Henri Taifel na John Turner (1979). Wataalamu hawa walipendekeza kwamba kunayo michakato ya kiakili ambayo huhusika katika kuwatathmini watu wengine kama “sisi” au “wao.”

“Sisi” huwa katika kategoria ya kundi ndani na “wao” huwa katika kategoria ya kundi nje.

Kundi ndani ni kundi ambalo huwa tunajitambulisha kwalo na kundi nje ni kundi ambalo huwa hatujitambulishi kwalo. Mifano ya makundi katika jamii ambayo wanataluma hawa waliyataja ni pamoja na;

- a) Rwanda : Wahutu na Watutsi
- b) Yugoslavia : Wabosnia na Wasarbi
- c) Ujerumani : Mayahudi na Wanazi
- d) Kandanda : Man United na Liverpool
- e) Jinsia : Wanawake na Wanaume
- f) Matabaka : Tabaka la juu na la chini
- g) Ireland Kaskazini : Wakatoliki na Waprotestanti

Mifano hii inajumuisha mifano ya makundi nje na makundi ndani. Tathmini hii hutendeka katika mpangilio mahususi. Wataalam hawa walipendekeza vipengele vitatu ambavyo hutumika katika kutathmini makundi nje na makundi ndani katika jamii. Vipengele hivi ni kama vifuatavyo:

- a) Kipengele cha uainishaji.
- b) Kipengele cha kujitambilisha na jamii.
- c) Kipengele cha ujilinganishaji kijamii.

1.6.1 Kipengele cha Ujiainishaji.

Katika kipengele cha kwanza ambacho ni uainishaji, wataalamu hawa wanasema kuwa, binadamu huainisha vitu ili aweze kuvielewa na kuvitambua, jinsi ambavyo huwa tunawaainisha watu. Katika kuwaainisha watu, huwa tunatumia viainishi vya kijamii kama vile weusi, weupe, Mkenya, Mkristo, Mwislamu, mwanafunzi na kiongozi. Hii ni kwa sababu viainishi hivi huwa na umuhimu fulani katika jamii.

Kama tunaweza kuwaainisha watu katika kategoria Fulani, basi jambo hili huweza kutuarifu mambo mengi kuhusu watu hao. Vile vile jambo hili hutuwezesha sisi kuelewa mambo yanayotuhusu kwa kujua kikundi tunachojitambulisha kwacho. Kikundi tunachojitambulisha kwacho ni lazima kiwe na tabia na mienendo kama yetu. La ziada ni kwamba, mwanadamu anaweza akawa sehemu ya vikundi zaidi ya kimoja.

1.6.2 Kipengele cha ujitambulishaji na jamii.

Kipengele cha pili ni kipengele cha kujitambulisha na jamii. Kuhusu kigezo hiki wataalamu hawa wanasema kuwa huwa tunatwaa kitambulisho cha kikundi ambacho tumejitambulisha nacho kama sehemu yetu. Ikiwa kwa mfano umejitambulisha kama mwanafunzi, uwezekano upo kwamba utatwaa kitambulishi cha uwanafunzi na utanza kuyatenda matendo ambayo unaamini kuwa hutendwa na wanafunzi. Mwishowe utaingiana na kaida za kikundi hicho na hadhi yako itaenzika na kudumishwa kwa sababu ya uanachama wa kikundi hicho.

1.6.3 Kipengele cha Ujilinganishaji Kijamii.

Kipengele cha mwisho ni kile cha ujilinganishaji kijamii. Baada ya kuijainisha kama sehemu ya kikundi fulani na umejitambulisha na hicho kikundi, baadaye huwa unajaribu kukilinganisha

kikundi chako na makundi hayo mengine yaliyomo katika jamii. Kama unataka hadhi yako iendelee kudumishwa, basi ni lazima ujilinganishe vyema na makundi hayo mengine. Jambo hili ni muhimu katika kuelewa madhara husika kwa sababu mara makundi mawili yanapojitambulisha kama kinzani huwa panaondokea ushindani ili wanachama wa kila kundi husika waweze kudumisha hadhi yao katika jamii.

Nadharia hii ya kitambulishijamii inaoana vyema sana na mada yetu ya utafiti. Inaoana na mada yetu ya utafiti kwa misingi kwamba, ili uwepo ukinzani kati ya makundi mawili ni lazima iwepo sababu inayochangia ukinzani huo. Kwa mfano, ili kulitathmini vyema swala hili la utafiti, hebu tujaribu kuutumia mfano huu wa makundi haya mawili kinzani ya soka.

Mfano 1

a) Kandanda : Manchester United na Liverpool

Mfano huu unatubainishia wazi kwamba kunao ukinzani kati ya timu hizi mbili za kandanda. Swalii ni: Je, ukinzani huu kati ya vikundi hivi viwili unasababishwa na nini? Chanzo cha ukinzani huu ni ligi ya kandanda ya Uingereza. Yaani, ligi hii ndiyo inayosababisha makundi haya mawili kuwa kinzani. Kwa kawaida ligi huhusisha mashindano na timu inayoibuka kuwa shindi ndiyo hutuzwa kombe la ushindi wa ligi hiyo husika. Tuzo hili huinua na kudumisha hadhi ya jina la timu husika pamoja na wanachama, wachezaji na mashabiki wa timu hiyo. Timu shindwa huhisi kufedheheka na kusononeka machoni pa jamii. Jambo hili hutendeka pia kwa mashabiki wa timu hiyo shindwa.

Vile vile katika utafiti huu, tulitarajia kutathmini kama Sheng ndiyo kisababishi cha kuwepo kwa makundi mawili kinzani katika dini ya Wakristo. Hivyo basi mfano wa kimakundi tulioibuka nao ulikuwa huu.

b) Dini: Wanaoabudu kwa Sheng na Wasioabudu kwa Sheng.

Mfano huu ulituwezesha kujua kuwa kunazo athari hasi na chanya ambazo husababishwa na matumizi ya lugha hii ya Sheng katika dini ya Kikristo. Kuwepo kwa athari hizi katika dini ya Kikristo ndiko kumechangia kuwepo kwa dhana ya kundi nje – yaani wao - na dhana ya kundi ndani - yaani sisi - kama ilivyopendekezwa na Henri Taifel na John Turner (1979).

Katika muktadha wa dhana hii, kundi ndani (ambalo ni sisi), lilikihusisha kikundi cha watu - tuseme vijana- ambao wanaielewa lugha ya Sheng. Vijana hawa basi hujaribu kujitambulisha na kujilinganisha na makundi mengine katika jamii ambayo pia huitumia Sheng kama lugha yao ya mawasiliano katika jamii. Vile vile, vijana hawa wa jamiilugha ya Sheng hujaribu kuhakikisha kwamba wanapewa nafasi ya kuitumia Sheng katika kuakisi na kufanikisha matakwa yao ya kijamii kokote waendako na popote wajipatapo. Hali hii hutokana na sababu kwamba Sheng ni kitambulisho chao kama vijana na kwao, si vyema kukiacha kitambulisho chao nyuma. Na iwapo jambo kama hili litawatokea (yaani wakilazimika kutoitumia Sheng katika muktadha fulani kama vile wa ibada) basi huenda hadhi yao ikaathiriwa na hatimaye ikashushwa na kuangamizwa katika jamii. Mwishowe kikundi hiki (cha jamiilugha ya Sheng) kitajiona kama kilichodunishwa na kunyang'anywa hadhi yacho.

Kama ambavyo tumeona hapo juu, hakuna kikundi ambacho hupenda kufikwa na jambo kama hili. Ni kutokana na hali kama hii ambapo kila kikundi hujaribu kupigana ili kudumisha na kuendeleza hadhi na nafasi yake katika jamii. Na kwa misingi hii basi, hivi ndivyo mambo yalivyo katika himaya hii ya dini. Wale wanaopenda na kuienzi Sheng kama kitambulishi chao hujaribu juu chini kuona kwamba wamekubaliwa kuitumia lugha hii katika taratibu angalau zote za kidini. Wao wakifaulu kwa hili basi kulingana nao, hadhi na heshima zao zitaendelea kudumishwa na kuendelezwa katika jamii - hasa ya dini - kizazi baada ya kizazi.

La ziada ni kwamba, vijana hawa – wa jamiilugha ya Sheng - huvitumia vigezo vile vitatu ambavyo tumevijadili katika misingi ya nadharia hii katika utenda kazi wao wa kijamii. Kwa misingi ya vigezo hivi, vijana hawa huweza kuijainisha kama vijana waongea Sheng; huweza kujitambulisha na vijana wengine ambao pia huiongea Sheng, na hatimaye, wao kama vijana wa jamiilugha ya Sheng huweza kujilinganisha na makundi mengine katika jamii ambayo aidha huwa wanajamiilugha ya Sheng au wanajamiilugha ya dini ya Kikristo. Kundi hili lisiloongea Sheng hasa huwa la watu wenye umri wa juu. Watu hawa ni kama vile: madaktari, wazazi, walimu, na viongozi. Kundi hili la wasioongea Sheng pia hujitathmini kwa misingi ya vigezo hivi vitatu vile vile, ili kuijainisha kama kundi la wasioongea Sheng. Ujilingaishaji huu hatimaye ndio huzua utata na migogoro baina ya makundi haya mawili. Kimsingi, kichocheo cha utata na migogoro hii huwa lugha. Aidha, lugha ambayo hutumiwa na kikundi kimoja huwa chukizo au isiyoeleweka na kikundi hicho kingine. Hii ndiyo nadharia tulioitumia katika utafiti huu kwa

sababu ilitufaa zaidi katika kuvichambua vipengele vinavyooana na swala la athari za Sheng katika dini ya Kikristo.

1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada Hii.

Wataalamu ambao wameandika kazi zinazohusu Sheng ni wengi. Kazi ambazo wataalamu hawa wameziandika kuihusu Sheng zimeegemea taaluma zao za kisoshiolojia, anthropolojia, na isimu kwa asilimia kubwa. Sisi kama wana isimu jamii, utafiti wetu ulilenga kukita katika taaluma ya isimujamii peke yake. Katika kiwango hiki tulilenga kutathmini athari za Sheng katika dini ya Kikristo. Ari hii yetu ilichochewa na ukweli kwamba, mionganoni mwa wanaisimujamii wengi ambao wamezungumzia Sheng, hakuna wale ambao wamezungumzia athari za lugha hii katika asasi za jamii kama vile dini. Hata hivyo ukweli huu haukutufanya tuyapuuze yote yaliyoandikwa kuhusu Sheng ingawaje hayakuhusiana moja kwa moja na mada yetu ya utafiti. Hivyo basi tuligusia kazi kadhaa za wataalamu hawa ili kuonyesha misimamo na maoni yao kuihusu lugha hii ya Sheng.

1.7.1 Lugha ya Sheng.

Mazrui (1995) anadai kwamba Sheng ni msimbo wa vijana. Anazidi kusema kwamba msimbo huu ulianza mionganoni mwa vijana waliotoka katika jamii zenye mapato duni kiuchumi na walioishi katika mitaa ya mabanda iliyoko mashariki mwa jiji la Nairobi.

Haipothesia hii inaendelea kusema kwamba vijana walioishi na kulala katika nyumba yenye chumba kimoja cha kulala walibuni msamiati wa siri ili wazazi wao ambao pia walilala katika chumba hicho kimoja wasiyaelewe mazungumzo yao. Maoni kama haya pia yanatolewa na wataalamu kama: Osinde (1986), na Abdulaziz na Osinde (1997).

Kembo –Sure (1992), pia ana msimamo wenye maoni kama haya. Anasema kuwa Sheng ni msimbo wa vijana wa rika moja. Abdulaziz na Osinde wanadai kwamba Sheng ilianza katika miaka ya sabini. Nao Mazrui na Mpande (1990) na Mazrui (1995) wakiwa wanamnukuu Michael Ngugi wanasema kuwa Sheng ilianza mnamo miaka ya thelathini. Madai haya yanatokana na mifano ya leksimu za Sheng anazotoa Karanja kwa kusema kwamba lugha hii ilianza mionganoni mwa wezi wa mifukoni kama msimbo wao wa siri.

Spyroulos (1987:13), naye kwa upande wake anasema kwamba Sheng ilianza mnamo miaka ya hamsini na kutia fora katika miaka ya sabini. Jambo lililomchochea Spyroulos kusema hivyo ni kutokana na sababu kwamba, maandishi mengi katika makala ya majarida na katika magazeti yaliyohusu Sheng, yalianza kushudiwa mnamo miaka ya sabini. Hata hivyo madai haya bado hayana maana kwamba huu ndio ulikuwa mwanzo wa Sheng. Mtaalamu huyu alikisahau kitengo cha uigaji jinsi kiliviyotangulizwa na Chomsky. Mtu huijua na kuizungumza lugha kutokana na uigaji. Vijana wanaoizungumza Sheng leo hii, wamewaiga au waliwaiga wazungumzaji wengine waliowatangulia.

Madai hayo tofautitofauti yanayohusu asili na chimbuko la Sheng labda ndiyo yanayomwongoza Ngesa (2000) kudai kuwa hakuna asili moja ya lugha ya Sheng.

Kunao wataalamu ambao wanatazama Sheng kama lugha ya msimu. Miiongoni mwa wataalamu hawa ni Iribemwangi na Mukhwana (2011). Lakini hebu tujiulize swalii hili; Lugha msimu ni lugha gani? Lugha msimu ni lugha ambayo hujikita katika msimu fulani na huaminika kutoweke baada ya msimu huo kutamatika. Lugha msimu hutumia mbinu za kiusemi ambazo huwatambulisha watu na kuwafanya kuhisi kuwa na mshikamano wa umoja. Majukumu ya lugha msimu huwa ya kisaikolojia na ya kijamii. Asili na chimbuko la lugha msimu, li katika nchi ya Marekani hasa miiongoni mwa Wamarekani weusi. Mazrui (1995) anasema kuwa Wamarekani weusi waliopelekwa marekani waliishia kuwa huru baada ya utumwa kupigwa marufuku. Wamarekani hawa weusi baadaye walianza kubaguliwa kwa misingi ya rangi. Wao walinyanyaswa sana na hata wakanyimwa haki zao. Jambo hili liliwabidiisha kubuni leksimu zilizoakisi hali ya unyonge wao wa kimaisha. Leksimu hizi zilienea sana miiongoni mwa Wamarekani hawa Weusi. Baadaye leksimu hizi zilipata kueleweka na Wamerikani Weupe waliotoka kwenye jamii zenye uwezo wa kiuchumi. Pindi Wamerikani hawa Weusi walipogundua jambo hili, nao walibadili leksimu ili wazidi kujitambulisha na kutengana na Wamarekani weupe waliokuwa na uwezo wa kiuchumi. Lugha hii ya Wamerikani hawa Weusi ilikuwa lugha ya msimu kwa sababu ilibadilika badilika kileksimu kadri mateso yao yalivyozi kukiithiri. Ni vyema kueleweka hapa kuwa kubadilika huku kwa leksimu hakukuwa na maana ya kubadilika kwa hali ya Wamarekani Weusi hawa kiuchumi. Hii ilikuwa tu kama njia ya weusi hawa kuasi na kujitenga na Wamerikani Weupe wenye uwezo wa kiuchumi. Hali hii inapolinganishwa na Sheng haileti uwiano wowote; na kama upo, basi ni finyu mno. Mazrui

(1995) anasema kuwa Sheng ni lugha msimu inayohusishwa na vijana wanaotoka katika jamii yenyе uwezo mdogo wa kiuchumi na wanaoishi katika jiji la Nairobi. Misingi hii ndiyo inayomfanya mtaalamu huyu adai kwamba Sheng ni lugha inayowatenga wale wenye uwezo wa kiuchumi na wale wasio na uwezo wa kiuchumi. Lakini ukweli wa mambo ni kuwa hata wale walio na uwezo wa kiuchumi huizungumza Sheng. Sheng ambayo wao huizungumza huwa imeja leksimu za Kiinereza kuliko leksimu za Kiswahili. Ni kutokana na sababu hii ambapo tunasema kuwa Sheng si lugha msimu. Maoni yetu ni kwamba, Sheng ni lugha ambayo imelemaa. Ni lugha ambayo haina uwezo wa kukua hadi ikafikia kilele cha ukomavu, na hivyo basi ikawekewa sheria na kanuni za kisarufi kama vile Krioli na Pijini. Sababu kuu ni kwamba, lugha hii hukua na hubadilikabadilika kila uchao, na wala malengo yake sio sawa na yale ya lugha hizo mbili ambazo tumezitanguliza hapo juu.

Madai mengine yanasema kuwa Sheng ni ubadilishanaji msimbo. Ubadilishanaji msimbo huwa tukio la kutumia lugha mbili au zaidi katika mazungumzo au maandishi kwa kubadili neno, sentensi au kirai katika tukio la usemi. Mazrui (1995) anasema kwamba Sheng ni lugha ambayo kimsingi imekita kaida zake katika ubadilishanaji misimbo baina ya lugha ya Kiswahili na Kingereza. Jambo hili si kweli. Lugha ya Sheng haina misingi yake katika lugha ya Kiswahili na Kingereza tu; misingi yake pia imo katika lugha za kienyeji kama vile Kiluhya, Kikisii, Kimeru, Kikuyu, Kikamba, Kimaasai na Kikalenjin. Filip Mahu (2009) amehusisha Sheng na makundi yenyе kutenda mambo mabaya na yaliyo kinyume na maadili ya jamii. Makundi haya ni pamoja na makundi ya wezi, wanyanganyi, wabakaji, waraibu na walanguzi wa dawa za kulevyu, makahaba na walaghai.

Mitchell na Anthony (2005) wanasema kuwa Sheng ni istilahi mwiko katika hotuba za kawaida zinazojumuisha watu wa matabaka ya juu (watu wenye majukumu ya kiserikali na kiofisi). Sababu ya kusema haya ni kuwa leksimu za Sheng huchukua nafasi ya leksimu sanifu na muhimu zinazostahiki kutumika katika miktadha maalum.

Mtazamo wa mwanataluma huyu ambao unaihusisha Sheng na sifa zilizo mbaya katika jamii, tuliuunga mkono. Kwa hivyo, si vyema basi lugha yenyе sifa kama hizi kuchanganywa na lugha ya dini; lugha ambayo inaaminika kuwa na sifa nzuri kwa malengo na matarajio ya kumwabudu Mungu na kuzitenda kaida za dini takatifu ya Kikristo. Kila kitu duniani huwa na mipaka na sheria zake ambazo hukiongoza katika kuafiki malengo yake ya kuwepo hapa duniani. Na iwapo

mipaka na sheria zinazokiongoza kitu hicho zitalegezwa au kuondolewa, basi athari kadha wa kadha katika utenda kazi wa kitu hicho zitashuhudiwa. Hivi ndivyo ilivyo lugha ya dini. Kuwapo kwa Sheng katika lugha hii bila shaka kumesababisha athari kadhaa.

1.7.2 Dini

Dhana ya kisosholojia ya dini ni dhana ambayo kimsingi imezungumziwa kwa kina na Durkheim (1921). Durkheim aliitazama dini katika muktadha mzima wa jamii na akatambua nafasi yake ya kuchochea fikra na tabia za wanajamii. Durkheim aligundua kwamba watu hujaribu kutenganisha ishara, vifaa na kaida ambazo ni takatifu na ishara, vifaa na taratibu za maisha ya kila siku, zinazochukuliwa kama zenye kukufuru. Vifaa vitakatifu mara nyingi huaminika kuwa na utakatifu ambao huvitenga na vifaa vya kidunia. Hata katika tamaduni zilizoendelea, watu huzidi kuvitazama vifaa vitakatifu kwa hisia za kumbukumbu na heshima hata kama hawaamini kwamba vifaa hivyo vina nguvu za kipekee

Durkheim pia alidai kwamba dini huwa haijihusishi tu na imani, lakini pia huzingatia kaida na sheria za kila mara katika upande wa kikundi cha waumini, ambao hujenga na kuimarissha hisia za umoja. Kaida huwa muhimu kwa kuwaunganisha wanachama wa kikundi cha dini na hukubali mtu binafsi kuiondokea mitazamo ya kidunia ya kila siku na kuingia katika maeneo ya juu ya tajriba za dini. Kaida na sherehe takatifu mara nyingi huwa na umuhimu katika kutekeleza matukio kama vile ya kuzaliwa, ndoa, wakati wa matatizo na vifo. Nadharia ya Durkheim ya Dini inajitenga na jinsi ambavyo wanaumuundo hutathmini matukio ya kijamii. Kulingana na Durkheim, watu huiona dini kama inayochangia maendeleo ya kijamii kwa jumla. Kwa misingi hii basi dini hufanya kazi ya kushikamanisha wanajamii kwa kuwaongoza katika kukiri kaida na imani zao kila wakati.

Durkheim alitabiri kwamba ushawishi wa dini ungedidimia kadri ambavyo jamii ingezidi kuijimarisha kiuchumi. Aliamini kwamba mawazo ya kisayansi yatachukua nafasi ya mawazo ya kidini na watu wataanza kuzipuuza kaida na sherehe za kidini. Pia aliona kwamba dhana ya ‘Mungu’ inaelekea kuangamia. Badala yake, alikuwa na maoni kwamba jamii itakuza na kuimarissha dini ya kiserikali. Dini hii itatkuza mambo kama vile sherehe za kiserikali, magwaride na uzalendo. Taratibu hizi za kiserikali zitachukua nafasi ya ibada za kanisa. Iwapo dini za kijamii zitaendelea, basi hilo litafanyika tu kwa kusudi la kuhifadhi mshikamano wa

taratibu za kijamii. Maelezo haya ya Durkheim yatakuwa na mchango mkubwa sana katika mada hili yetu ya utafiti. Sababu ni kwamba, Sheng kama lugha, ni chombo au kifaa cha mawasiliano. Hata hivyo kifaa hiki si kitakatifu, kulingana na tathmini na misingi ya dini ya Kikristo. Sababu ni kwamba Sheng inahusishwa na sifa au mambo mabaya katika jamii. Mfano mahususi - wa sifa hizi mbaya – ni kuwa, Sheng hutumiwa na makundi mabaya katka jamii kama vile wevi, wauzaji wa mihadarati na makahaba.(Filip Mahu 2009).

1.8 Njia za Utafiti.

Katika utafiti huu, tulizitumia njia zifuatazo:

1.8.1 Ukusanyaji Data

Kwa kiwango kikubwa, utafiti huu ulifanyika nyanjani. Huko nyanjani, tulitumia mbinu mbili za ukusanyaji data. Mbinu hizi ni pamoja na hojaji na mahojiano ya moja kwa moja.

Tuliihoji idadi ya Wakristo kumi na watano: wanawake saba na wanaume wanane. Idadi hii ilijumuisha wanaume kwa wanawake ambao wamekuwa wakiishi katika mtaa wa Umoja angalau kwa muda wa miaka kumi na kuendelea. Umri wao ulikuwa kati ya miaka 31 hadi 50. Watu wenye umri huu huwa wameanza kutulia kutoptana na purukushani za maisha. Wao huwa wameanza kujitenga na mambo kadhaa ya kidunia wanayoamini kuwa ni ya kipuzi, ya kitoto au yenyе kuwalettea fedheha. Mojawapo ya mambo haya ni matumizi ya lugha ya Sheng. Tuliwajumuisha wahusika ambao wamesoma na wale ambao hawajasoma. Data yetu tuliiinakili kwa maandishi kwenye kitabu na karatasi lenye maswali husika. Data hii ndiyo tuliyoitumia katika kuchanganua, kutathmini na kuishughulikia mada yetu ya utafiti. Yani uchambuzi wa data hii ndio uliotusaidia katika kuziththmini athari za Sheng katika eneo letu mahususi la utafiti. Tuliwaacha nje watu wenye umri wa miaka 51 na kuendelea kwa sababu kupata habari za kuaminika kutoka kwao huwa swala lenye changamoto kadha wa kadha.

Katika hojaji yetu, tuliwashirikisha watu kumi na watano vile vile. Idadi hii ilijumuisha wasichana saba na wavulana wanane. Wahusika wote walikuwa aidha wanasoma, wamemaliza kusoma au wanafanya kazi. Wote hawa walikuwa wale ambao wameishi katika mtaa wa Umoja kwa muda wa miaka kumi na kuendelea.Umri wao ulikuwa kati ya miaka 12 hadi 30. Hii ni kwa sababu idadi kubwa ya watu wanaozungumza Sheng inapatikana katika kategoria hii kiumri.

Vijana wenyе umri wa miaka kati ya 12 hadi 30 huwa katika Shule za Msingi, Sekondari, Vyuo vya Anuai, Vyuo Vikuu au wanafanya kazi. Umri huu ndio unaoaminika sana katika kuienzi na kuitumia Sheng hasa katika maeneo yao ya elimu, ibada na sehemu za umma. Tuliwaacha nje watoto wenyе umri chini ya miaka 12 kwa sababu, kwa kiwango kikubwa wao huwa hawana uelewa dhabiti unaohusiana na lugha. Wao huweza kuchanganya leksimu za lugha mbalimbali bila ya kufahamu lugha mahususi inayozimiliki leksimu hizo. Mbinu tumiwa kwao huwa uigaji.

1.8.2 Uchanganuzi wa Data.

Baada ya kuikusanya data, tuliichanganua kwa misingi ya nadharia ya kitambulishi jamii. Katika kuichanganua data hii tulikita katika mbinu ya ujainishaji, ujitambulishaji na hatimaye ujilinganishaji. Kufanya hivi kulitusaidia katika kuzikubali haipothesia tulizozibuni. tumeichanganua data hii kwa kuiambatanisha na mifano mahususi ili kuithibitisha mada yetu ya utafiti. Mhimili mkuu wa uchanganuzi wetu ulikita katika hojaji na mahojiano ya ana kwa ana. Matokeo ya utafiti huu yamewasilishwa kwa njia ya hisabati na tarakimu.

1.9 Umuhimu wa Utafiti Huu.

Utafiti huu utapeleka mbele mitazamo na maoni yanayoihusu lugha ya Sheng hasa katika mawanda ya athari zake katika jamii. Wataalamu, Wanataluma na walimu katika Nyanja mbalimbali za kielimu na kitaaluma wametoa michango na maoni tofautitofauti kuhusiana na lugha hii ya Sheng. Kuna wale ambao michango na maoni yao ni hasi na kunao ambao michango na maoni yao ni chanya. Nayaunga mkono maoni na michango ya makundi yote haya mawili. Sababu ni kwamba waliyoyasema yote yana umuhimu mkubwa sana katika nyanja hii ya elimu. Pamoja na hayo, ni vyema ieleweke kuwa malengo ya Sheng katika mawasiliano ni tofauti kabisa na malengo ya lugha zingine zilizowahi kuchimbuka na kutumika katika mawasiliano kama vile Krioli na Pijini. Malengo ya Sheng yanahusishwa (kwa kiwango kikubwa) na sifa mbaya katika jamii. Miongoni mwa sifa hizi mbaya ni pamoja na uhifadhi wa siri za mazungumzo baina ya watu au makundi husika ili mazungumzo yao yasipate kueleweka na wale wasiolengwa. Hivyo basi atakayeisoma kazi hii atapata kuzielewa vyema athari za lugha hii katika dini ya Kikristo. Ufahamu huu huenda ukamwongoza katika kuifanyia mada hii utafiti wa kina zaidi, hasa kwa kuvishughulikia vipengele muhimu zaidi ambavyo huenda ikawa sikuweza kuvishughulikia katika utafiti huu.

SURA YA PILI

2.0 UUNDAJI WA LEKSIMU ZA SHENG

Utangulizi

Swala la Sheng ni swala ambalo kwa hakika limevitawala vinywa vyta wataalamu, wasomi na wanataalamu wengi kwa muda mrefu sasa. Wataalamu wote hawa wamekuwa wakiyatoa madai yanayo hitilafiana kuihusu lugha ya Sheng. Kati yao kuna wale walio na msimamo kwamba Sheng si lugha kwa sababu haina jamii wala mfumo wa kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na hata kisemantiki unaojibainisha. Kwa sababu ya ukosefu wa viwango hivi muhimu vyta muundo wa lugha, basi inakuwa vigumu kwa wataalamu husika kuiai nisha Sheng kama lugha na kuiwekeea sheria za utenda kazi wake. Wale wanaoamini kwamba Sheng ni lugha wanafanya hivyo kwa madai kwamba Sheng inao uwezo wa kufanikisha mawasiliano miongoni mwa jamii husika. Madai haya ndiyo tunayoyaunga mkono. Tunayaunga mkono kwa sababu lugha yoyote ele hufaulu kuitwa lugha iwapo ina uwezo wa kufanikisha mawasiliano miongoni mwa jamiilugha husika. Sheng inayo sifa hii ya msingi. Ufuatao ni mfano wa mawasiliano kati ya wanajamiilugha ya Sheng.

Mfano 1

Sheng: X. Joni, buda ameishia chach?

Y. Du! Ameishia ndonyo na mathee.

Tafsiri: X. John, baba ameenda kanisani?

Y. La! Ameenda sokoni na mama.

Mfano huu unatudhihirishia kwamba mhusika X na Y waliweza kuwasiliana katika mazungumzo yao. Hili linathibitishwa na ukweli kwamba X alimwuliza Y swalii, naye Y akamjibu.

Mawasiliano haya yalitendeka katika misingi ya lugha ya Sheng. Hivyo basi Sheng ina uwezo wa kufanikisha mawasiliano mongoni mwa wanajamiilugha wake.

Sasa swali ni hili: Je, Sheng ina jamii? Kabla ya kulijibu swali hili ilikuwa vyema kwetu kwanza kuelewa maana ya neno “Jamii.”

Buliba na wengine (2011: 28) wanatoa fasili ya neno “Jamii” kwa kusema kuwa:

“Jamii ni kikundi cha watu wanaoishi katika mazingira sawa ya kijogrofia na ambao kupitia kwa kazi zao, dini zao, au njia zao za maisha, au vyote kwa pamoja, hupewa umoja wanapojilinganisha na vikundi vingine vya watu.”

Kamusi ya Oxford Advanced Learners Dictionary (2010: 1414) durusu la 8, nayo inafasiri neno jamii kwa kusema kwamba;

“Jamii ni watu kwa jumla wanaoishi pamoja katika eneo maalum. Ni kikundi cha watu ambao huja pamoja kwa sababu ya kusudi fulani mahususi.”

Kulingana na fasiri hizi, jambo bayana linalojitokeza ni kwamba jamii ni kikundi mahususi cha watu wanaoishi katika eneo moja maalumu na wanaoshiriki changamoto sawa za kimaisha. Mhimili mkuu wa jamii yoyote ile huwa lugha yao. Jamii husika huitumia lugha ili iweze kuwasiliana kwa ajili ya kufanikisha na kuendeleza kaida za maisha yao ya kila siku.

Fasiri hizi vile vile zilituwezesha kufahamu kwamba Sheng ina jamii. Je, jamii ya Sheng ni jamii gani? Iribemwangi na Mukhwana (2011:115), wanadai kwamba Sheng ni lugha ya vijana. Wataalamu hawa wawili wanazidi kudai kwamba asili ya lugha hii ni maeneo ya makaazi duni mashariki mwa jiji la Nairobi. Mitaa hasa inayohusishwa na chimbuko la lugha hii ni pamoja na Kaloleni, Bahati, Shauri Moyo, na Jericho. Jambo lililowachochea na kuwasukuma vijana hawa kuanza kuzungumza na kuwasiliana kwa lugha yenyе usiri ni umaskini. Umaskini huo uliwalazimu vijana hawa kuishi na kulala katika nyumba moja yenyе chumba kimoja cha kulala na wazazi wao. Hali hii iliwachochea vijana hawa kutafuta na kubuni lugha ambayo kwayo, wangeweza kuwasiliana bila ya wazazi wao kuyaelewa mawasiliano hayo yao.

Lugha ya Sheng ni lugha ya vijana, hasa vijana wanaoishi mijini. (Iribemwangi na Mukhwana, 2011:124). Lugha hii hujibainisha kwa hili hasa pale ambapo huwa inawatema nje watu

waliovuka mipaka ya umri wa kuitwa vijana. Je, lugha hii hufaulu vipi katika kulitenda hili? Lugha hii hujiumbua na kujiumba upya kila kuchao. Vile vile huwa inabadilisha badilisha leksimu zake mara kwa mara. (Joun Fillip Maho 2009: wikipedia). Ukengeushi huu ndio ambao huifaulisha lugha hii kuwatema nje wale waliovuka umri wa kuitwa vijana na kuwaalika ndani wanajamii wapya. Wale walioafiki umri wa kujiunga na jamii hii huingia ndani huku wakiwa wamejihami kwa leksimu mpya zisizoleweka bayana na wale waliotemwa nje. Hali hii ndiyo huchangia kuwepo kwa visawe vingi katika lugha hii ya Sheng. Tazana mfano huu wa visawe vinavyomrejelea msichana:

Mfano 2

Msichana: manzi, msupa, mrembo, totois, nguna, dem, mama, mshi, shore, mbus, atoti.

Tazama mfano huu katika sentensi:

Mfano: 3

Sheng awali: Mamnzi wa kitambo walikuwa wanajidoo sana.

Sheng leo: Mambus wa bafoo walikuwa wanajidai sana.

Tafsiri: Wasichana wa zamani walikuwa wakiringa sana.

Jambo hili vile vile huiendeleza na kuikuza sifa nyingine ya lugha hii ambayo ni ufichaji na uhifadhi wa siri miongoni mwa jamii husika, yaani jamii ya Sheng. Aliyechujwa kutoka jamiilugha ya Sheng alichujwa pamoja na leksimu zake za Sheng alizokuwa akizijua, na aliyealikwa ndani ya jamiilugha hii, aliingia na leksimu zake mpya asizozielewa yule aliyechujwa. Na hivi ndivyo lugha hii hujibainisha kama sio lugha tu bali lugha ya vijana.

Sifa nyingine muhimu ambayo huibainisha na kuitofautisha lugha hii na lugha zingine ni sifa ya kimofolojia ya uundaji wa maneno. Je, mofolojia ni nini?

“Mofolojia ni tafsiri ya neno la Kiingereza “Morphology” lakini asili kamili ya neno hili ni lugha ya kiyunani. Katika lugha ya Kiyunani, neno hili liliandikwa kama “morph” likiwa na maana ya muundo au um. (Aurbuch na wengine 1971: 106).”

Kutokana na maelezo haya, tunapata kuelewa kwamba mofolojia ni utanzu wa isimu, ambao hushughulikia miundo ya maneno. Pia wapo wataalamu wengi ambao wamewahi kutoa fasiri mbalimbali za neon,’neno. ’

Neno ni kipashio cha kiisimu kinachoundwa na mofimu moja au zaidi. (Habwe na Karanja, 2012: 71) Kamusi sanifu ya isimu na lugha (1990: 58), nayo inasema kuwa; “*Neno ni silabi au mkusanyiko wa silabi zinazotamkwa au kuandikwa na kuleta maana.*”

Kutokana na maelezo ya fasiri hizi mbili, tunapata kufahamikiwa kwamba, neno ni kipashio kidogo cha kiisimu ambacho hubeba maana ya kileksika au maana ya kisemantiki. Tazama mfano huu:

Mfano 4

Sheng: Mbuyu.

Tafsiri: Baba.

Kutokana na mfano huu, tunapata kuelewa kwamba, neno “mbuyu” katika lugha ya Sheng lina maana ya mzazi wa kiume “baba.”

Je, uundaji wa maneno ni nini?

Jefwa, M. (2010: 49) anasema kuwa uundaji wa maneno ni:

“*Uambatanishaji wa mofimu moja au zaidi hadi kufikia kiwango cha mofimu hiyo au hizo kuleta maana kileksika katika lugha yoyote ile.*” Mtaalamuy huyu anazidi kwa kusema kuwa: “*lugha ikiwa chombo chenye uhai, haiachi kukua. Hali hii ya kukua kwa lugha hutokana na mambo mengi yatendekayo katika jamii. Mambo haya ni kama vile: uvumbuzi wa kisayansi, ukopaji na hata ubunifu wa maneno mapya.*” Kulinga na mtaalamu huyu, Mbinu za kimofolojia zitumikazo katika uundaji wa maneno katika lugha za ulimwengu ni pamoja na:

Unominishaji, ukopaji na utohozi, uhulutishaji, ujenzi ghairi, ukatizaji, akronimu, uambatanishaji na uambishaji.

Kati ya mbinu hizi za uudaji wa maneno, lugha ya Sheng kimsingi inatawaliwa na mbinu mbili kuu za uundaji wa maneno. Mbinu hizi ni ukopaji na utohozi na ubunifu wa leksimu. Mbinu hizo zingine za uundaji wa maneno katika Sheng hasa hutegemia mbinu ya ukopaji na utohozi.

Uundaji huu wa maneno haya ya Sheng ndio huwa chanzo cha chimbuko la kutolewana kati ya wafuasi wa dini ya kikristo wanaolewa Sheng na wale wasioilewa Sheng. Kutolewana huku hasa hushuhudiwa katika maeneo kama vile: nyumbani, shulenii, makanisani, makongamanoni na hata kwenye vyombo vya habari kama vile redio na televisheni. Ifuatayo ni mifano ya mbinu za uundaji wa maneno katika lugha ya Sheng jinsi tulivyobaini katika utafiti wetu.

2.1 Ukopaji na Utohozi

Ukopaji ni hali inayojumuisha uhamishaji wa kipashio fulani kutoka lugha moja na kukiingiza katika lugha nyingine. Kwa hivyo, kuna lugha changizi na lugha pokezi. (Jefwa, 2010: 49).

Hock na Joseph (1996: 28), wanasema kuwa ukopaji ni uhamishaji wa leksimu mahususi au set ya leksimu au faridi fulani kutoka lugha moja au lahaja moja hadi nyingine. Kuna aina mbili ya ukopaji : ukopaji sisisi na ukopaji tohozi. Ukopaji sisisi ni pale ambapo leksimu fulani inahamishwa kutoka katika lugha changizi hadi lugha lengwa bila ya kufanyiwa marekebisho yoyote. Ukopaji tohozi nao hutokea pale ambapo neno limelokopwa hufanyiwa uhawilishaji ili lichukue muundo wa kimofolojia wa lugha kopa. Iribemwangi na Mukhwana (2011: 157) nao wanafasiri maana ya neno utohozi kwa kusema kuwa utohozi hutokea pale ambapo leksimu imekopwa kisha ikafanyiwa marekebisho ya kifonolojia, kimofoloji au kisemantiki ili ifuate kanuni na muundo wa lugha kopaji. Kuhusu uhawilishaji, Matthews (1997:7) anasema kuwa uhawilishaji hutokea pale ambapo leksimu zinabadilishwa ili kuakisi mfumo wa kisauti wa lugha kopa.

Arlotto (1972:184) naye ana maoni kwamba baada ya ukopaji leksimu kopwa hupatiwa uasilia wa lugha kopa. Ni katika kupokea uasilia wa lugha kopa ndipo uhawilishaji hufanywa. Lugha kopeshi nayo huwa haipotezi neno hilo lililokopwa na lugha nyingine. Hartman na Stork (1972:29) nao wana maoni kwamba wakati mwingine leksimu iliyokopwa huhawilishwa. Ubayana wa maelezo ya wataalamu hawa ni kwamba uhawilishaji huwa sio jambo la lazima katika ukopaji wa leksimu.

Fronkin na Rodman (1988:309) pia wana maoni kuwa lugha zote ulimwenguni hukopa msamiati. Hivyo basi misamiati hujumuisha leksimu asilia na leksimu mkopo. Ukopaji ni mbinu ya uundaji wa maneno ambao kwa kweli umetajirisha sana lugha za ulimwengu . Miiongoni mwa lugha ambazo zimefaidi kutokana na mbinu hii ya uundaji wa maneno ni Kiswahili na Sheng. Kiswahili kina maneno mengi sana yaliokopwa kutoka katika lugha kama vile Kiarabu Kijerumani Kiajemi na Kiingereza. Sheng pia imeziiga sifa hizi za Kiswahili kwa kukopa maneno kutoka kwa lugha kama vile Kiingereza, Kikuyu Kiswahili Kifaransa na lugha zingine za kienyeji kama vile Kidholuo na Kiluhya. Ufuatao ni mfano wa maneno ya Sheng yaliyokopwa kutoka katika lugha ya Kiingereza, Kiswahili, Kikuyu pamoja na lugha zingine kama vile Kifaransa, Kidholuo, na Kiluhya.

2.1.1 Ukopaji na Utahozi: Maneno ya Kiingereza

Kimsingi chimbuko la lugha ya Kiingereza ni nchi ya Uingereza. Wazungumzaji asiia wa lugha hii huitwa waigereza. Leo hii, lugha ya Kiingereza inazungumzwa katika mataifa mengi duniani kote. Lugha hii vile vile inatumika kama lugha ya mawasiliano karibu duniani kote. (Oxford Advanced Learners Dictionary 2010:486).

Nchini Kenya lugha ya Kiingereza ilitangulizwa na wakoloni na wamishonari kabla ya vita vya kwanza na vya pili vya ulimwengu. Jambo hasa lililochocha lugha hii kukita mizizi nchini Kenya ni kutokana na sababu kwamba, Wamishonari waliitumia lugha hii sana katika shughuli zao za kuieneza injili na dini ya Kikristo. Vile vile hii ndio lugha ambayo ilitumiwa na Wamishonari katika kuwasiliana na kuwaelekeza wanafunzi katika shule zao za kimishenari. Hali hii iliwabidi watoto pamoja na walimu wa kiafrika kuijua lugha hii ya Kiingereza ili waweze kufahamu vyema maelezo yaliyokuwa vitabuni pamoja na maelekezo yaliyotolewa na wamishonari hao katika mafundisho yao. Matokeo ya hali hii yalikuwa kwamba Waafrika wengi waliofuzu kutoka katika shule hizi za wamishonari walikuwa na uwezo wa kuongea Kiingereza kwa ufasaha.

Vile vile baada ya nchi ya Kenya kupata uhuru kutoka kwa Mwingereza mnamo mwaka wa 1964, rais wa kwanza wa jamhuri ya Kenya, Mzee Jomo Kenyatta aliitangaza lugha ya kiingereza kama lugha rasmi. Matokeo ya tangazo na amri hiyo ya rais yalikuwa kwamba

Kiingereza kilipewa hadhi ya juu nchini kuliko lugha nyinginezo (kikiwemo Kiswahili pamoja na lugha za kiasili). Kwa misingi hii, lugha ya Kiingereza ndiyo iliyotambuliwa kama lugha faafu kwa matumizi ya elimu shuleni, katika mikutano na taratibu zote za kiserikali na pia katika mawasiliano yote ya kimataifa. Jambo hili bado linatendeka hadi leo hii, mighairi ya Kiswahili (ambayo ndiyo lugha ya taifa) kupewa hadhi iliyo sawa na Kiingereza katika utekelezaji wa majukumu ya serikali. Hivyo basi Kiingereza ni lugha maarufu nchini Kenya; ndiyo lugha msingi inayotumiwa katika kuwaelekeza wanafunzi shuleni. Sababu hizi ndizo ambazo zimechangia pakubwa kuwepo kwa leksimu za Kiingereza katika Sheng. Ifuatayo ni mifano ya leksimu za Kiingerezajinsi zilivyojidhihirisha katika jamiilugha ya Sheng, mtaani umoja.

Mfano 5

	<i>Leksimu mkopo</i>	<i>leksimi asili</i>	<i>maana</i>	<i>lugha changizi</i>
a)	/ Wode: /	water	maji	Kiingireza
b)	/ Ticha /	teacher	mwalimu	Kiingereza
c)	/ Mshi: /	she	msichana	Kiingereza
d)	/ Keja /	cage	nyumba	Kiingereza
e)	/ Ferare /	fare	nauli	Kiingereza
	/ Tao /	town	mjini	Kiingereza
f)	/ Cheki /	check	tazama	Kiingereza
g)	/ Mode: /	mode	mwalimu	Kiingereza
h)	/ buku /	book	kitabu	Kiingereza

Ifahamike hapa kwamba, neno moja linaweza likakopwa na kuhawilishwa na zaidi ya lugha moja. Kwa mfano katika mifano hii ya maneno kopwa na toholewa kutoka katika lugha ya Kiingereza, lipo neno ambalo limekopwa na kutoholewa na zaidi ya lugha moja. Neno hili ni “buku.” Kimsingi, hili ni neno la Kiingereza “book,” lenye maana ya “kitabu.” Sheng imelikopa

neno hili kwa mtindo wa ukopaji sisisi kutoka katika lugha ya Kiswahili, na kwa mtindo wa utohozi kutoka katika lugha ya Kiingereza.

2.1.2 Ukopaji na Utohozi: Maneno ya Kiswahili

Waswahili ni Wabantu ambao makazi yao yanapatikana pwani mwa Afrika Mashariki. Wanapatikana katika mataifa kama vile Kenya, Tanzania na Mozambiki. Kiswahili ndicho kiunzi muhimu cha jamii ya Waswahili. Jina Kiswahili lilitokana na neno la Kiarabu “sawahil” lenye maana ya “watu wa pwani.” (Oxford University Press 2003:181).

Kiswahili kina lahaja nyingi sana. Mifano ya lahaja hizi ni pamoja na Kiamu, Kinguja, Kipemba, Kimrima, Kipate, Kimvita na Kingozi. Kati ya lahaja hizi zote, lahaja ya Kiamu ndiyo iliyochaguliwa ili kuwa kama Kiswahili sanifu nchini Kenya na Tanzania. Nchini Kenya Kiswahili kimekuwa kikitumiwa kama lugha ya taifa kwa miaka mingi sasa. Lakini baada ya nchi hii kujipatia katiba mpya mnamo mwaka wa 2010, lugha hii ilipata hadhi mpya. Leo hii lugha hii sio lugha ya taifa tu, bali pia ni lugha rasmi. Hata hivyo utenda kazi wa hadhi hii mpya ya Kiswahili bado haujaanza kushuhudiwa vivilvyo katika ngazi mbali mbali za serikali. Kinyume na hayo, Kiswahili ni lugha maarufu sana miongoni mwa Wakenya. Kinyume na kuwa lugha rasmi na lugha ya taifa, Kiswahili kimeanza kuwa lugha ya kwanza hasa kwa baadhi ya watoto wanaozaliwa mijini (kama vile Nairobi) na watoto wanaozaliwa katika familia za wazazi wenye asili ya makabila tofauti.

Kwa kiwango fulani, lugha ya Kiswahili huhusishwa na watu maskini. Yaani tabaka la watu wenye mapato duni kiuchumi katika jamii. Watu wa tabaka la juu hupenda sana kujihusisha na matumizi ya Kiingereza katika shughuli zao za kila siku. Jambo hili hujidhihirisha sana hasa katika miji. Mojawapo ya miji hii ni mji wa Nairobi. Ni kutokana na sababu hizi ambapo kwa kiwango fulani Sheng hutumika kama daraja ya kuwaunganisha watu wa daraja la juu na wale wa daraja la chini kwa kurahihisha mawasiliano kati yao. Hali hii ndiyo ambayo imechangia kuwapo kwa misamati ya kiingerea na Kiswahili katika Sheng. Ifuatayo ni mifano ya leksimu za Kiswahili jinsi ambavyo hujidhihirisha katika Sheng.

Mfano 6

Leksimu mkopo

leksimu asili

maana

lugha changizi

a)	Chapa	chapa	filisika/konda	Kiswahili
b)	Chuo	chuo	shule	Kiswahili
c)	Majuu	juu	ulaya	Kiswahili
d)	Katia	kata	tongoza	Kiswahili
e)	Mzae	mzee	baba	Kiswahili
f)	Mahewa	hewa	muziki	Kiswahili

Maneno haya ya Kiswahili hukopwa na lugha ya Sheng kisha hupewa maana mpya katika lugha hiyo. Kwa mfano, neno “chapa ni neno la Kiswahili lenye maana ya kutia adabu au kurudufisha. Lakini kando na maana yake ya msingi, neno hili limepata maana mpya katika lugha ya Sheng kama vile tumeonyesha katika jedwali hapo juu.

2.1.3 Ukopaji na Utahozi: Maneno ya Kikuyu.

Wakikuyu ni sehemu ya wabantu na wanapatikana katika maeneo ya Afrika Mashariki, nchini Kenya. Hili ndilo khabla kubwa nchini Kenya na lugha yao ya mama inajulikana kama kikuyu (haya ni kwa mujibu wa mofolojia na fonolojia ya Kiwahili). Wao wenye huijita “Agikuyu” na wanapatikana katika mkoa wa kati kwenye kitovu cha Mlima Kenya. Haya ndiyo maeneo yao ya asili tangu walipowasili nchini Kenya kutoka Afrika ya Magharibi. Inakisiwa kwamba idadi kamili ya Wakikuyu nchini Kenya ni watu 6,623,000. (I. Larsen 2009: wikipedia).

Lugha ya Kikuyu inaaminika kuwa na lahaja takriban sita. Hata hivyo, lahaja hizi huwa haziadhiri mawasiliano kati ya wanajamii wa lugha hii. Mifano ya lahaja hizi ni pamoja na;

- a) Kikirinyaga
- b) Kigichugu
- c) Kinyeri
- d) Kimurang'a
- e) Kindia

f) Kikiambu

Leo hii Wakikuyu hawapatikani tu katika eneo la Mlima Kenya. Wao wamezagaa na kutawanyika katika kila pembe ya nchi ya Kenya. Vile vile, inaaminika kwamba asilimia kubwa ya wakaazi wa mji mkuu wa Kenya (Nairobi) inamilikiwa na wakikuyu. Hali hii huenda ikawa imechangiwa na ukaribu uliopo kati ya maeneo yao ya asili (kama vile Kiambu Nyeri na Murang'a) na mji wa Nairobi. Lughu hii ndio ya tatu kwa umaarufu nchini Kenya na jijini Nairobi. Si jambo la kawaida kwa mkaazi wa Nairobi atembee kwa zaidi ya mita 500 kabla ya kusikia Kikuyu kikizungumzwa aidha kwenye redio, kwenye mawasiliano ya simu tamba, katika sehemu za biashara ama kati ya watu wawili au zaidi. Kwa kiwango fulani, lugha hii hutumiwa kama lugha ya mawasiliano hata katika ofisi za kiserikali kama vile ofisi za T.S.C na K.R A.

Vile vile wakaazi na wamiliki wengi wa mashamba na biashara katika mji wa Nairobi na mtaa wa Umoja pamoja na maeneo jirani, ni wa asili ya Kikuyu. Ni kutokana na umaarufu wa lugha hii hasa katika mji wa Nairobi na mtaa wa Umoja ambapo misamiati yake mingi inapatikana katika lugha ya Sheng. Ifuatayo ni mifano ya leksimu za lugha hii jinsi zinavyojidihirisha katika Sheng.

Mfano 7

<i>Leksimu mkopo</i>	<i>leksimi asili</i>	<i>maana</i>	<i>lugha</i>
a) Ngiri	ngiri	elfu	Kikuyu
b) Shos	cucu	nyanya	Kikuyu
c) Ndonyo	dunyu	soko	Kikuyu
d) Maidhaa	madhaa	wakati	Kikuyu
e) Mukoro	mukuru	mzazi	Kikuyu
f) Morio	muriu	rafiki	Kikuyu
g) Keroro	kiruru	pombe	Kikuyu

Lugha ya Sheg ina misamiati mingi kutoka lugha ya Kikuyu. Jambo hili linatokana na sababu kwamba sehemu hii ya umoja pamoja na maeno jirani yana wakaazi wengi wenyewe asili ya kikuyu kuliko makabila mengine yanayopatikana katika eneo hili. Kati ya jumla ya wakaazi wote wa eneo hili la umoja, jamii ya Wakikuyu inamiliki asilimia 41% ya wakaazi wake. Hii ni kulingana na uchanganuzi wa data yetu.

2.1.4 Ukopaji na Utahozi: Maneno ya Kifaransa, Kiluhya, na Kidholuo

Wabaluhya ni sehemu ya Wabantu wanaopatikana katika Afrika ya Mashariki, magharibi mwa nchi ya Kenya. Neno “Baluhya” huwa na maana ya “watu wenyewe uhusiano wa kiukoo” na hujumuisha watu wanaotoka katika makabila mengi yenye sifa za kifonolojia, kimofolojia na kisemantiki zinazokaribiana. Wabaluhya wengi bado wanashikilia na kuendeleza utamaduni na imani zao za kienyeji, lakini kuna wengine ambaeo ni Wakristo. Kazi yao kuu ni ukulima. Wanaume wengi Wabaluhya mara nyingi huenda mijini na katika machimbo ya dhahabu kule Kakamega ili kutafuta kazi. (Wagner 1949).

Habari hizi za mtaalamu huyu zinazoihusu jamii ya Wabaluhya bado zina ukweli wa kiasi fulani hata waleo. Mji wa Nairobi una idadi kubwa sana ya Wabaluhya. Inaaminika kwamba wengi wao hufanya kazi mjini Nairobi kama mabawabu na wapishi. Ingawaje mjini Nairobi kuna Wabaluhya wengi, leksimu zao bado hazijaweza kushudiwa sana katika Sheng, mtaani Umoja. Labda hii inatokana na sababu kwamba jamii ya Wabaluhya ni jamii ambayo inajumuisha lahaja zaidi ya 15 hivi kwamba wakati fulani huwa vigumu kwa wanajamii hawa wote kuwasiliana wanapozungumza. Kwa mfano Kibukusu na Kimaragoli zote ni lahaja za Kibaluhya lakini wanajamii wa lahaja hizi mbili za Kiluhya huwa hawaelewani katika mazungumzo yao.

Kidholuo ni lugha ambayo huzungumzwa na wajaluo wanaopatikana magharibi mwa chi ya Kenya. Jamii hii hasa ile inayoishi mjini Nairobi huenzi sana kujihusisha na uzungumzaji wa Kiingereza au lugha yao ya mama (kidholuo). Uzungumzaji wao wa Kiswahili (kwa wengi wao) huwa wa kiwango cha chini sana hivi kwamba huwa hawazifuati sheria na kanuni za kisarufi ambazo huongoza na kuelekeza matumizi ya Kiwahili. Katika eneo la Umoja, idadi ya wajaluo ni ndogo sana ikilinganishwa na ile ya Wakikuyu. Hii ndiyo sababu leksimu za kidholuo bado hazijaweza kushuhudiwa kwa wingi katika Sheng.

Kifaransa ni lugha ambayo kiasili huzungumzwa na Wafaransa, kutoka taifa la Ufaransa. Lugha hii haina mizizi yake katika nchi ya Kenya. Mizizi ya Kifaransa hasa iko katika mataifa yaliyotawaliwa na Ufaransa. Mataifa haya hasa yanapatikana magharibi mwa bara la Afrika. Kenya si mojawapo ya mataifa hayo. Hii ndiyo maana leksimu za Kifaransa hazipatikani mno katika Sheng. Ifuatayo ni mifano ya leksimu za Kifaransa, Kibaluhya na kidholuo jinsi zinavyojidhihirisha katika Sheng.

Mfano 8

	<i>Leksimu mkopo</i>	<i>leksimu asili maana</i>	<i>lugha changizi</i>
a)	Demu	madame	msichana
b)	Sota	sota	kufirisika
c)	Atoti	atoti	msichana
d)	Saikoro	msakhulu	mzee
e)	Buda	budha	baba
			Kiswahili/ Kihindi

Neno buda limeeleweka na wataalamu kadha kama neno la Sheng linalotokana na neno la kihindi “budha,” lenye maana ya mtu mwenye heshima zake au mwanzilishi wa dini ya “Budhism.” Lakini huu sio ukweli wa asilimia mia moja. Ifahamike kwamba lugha ya Kiswahili pia inalimiliki neno hili “buda” lenye maana ya ndovu mzee au mwanamume mzee aliyeanza kung’oka meno. Vile vile, lugha huwa na mazoea ya kukopa kuto kwa lugha iliyo karibu nayo au yenye sifa zinazokaribiana nayo. Kwa misingi hii kuna uwezekano mkubwa sana kwamba Sheng ilikopa neno buda kutoka kwa lugha ya Kiswahili wala sio Kihindi. Yaani Kiswahili ki karibu sana na Sheng kuliko Kihindi. Kuwepo kwa neno hili katika lugha ya Kihindi na Kiswahili ni jambo la Kisadfa tu. Kwa mfano leno “msondo” linapatikana kisadfa katika lugha ya Kiswahili na lugha ya Kibaluhya. Ingawaje umbo la neno hili ni moja katika lugha hizi zote mbili, maana msingi ya neno hili katika lugha hizo mbili ni tofauti kabisa. Katika Kiswahili, neno ‘msondo’ lina maana ya, *aina ya ngoma ambayo huchewa na wanajamii lugha ya mijikenda*. Katika jamii ya Wabaluhya, neno msondo huwa na maana ya, *sehemu tupu ambayo hutumiwa na binadamu kwa kupidishia kinyesi*.

2.2 Mbinu ya Ukatizaji.

Ukatizaji ni mbinu ya kuundia maneno ambayo huunda maneno kwa kuyafupisha. Katika mbinu hii vile vile, maneno huundwa kwa kudondosha silabi moja au zaidi. (Jefwa, 2011: 51)

Tuki (1990), nayo inasema kuwa: “*ukatizaji ni hatua ya kufupisha neno kwa kuondoa sehemu ya mwanzoni au mwishoni*”. Neno “sehemu” katika fasiri hii ina maana ya “silabi.”

Kulingana na fasiri hizi mbili za neno ukatizaji’ tunapata kuelewa kwamba ukatizaji ni ufupishaji wa neno, katika lugha yoyote ile. Iribemwangi na Mukhwana (2011:166) nao wana maoni kuwa ukatizaji ni mbinu ya uundaji wa maneno inayohusu ufupishaji wa majina, maneno au vifungu vya maneno. Yule (1985:54) naye anasema kwamba ukatizaji hutokea pale ambapo neno lenye zaidi ya silabi moja hupunguzwa silabi ili neno hilo liwe fupi kimuundo. Kulingana na maoni ya wataalamu hawa, ni bayana kwamba jukumu msingi la ukatizaji ni kufupisha silabi fulani za mwanzo, kati au za mwisho wa neno ili kuunda neno jipya. Mbinu hii ya uundaji wa maneno hutumika na lugha nyingi ulimwenguni. Kwa mfano, lugha ya Kiingereza imeunda maneno yafuatayo kwa kutumia mbinu hii.

Mfano 9

	Neno	ukatizaji
a)	Bicycle	bike
b)	Professor	prof
c)	Fantasy	fan
d)	Coka cola	coke

Lugha ya Kiswahili pia huwa na maneno yalyoundwa kutokana na michakato ya mbinu hii ya ukatizaji. Mifano ya maneno hayo ni pamoja na yafuatayo.

Mfano 10

Neno	Ufupishaji
-------------	-------------------

Bibi	Bi
Mwanamke	Mke
Mwanamume	Mume
Bibi harusi	Bi. Harusi

Lugha ya Sheng pia inayo maneno yalioundwa kwa mbinu hii. Hata hivyo maneno ya Sheng yalioudwa kwa mbinu hii huwa ya kukopwa kutoka katika leksimu za lugha zingine. Yaani, lugha hii huwa haina maneno yake binafsi ya asilia ila tu, yale ya kujibunia. Hivyo basi maneno ambayo yamekatishwa katika lugha hii, mwanzoni huwa yamekopwa (na yakatoholewa) kisha yakafupishwa au kukatizwa. Tazama mfano huu ufuatao:

Mfano 11

Leksimi mkopo	leksimi asili	maana	lugha changizi
a) Sunday	/ sande:/	jumapili	kiingereza
b) Practice	/ tizi:/	zoezi	Kiingereza
c) Sister	/ siz /	dada	Kiingereza
d) Saturday	/ sato: /	jumamosi	Kiingereza
e) Jesus	/ jesi: /	yesu	Kiingereza
f) Dereva	/ dere: /	dereva	Kiwsahili

g)	Brother	/ bro: /	kaka	Kiingereza
h)	Basketball	/ bako /	mpira	Kiingereza

Kati ya maneno yaliyokatizwa kuna yale ambayo hufanyiwa marekebisho ya kifonolojia hivi kwamba matamshi au sauti za maneno hayo hurefushwa yanapotamkwa. Muundo wa pili huwa wa kimofolojia. Yaani neno husika hukatizwa tu lakini maana msingi ya neno hilo huwa haibadiliki. Huddleston (2002: 1634) anasema kuwa kuna aina tatu za ukatizaji; ukatizaji awali, ukatizaji kati na ukatizaji tamati. Kulingana na uchanganuzi wa data yetu tumbaini kwamba lugha ya Sheng inatawaliwa na sifa za ukatizaji awali na tamati. Sifa za ukatizaji wa kati haina. Hivi ndivyo ilivyo katika lugha karibu zote zenyeha sifa ya kibantu. Lugha hizo huwa na sifa za ukatizaji awali na tamati, na sio ule wa kati. Hivyo basi Sheng pia imechukua sifa hizo za kibantu zinazohusiana na ukatizaji.

2.3 Mbinu ya Uambishaji.

Uambishaji huwa utaratibu wa kuongezea viambishi katika mzizi wa leksimu ili kuunda leksimu mpya. Mbinu hii hujumuisha viambishi awali na viambishi tamati. Viambishi hivi huambishwa kwenye mzizi wa neno ili kuunda maneno mapya. (Jefwa 2010: 52). Matthews (1997:7) naye anasema kuwa uambishaji ni utaratibu wa kuongezea herufi, sauti au makundi yao katika mzizi wa neno na kwamba nyongeza hiyo hubadilisha maana na uamilifu wa neno hilo. Richards na wengine (1985:105) pia wana maoni kwamba uambishaji ni uongezeaji wa viambishi katika mzizi wa neno kwa lengo la kuunda neno jipya.

Sheng huitumia mbinu hii pia ili kijiundia leksimu mpya. Hata hivyo leksimu za Sheng zilizoundwa kwa mbinu hii huwa za mkopo. Leksimu hizo hukopwa kutoka kwa lugha kadhaa kisha hutoholewa kabla ya kufanyiwa uambishaji. Viambishi ambavyo hutumiwa huwa viambishi awali na viambishi tamati.

Mfano 12

Uambishji (mofu)	Leksimu lekska	Maana
a) M+ supa	msupa	msichana
b) M+ shii	mshii	msichana

c)	U+ fala	ufala	ujinga
d)	U+ sorora + ji	usororaji	udadisi
e)	M + sapere	msapere	Mkikuyu
f)	M + ngoso	mngoso	Mzungu
g)	Ki + jadhee	kijadhee	Kidholuo
h)	Vi + noma	vinoma	vibaya
i)	Vi+ dedli	videdli	hatari
j)	Ku+ nais	kunais	kufurahisha/ kupendeza
k)	Ku+ akt	kuakt	kuigiza
l)	Ku+ plei	kuplei	kucheza

Katika mifano hii ni bayana kwamba kuna viambishi vyta unominishaji vinavyojidhihirisha. Viambishi hivi vinawakilishwa na mofu {m}, {u}, {ki} na {ku} kama zinavyojitokeza kwenye maneno kama vile “msupa,” “kunais” na “usororaji.” Pia mfano huu unajumuisha mofu zinazowakilisha vielezi. Mifano ya mofu hizi ni pamoja na; {vi} kwenye maneno “vinoma” na “videdli.”

2.4 Mbinu ya Ubadilishaji Silabi.

Katika mbinu hii ya ujenzi wa maneno, neno kopwa hutoholewa kwanza. Halafu, silabi za neno hilo toholewa hupanguliwa na zikapangwa upya. Upanguaji na upangaji upya wa silabi za neno hilo husika, hulipa neno hilo ujenzi au muundo mpya wa kinyume nyume. Muundo huo mpya huwa haubadilishi maana asilia ya neno hilo. Mbinu hii ya uundaji wa maneno bado haijatia fora sana katika lugha zingine za kitaifa na za kimataifa. Ni jambo gumu kupata lugha nyingine kando na Sheng ikiwa imetumia mbinu hii katika uundaji wa leksimu zake. Hii ni mbinu ya kipekee ambayo jamii ya Sheng inajivunia kuwa nayo ulimwenguni kote. Mbinu hii huifaa jamii hii sana kwa sababu wao pekee yao ndio huitumia katika ufichaji wa siri za mazungumzo yao.

Ogechi (2005:340) anasema kwamba neno husika hukopwa kisha matamshi ya neno hilo hurekebishwa kabla ya silabi za neno hilo kurekebishwa. Ubadirishaji silabi huu huwa utaratibu wa kimakusudi ambao hutumiwa na Sheng kwa kuundia leksimu zake. Ifuatayo ni mifano ya leksimu za Sheng zilizoundwa kwa mbinu hii ya ubadirishaji silabi.

Mfano 13

Leksimu chagizi leksimu toholewa ujenzi kinyume lugha chagizi.

a)	Bread	bredi	dibre	Kiingereza
b)	Story	stori	risto	Kiingereza
c)	Card	kadi	dika	Kiingereza
d)	Nyumba	nyumba	mbanyu	Kiswahili
e)	Mbele	mbele	lembe	Kiswahili
f)	Manyanga	manyanga	nganya	Kiswahili
g)	Pisto	bunduki	itos	Kiingereza

Kulingana na mifano hii leksimu changizi ni leksimu ambazo zina uwezo wa kuelewaka bayana na mwanajamii wa lugha husika. Lakini punde tu leksimu hizi zinapofanyiwa marekebisheshi ya ubadirishaji silabi, maana msingi ya neno hilo hufichwa kiasi kwamba huweza kuelewaka tu na watu wa jamii lengwa. Maana msingi ya neno hilo huwa haibadilishi. Vile vile maneno ambayo hutumika katika mbinu hii ya uundaji wa maneno huwa ya mkopo.

2.5 Onomatopia: Tanakali za Sauti.

Onomatopia pia hujulikana kama tanakali za sauti. Onomatopia ni ujenzi wa neno kwa kuiga sauti au milio wa kitu. (TUKI, 2009: 43). Iribemwangi na Mukhwana (2011: 159) nao wana maoni yanayodai kwamba Onomatopea ni mbini ya uundaji leksimu ambapo leksimu huundwa kutokana na sifa, uamilifu, umbo, sauti au milio. Kuna madai mengine yanayosema kwamba Onomatopia ni uundaji wa maneno kutokana na sauti asilia. Lugha nyingi ulimwenguni huwa na

sifa ya kujiundai maneno kwa kutumia mbinu hii ya Onomatopia. Kwa mfano, lugha ya Kiingereza ina mifano ifuatayo ya Onomatopea.

Kiingereza **maana**

Buzz	toa sauti kama nyuki
Hizz	pumua kwa sauti ya nyoka
Crowl	enda kwa tumbo
Slither	enda kama konokoni

Lugha ya Kiswahili nayo ina mifano ifuatayo ya Onomatopia;

Kiswahili **Maana**

Kifagio	Kifaa cha kufagia
Kifutio	Kifaa cha kufutia
Patipati	Aina ya kiatu chenye kamba mbili
Pikipiki	Chombo cha usafiri chenye umbo kama baiskeli.
Tukutuku	Chombo cha usafiri chenye magurudumu matatu

Mifano hii ya Onomatopia za Kiswahili imetokana na sifa zinazotokana na vitenzi husika. Vitenzi hivi ni “fagia” na “futa.” Leksimu “pikipiki” na “patipati” nazo ni Onomatopia zinazotokana na sauti ambazo vifaa hivyo hutoa punde vinapokuwa katika matumizi.

Lugha ya Sheng pia hujiundai leksimu zenyе sifa za Onomatopia. Inazo mifano kadha ya maneno yalioundwa kwa mbinu hii. Mifano ya leksimu hizi ni kama ifuatayo.

Mfano 14

<i>Leksimu tanakali</i>	<i>Maana</i>	<i>Lugha</i>
a) Kacha	pingu	Sheng
b) Bling bling	mapambo ghali	Kiingereza
c) Mnga'aro	mavazi	Kiswahili
d) Poko	kahaba	Sheng
e) Mburrcha	matatizo	Sheng

Leksimu za Sheng ambazo huundwa kwa misingi ya mbinu hii huwa chache ikilinganishwa na lugha nyingine. La msingi kueleweka hapa - japo halina umuhimu maalum katika kitengo hiki - ni kwamba De Saussure (1916) alikuwa na mawazo kwamba katika lugha (yooyote ile) huwa hakuna uhusiano wa moja kawa moja kati ya kiashiria na kiashiriwa. Dhana hii ya De Saussure inaonekana kuzua ukinzani fulani na wazo hili la uundaji wa maneno kwa mbinu ya Onomatopia. Hata hivyo hili sio jambo letu la mjadala katika kiwango hiki.

2.7 Upolisemia

Iribemwangi na Mukhwana (2011:166) wanasema kuwa upolisemia ni kule kuongezea maana kwa maneno yaliyomo katika lugha. Hii ina maana kwamba, neno fulani katika lugha fulani linaweza likapewa maana nyongeza, kando na maana leksika ya neno hilo. Kwa mfano katika Kiswahili neno “mzee” hapo awali lilikuwa na maana moja kuu: mtu mwenye umri unaozidi miaka hamsini hivi. Lakini leo hii neno hili limepanua maana yake hivi kwamba lina maana mpya au mtu mwenye sifa za kihadhi bila ya kujali umri. Lakini kwa kiwango fulani tuligundua kuwa huu sio upolisemia jinsi unavyofasiriwa na Iribemwangi na Mukhwana. Katika kiwango cha Sheng, huu ni ukopaji wa maumbo ya maneno ya Kiswahili, kisha maumbo hayo yanafanywa kuwa leksimu na kupewa maana mpya katika lugha ya Sheng.

Ogechi (2005:343) naye anasema kuwa nomino kopwa katika Sheng hupata upanuzi wa maana kisemantiki. Ogechi anatoa mfano wa neno la Kiswahili “chuo” ambalo maana yake msingi ni masomo ya kiwango cha anuai. Neno hili limekopwa na lugha ya Sheng na likapanuliwa maana

yake. Katika lugha hii, chuo ni shule yoyote ile iwe ya msingi, chekechea, anuai au Chuo kikuu. Maneno mengine ambayo yameundwa kwa sifa za upolisemia katika lugha hii ya Sheng ni pamoja na:

Mfano 16

<i>Neno</i>	<i>maana asili (Swahili)</i>	<i>maana ziada (Sheng)</i>
chapa	tia adabu	kufilisika/ kukonda
choma	kuunguza	kuvuta bangi
zidi	pita kiasi	kutembea
teke	pigo la nguu	haraka
kaa	keti	jamia
ganda	ngozi/shikana	chapa

2.8 Ubunifu wa Leksimu

Ubunifu wa maneno katika lugha huchochewa na mambo kama vile uvumbuzi wa kisayansi wa vifaa vipyta katika jamii. Jambo kama hili litokeapo, basi jamii husika huwa haina budi ila kubuni msamiati wa kutumiwa kwa kutajia vifaa hivyo. Kwa mfano lugha ya Kiswahili ilijibunia misamiati ya vifaa vya kisayansi vilivyovumbuliwa kule marekani na vikashirikishwa kiutenda kazi katika mazingira ya Afrika Masharki: nchini Kenya. Vifaa hivi ni kama vile tarakilishi, barua pepe, barua meme, kipepesi, mtandao na rununu.

Kulingana na Hartmann na Stork (1972:29) ubunifu ni mchakato au matokeo ya kuunda leksimu mpya kimakusudi kutookana na faridi za kimofolojia zilizopo. Katika jamii, kuna hali inayoweza kuzuka na kuwalazimu wanajamii hiyo husika kubuni msamiati wa kutajia kifaa au hali ambayo ni geni kwao. Leksimu kama hiyo huwa haihuzishwi na ukopaji wala otohozi. Mbinu hii huwa na sifa za kuitajirisha lugha husika ndani kwa ndani. Lugha za ulimwengu huwa na sifa hii ya kujibunia maneno ili kuakisi au kuziba pengo fulani la hitaji katika jamii. Kwa mfano lugha ya Kiingereza na Kiswahili imebuni maneno yafuatayo ya kuvitajia vifaa vya kisayansi ambavyo vimevumbuliwa hivi maajuzi.

Mfano 17

Kiingereza	Kiswahili
Hand set	simu ya mkononi
Mobile phone	rununu
Computer	tarakilishi
Laptop	kipakatalishi
Ipad	aipadi

Maneno haya hayakuwemo katika leksimu awali za lugha hizi mbili lakini maadam vifaa hivi vimebuniwa kisayansi hivi karibuni katika jamii hizi mbili, ilibidi jamii hizi zibuni maneno ya kuvitajia vifaa hivi. Maneno haya hayatokani na ukopaji wala utohozi.

Jinsi tulivyosema hapo awali kwamba ubunifu wa leksimu mpya katika jamii husika huchochewa na mabadiliko katika mazingara ya matumizi lugha. Kifaa kipyaa au hali mpya inapozuka Vile vile lugha ya Sheng hujibunia misamati ili kuirutubisha lugha hiyo kwa leksimu fokofoko. Ifuatayo ni mifano ya leksimu za Shengzilizoundwa kwa mbinu ya ubunifu.

Mifano 18

Leksimu buniwa	maana
a) Ndula	kiatu
b) Mbota	saa
c) Ngata	petroli
d) Dinga	gari
e) Mboch	mjakazi
f) Ngwai	bangi
g) Nangoz	simu

- h) Tei pombe
- i) Mawenzere makalio
- j) Manyura kufa
- k) Makagare mapumbu
- l) Tonji mwizi
- m) Karao polisi
- n) Kacha pingu
- o) Mbus msichana

2.9 Akronimu

Katika akronimu herufi au silabi za mwanzo za neno au seti ya maneno hutumika kuundia leksimu nyingine mpya. Akronimu aghalabu huandikwa kwa herufi kubwa na hizo herufi husimamia neno fulani mahususi.

Obuchi na Mukhwana (2010:109) wanasema kuwa akronimu ni utaratibu wa kuunda leksimu kwa kufupisha maneno yanayotumiwa pamoja kwa kuchukua herufi au silabi za mwanzo za maneno hayo. Sehemu za kila neno katika kishazi huchukuliwa na kuunganishwa ili kuunda leksimu moja mpya yenye kusimamia dhana moja. Mbinu hii ina sehemu ya matumizi yake hasa katika lugha ya kiingereza. Mifano ya maneno ya kiingereza ambayo yameundwa kutokana na mbinu hii ni pamoja na;

Mfano 19

Akronimu	Maana Kamili
NATO	North Allaiance Treaty Organization
NASA	National Aeronautic And Space Administration
UNESCO	United Nations Education Scientific and Cultural Organization

UNEP	United Nations Environmental Program
KANU	Kenya African National Union
KARI	Kenya Agricultural Research Institute
KEFRI	Kenya Forestry Research Institute
KETRI	Kenya Trypasonomius Research Institute

La msingi kueleweka hapa ni kwamba katika akronimu, baada ya kuunda leksimu, leksimu hiyo hutamkwa kama neno moja baada ya mazoea, na wala sio kama herufi moja moja.

Mbinu hii ya uundaji wa maneno bado haijakita katika lugha ya Sheng. Labda jinsi siku zinavyozidi kusonga ndivyo matumizi yake katika lugha hii yatakapoanza kushuhudiwa.

2.10 Kaleki: Tafsiri Mkopo

Hii pia ni moja wapo ya mbinu kadhaa za uundaji wa maneno. Katika mbinu hii lugha hukopa na ikatafsiri neno au maneno husika moja kwa moja au neno kwa neno. Kwa mfano, lugha ya kiingereza imetumia mbinu hii ili kujipatia msamiati mwangi kutokana na leksimu za lugha nyinginezo kama vile kijerumani, kifaransa na kihispania. Vile vile Lugha ya Kiswahili imetumia mbinu hii ili kuijundia leksimu. Leksimu hizi zimetokana hasa na maneno ya kiingereza. Ifuatayo ni mifano ya maneno ya Kiswahili yaliyoundwa (kwa mbinu hii ya kalek) kutokana na maneno ya Kiingereza.

Mfano 20

Kiingereza	Kiswahili
Sugar mummy	mama sukari
Sugar daddy	baba sukari
United Nations	umoja wa mataifa
Speech organs	ala za sauti
Cocktail party	karamu ya mkia wa jogoo

Hata hivyo mbinu hii ya uundajiwa maneno huwa na changamoto zake. Changamoto hizi hutokana na maana ambayo huweza kutafsiriwa kutohukana na maneno yalioundwa katika lugha pokezi. Yaani maana halisi katika lugha chagizi mara nyingi huwa sio tafsiriwa katika lugha pokezi. Lugha ya Sheng bado haina mbinu hii katika uundaji wa maneno yake.

2.11 Uhulutishaji

Huu huwa mchakato wa kuunganisha maneno mawili yenye maana tofauti ili kuunda umbo la neno lingune lenye maana tofauti. Yaani mwanzo wa neno fulani (la kwanza) huchukuliwa na kuunganishwa na mwisho au mwanzo wa neno la pili ili kuunda leksimu mpya. Lugha nyingi huwa na maneno yalioundwa kwa kutumia mbinu hii ya uhulutisha. Kwa mfano, lugha ya kiingereza ina mifano ya maneno yafuatayo.

Mfano 21

Uhulutishaji	Maana
Smoke + fog = smog	mchanganyiko wa ukungu na moshi
Gas + alcohol = gasohol	mchanganyiko wa gesi na pombe
Hotel + motor = motel	msafara wa magari

Mbinu hii ya uundaji wa maneno pia inajitokeza katika lugha ya Kiswahili. Yaani kunayo pia majina ya Kiswahili ambayo yameundwa kwa mbinu hii ya uhulutishaji. Mifano ya majina haya katika lugha ya Kiswahili ni kama ifuatayo;

Mfano 22

Chamcha	=	Chakula cha mchana
Chajio	=	Chakula cha jioni
Ukimwi	=	Ukosefu wa kinga mwilini

Fupaja = Mfupa wa paja

Mbinu hii ya uunda wa maneno huwa na sifa zinazokaribiana na zile za akronimu. Hata hivyo hizi ni mbinu mbili tofauti za uundaji wa maneno, jinsi tumevyofafanua katika maelezo ya kila mfano wa uundaji wa maneno kwa misingi ya mbinu hizi mbili.

2.12 Uambatishaji

Kulingana na Franklin na Rodman (1988:137) uambatanishaji ni mbinu ya kuunda maneno kwa kuunganisha maneno mawili ambayo kwa kawaida huwa hayawi pamoja (kwa mujibu wa muundo wa lugha husika) ili kuunda neno jipya. Neno linalojitokeza huwa neno ambatano. Neno hilo jipya huwa halitazamwi kama maneno mawili ila neno moja. Neno ambalo huundwa huwa na maana tofauti na maneno awali ambayo yalitumika katika uundaji wake. Lugha nyingi kama vile kiingereza, Kiswahili na Sheng zimejiundia maneno kwa kutumia mbinu hii sana. Kwa mfano, leksimu zifuatazo hujitokeza katika lugha ya kiingereza.

Mfano 23

Glass +	ware	=	glassware
Under +	ware	=	underware
Class +	room	=	classroom
Bed +	room	=	bedroom
Text +	book	=	textbook
House +	girl	=	housegirl
Hand +	bag	=	handbag
Foot +	ball	=	footbal

Vile vile mifano ifutayo hujitokeza katika lugha ya Kiswahili.

Mfano 24

Mja	+ mzito	=	mjamzitio
Soko	+ huru	=	sokohuru
Kiangaza	+ macho	=	kuangazamacho
Kiinua	+ mgongo	=	kinuamgongo
Mwana	+ jeshi	=	mwana jeshi
Bata	+ mzinga	=	batamzinga
Paka	+ shume	=	pakashume
Mwana	+ sesere	=	mwana sesere

Katika mifano hii ya kiingereza na Kiswahili ambayo tumeitaja hapo juu, maneno mawili ya awali ambayo hutumiwa katika uundaji wa neno ambatano, huwa na maana yazo leksia. Lakini punde tu yanapounganishwa ili kuunda neno jipya (neno ambatano) maneno hayo ya awali hupoteza maana yazo asilia. Neno jipya ambalo huundwa kutokana na maneno hayo mawili huchukua maana leksia iliyo tofauti na maana za maneno ambayo yaliliunda. Sheng pia huwa na maneno ambayo yameundwa kwa misingi ya mbinu hii. Mifano ya maneno haya ni pamoja na ifuatayo;

Mfano 25

Uambatishaji	maana
Buu + fee	= bufee
Chiki + dii	= chikidii

2.13 Unyumbuzi Kapa

Unyumbuzi kapa huchukuliwa kama aina fulani ya uambishaji, japo ni uambishaji ambao haudhihiriki kimofolojia. Hivyo basi hata ingawa leksimu huwa haiwi na viambishi vya kiothografia huwa inachukuliwa kwamba viambishi hivyo huwa kapa.

Kuhusu unyumbuzi kapa, Katamba (1993:54) ana maoni kwamba leksimu mpya inaweza kuundwa bila ya kubadili umbo la leksimu asilia. Katika mchakato huu leksimu hubadilisha kategoria yake bila kuambishwa wala kufanyiwa jambo lolote linaloweza kubadili umbo la leksimu hiyo. Yaani leksimu ambayo ni nomino inaweza ikatumika kama kitensi katka mazingera tofautitofauti.

Matumizi ya unyumbuzi kapa katika uundaji wa maneno hujibainisha vyema katika lugha ya kiingereza kuliko lugha ya Kiswahili na Sheng. Mfano ufuatao ni wa kiingereza. Katika mfano huu leksimu *cook* limetumika kwa maana ya nomino na maana ya kitensi mtawalia.

Mfano: 26

- a) Agness will cook today (Agness atapika leo)
- b) Agness is the cook today (Agness ndiye mpishi leo)

Katika mfano wa kwanza neno *cook* linajitokeza kama kitensi na katika mfano wa pili neno *cook* linajitokeza kama nomino. Mbinu hii haikujitokeza katika uchanganuzi wa data yetu. Hii ilitokana na sababu kwamba lugha ya Kiswahili na Sheng ni lugha zenyeye sifa za kibantu. Lugha za kibantu huwa lugha ambishi bainishi. Yaani ili kategoria ya neno ibadilike ni lazima viambishi nyambuzi viongezwe kwenye mzizi wa neno husika.

2.14 Ujenzi Ghairi

Kulingana na Warambo (2011:41) ujenzi hairi ni hali ambapo leksimu ya aina fulani (mara nyingi huwa ni nomino) inapunguzwa kimaumbo ili kuunda leksimu nyingine yenyeye umbo tofauti. Mara nyingi leksimu ambayo huundwa huwa kitensi. Kwa mfano lugha ya kiingereza imeunda maneno yafuatayo kwa kutumia mbinu hii ya uundaji wa maneno,

Mfano 27

Neno awali (nomino)	neno undwa (kitensi)	maana
Actor	act	igiza
Driver	drive	endesha

Televisheni	televise	tangaza
Prayer	pray	omba
Editors	edit	Hariri
Conductor	conduct	ongoza

Kiswahili na Sheng ni lugha mbili ambazo zina sifa za kiisimu zinazokaribiana sana. Hii inatokana na sababu kwamba Sheng ni kijilahaja au kimelea cha lugha ya Kiswahili. Hivyo basi mara nyingi sifa za kimuundo zinazopatikana katika Kiswahili, pia hupatikana katika Sheng. Mbinu hii ya uundaji wa maneno kwa kiwango kikubwa bado haijashuhudiwa katika lugha ya Kiswahili. Labda hii ndiyo sababu kwamba mbinu hii haina mizizi katika uundaji wa maneno ya Sheng vile vile.

Ni vyema kuweka bayana kwamba ujenzi ghari na ukatizaji hukanganya wakati mwingine. La msingi kueleweka hapa ni kwamba, ujenzi ghairi huwa utaratibu wa kimofolojia wa kuchanganua neno kwa misingi ya mofolojia yake ilhali ukatizaji huwa mfanyiko wa kifonolojia unaonuiwa kufanya neno kuwa fupi kimatamshi. Maneno yanayoundwa kutokana na ujenzi ghairi huwa na sifa za vitenzi. Vitenzi hivi hutokana na ukarabati wa kimofolojia ambao hufanyiwa nomino husika. Hivi sivyo ilivyo na mbinu ya ukatizaji.

Hitimisho

Katika sura hii tumeshughulikia uundaji wa maneno ya Sheng kwa kuzingatia mbinu za uundaji wa maneno kimofolojia. Mbinu za uundaji wa maneno tulizozichunguza na kuzibaini katika lugha hii ni pamoja na: Ukopaji na Utahozi, Uambatishaji, Upolisemia, Onomatopea na ubunifu. Hata hivyo tuliweza kubaini kwamba, mhimili mkubwa wa uundaji wa maneno katika lugha hii ya Sheng huwa ukopaji na utahozi. Ukopaji na utahozi huu hasa hutokana na maneno ya Kiswahili, Kikikuyu, na Kiingereza. Leksimu zingine zinazotokana na lugha zingine zipo japo si nyingi ikilinganishwa na leksimu zinazotokana na lugha hizo tatu ambazo tumezitaja hapo awali.

Utafiti wetu pia umetubainishia kwamba, mbinu hizi za uuundaji wa maneno katika lugha hii ya Sheng ndio huwa chanzo na kichochezi cha kuwepo kwa hali ya kutolewana na mgogoro mionganoni mwa jamii ya dini ya Kikristo katika eneo hili la Umoja. Jambo hili ndilo ambalo

limepelekeea kuzuka kwa makundi mawil kinzani katika dini ya Kikristo katika eneo hilo. Kikundi cha kwanza hujumuisha wafuasi wanaopenda kuabudu na kumsifu Mungu kwa Sheng na kikundi cha pili ni cha wale wanaopenda kuabudu na kumsifu Mungu kwa misingi ya sajili ya dini ya Kikristo.

SURA YA TATU

3.0 VIFAFIWA NA SENTENSI ZA SHENG

Utangulizi

Katika sura ya pili, tulitathmini jinsi ambavyo lugha ya Sheng hujundia maneno ili lugha hiyo ipate kujitosheleza vyema kilekisimu. Katika sura hii ya tatu, tumebainisha kwamba leksimu hizi za Sheng huwa na sifa kadha za kisemantiki. Majawapo ya sifa hizi za kisemantiki ni pamoja na mahusiano ya vifahiwa. Yaani, leksimu za Sheng huwa na sifa za mahusiano ya vifahiwa. vifahiwa hivi hutumiwa na jamii ya Sheng katika utungaji wa sentensi. Vifahiwa hivi pamoja na sentensi hizi za Sheng ndivyo vifaa ambavyo wanajamiilugha ya Sheng huvitumia katika kufanikisha mawasiliano mionganoni mwao. Katika sura hii ya tatu tumetathmini na kuchanganua mahusiano haya ya vifahiwa pamoja na sentensi hizo katika misingi ya semantiki; kigezo cha maana na miundo ya sentensi. Kwa misingi hii tumeweza kubainisha kwamba jamii ya Sheng, baada ya kujiainisha kama jamii ya vijana kwa jinsi ya uteuzi na sifa za leksimu zake, huweza sasa kujitambulisha kwa makundi mengine katika jamii ambayo aidha huizungumza Sheng au lugha nyingine isiyokuwa na sifa za Sheng. Kigezo ambacho wao hutumia katika ujitalishaji huu huwa kigezo cha vifahiwa na miundo ya sentensi jinsi ilivyo tu na lugha zingine katika ulimwengu. Mionganoni mwa vigezo vingi vya kisemantiki ambavyo wanajamiilugha ya Sheng hutumia ili kufanikisha mawasiliano kati yao, ni vigezo hivi viwili vya kisemantiki ambavyo tumevitaja hapo awali. Yaani kigezo cha mahusiano ya vifahiwa na kigezo cha miundo ya sentensi. Kwa kufanya hivi, lugha ya Sheng sasa humiliki uwezo wa kusababisha athari zozote zile katika asasi yoyote ile katika jamii, ikiwemo asasi ya dini ya Kikristo.

Fasiri ya mahusiano ya kifahiwa ni fasiri ambayo imewahi kutolewa na wanaismu wengi. Mmoja wa wanaismu hawa ni Ferdinand De Saussure (1916). Katika fasiri hii, Saussure

anasema kuwa leksimu za lugha fulani huweza kuingia katika mahusiano tofauti. Moja wapo ya mahusiano haya ni vifahiwa. Katika muktadha huu wa mahusiano ya vifahiwa, maneno huweza kuhusiana hivi kwamba maana ya neno fulani huweza ikawa kinyume cha maana ya neno jingine. Mahusiano ya maneno haya husaidia kutoa na kueleza maana za maneno mengine. Kwa mfano, kuwepo kwa neno “mchele” katika lugha ya Kiswahili kunarahisisha kuwepo kwa maana ya kina ya maneno kama vile “wali”, “mpunga” na “mashendeya.” Vile vile katika lugha ya Sheng kuwepo kwa neno “ferare” kunasaidia kulielezea neno “bufee.” Kwa upande mwingine, maneno kama haya huweza kuingia katika uhusiano wima. Mifano ya vifahiwa katika lugha ya Kiswahili ni kama vile haiponomia, sinonimia, homonimia, polisemia, na antonomia. Katika utafiti wetu, tumeweza kubaini kwamba lugha ya Sheng inayo mifano hii ya mahusiano ya vifahiwa. Mifano hii ya mahusiano ya vifahiwa katika lugha ya Sheng ni kama ifuatayo:

3.1 Haiponomia


Haiponimu ni leksimu kopwa kutoka katika lugha ya Kiingereza “hyponym” lenye maana ya “neno ambalo maana yake inapatikana katika neno jingine lenye maana pana zaidi”. Neno hili (kubwa) ambalo hujumuisha maana ya neno au maneno mengine yenye maana ndogo huitwa neno kuu nayo maneno madogo ambayo hupatikana chini ya neno kuu ndiyo huitwa haiponimu. Habwe na Karanja (2011:209) wanafasiri maana ya neno haiponimu kwa kusema kuwa; “haiponimu ni uhusiano wa lugha ambapo maana fulani ya neno huwa sehemu ya maana kubwa ya neno. Neno lenye maana kubwa huitwa neno jumuishi ilhali maneno yenye maana ndogo huitwa haiponimia.”

Nayo Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugh (1990:30) inafasiri maana ya neno haiponomia kwa kusema kuwa; “haiponimia ni neno ambalo maana yake imejumuishwa katika maana ya neno jingine.” Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugh (1990:30) nayo inafasiri maana ya neno hiponimu kwa kusema kuwa, “hiponimu ni neno ambalo maana yake imejumuishwa katika maana ya neno jingine.” Yaani kulingana na tafsiri hizi, haiponimu huwa uhusiano uliopo baina ya neno maalum na neno jingine la kijumla linalohusiana nalo. Neno ambalo maana yake imejumuishwa katika maana ya neon jingine ndio huitwa hiponimu (Wamitila 2003:61).


Kutokana na fasiri hizi ni bayana kwamba haiponimu ni maneno ambayo huwa na uhusiano fulani wa kimaana. Maneno haya hujumuishwa chini ya neno moja kuu. Uhaiponimu ni sifa ambayo hupatikana katika lugha zote ulimwenguni. Kuwepo kwa haiponimu katika lugha fulani

hui fanya lugha hiyo kuwa na leksimu nyingi za kutajia vifaa vinavyopatikana katika mazingira ya watumizi wa lugha hiyo.

Ileweke hapa kwamba ingawaje lugha zote huwa na sifa za uhaiponimia, uhaiponimia huu hutofautiana sana katika lugha hizi. Kuna lugha ambazo huwa na msamiati mpana sana wa kutajia vitu vinavyopatikana chini ya neno kuu, kuliko lugha zingine. Kwa mfano lugha za Kiswahili na Kiingereza zote zina msamiati wa kutajia neno “mchele.” Lakini lugha ya Kiswahili ina msamiati mpana sana wa kutajia aina mbalimbali za mchele kuliko lugha ya Kiingereza. Katika lugha ya Kiingereza aina yoyote ile ya mchele (uwe umepikwa au la) huitwa tu *rice*. Kwa mfano Kiswahili kina haiponimu zifuatazo za kutajia neno kuu “mchele”



vile vile lugha ya Kiingereza ina msamiati mpana wa kutajia aina za barabara kuliko Kiswahili. Katika Kiswahili barabara yoyote ile huitwa barabara tu. Ifuatayo ni mifano ya haiponimu za kutajia barabara katika lugha ya Kiingereza.



Hii ni mifano ya haiponimu za kutajia aina mbalimbali za barabara hivi kwamba mtu anapotaja maneno kama vile *highway* na *street* katika mazungumzo yake atakuwa anarejelea leksimu za kutajia maana pana ya neno jumuishi, “road.” Lakini mtu anapotaja neno “road” katika mazungumzo yake haina maana bayana kwamba anarejelea maana ndogo ya leksimu “highway” au “street.”

Lugha ya Sheng pia ina sifa za uhaiponimia katika leksimu zake. Mojawapo ya mifano ya haiponimia ambazo tumeweza kubaini kuto kana na uchanganuzi wa data yetu ni kama ifuatayo;

Mfano 1

Sheng	Mfanyakazi
Udijo	konkodi



dere

karaao	kuro
--------	------

Tafsiri

Mfanyakazi
Mwalimu utingo dereva polisi kahaba

Mfano huu wa kihaiponimia unatuonyesha kwamba tunaposema “konkodi”, “dere”ama” karaao” huwa tunarejelea mfanyakazi. Lakini tunaposema mfanyakazi si bayana kwamba tunamrejelea “konkodi,” “dere,” ama “karaao.” Haiponimu hizi vile vile hutumiwa na jamiilugha ya Sheng katika utugaji wa sentensi. Sentensi hizi ndizo wao huzitumia katika mawasiliano yao na katika utekelezaji wa vipaji vyao vya kisanaa kama vile uimbaji. Ifuatayo ni mifano ya sentensi zenyet kujumuisha haiponimia, kama zilivyojidhihirisha katika data yetu.



(Uchanganuzi wa sentensi: mbinu ya wanamiundo)

Sentensi hii imeundwa kwa kutumia haiponimia za Sheng ambazo zimejumuishwa na leksimu zingine za Sheng. Haiponimia hizi ni pamoja na “dingo,” na “kara.” Leksimu hizi (au haiponimu) za Sheng zimeundwa kwa kutumia mbinu mbili tofauti. Leksimu / *dingo:/* ni leksimu ambayo imeundwa kwa mbinu ya ubadilishaji silabi. Neno awali lilitamkwa kama / mgodi: / leksimu hii si leksimu kopwa ila ni leksimu buniwa iliyokuwemo katika misamiati ya Sheng ya zamani. Watumizi wa Sheng ya leo wameifanyia leksimu hii mabadiliko kwa kudondosha mofu ya umoja {m}. Halafu baadaye wakazibadilisha kinyume nyume mofu za mzizi wa leksimu hii kabla ya kuchopeza mofu {n}. Mofu {n} ilichopekwa katika leksimu hii ili kurahihisha matamshi ya leksimu, “*dingo.*” Leksimu “*kara*” ni leksimu ya Sheng ambayo imeundwa kwa mbinu ya ubunifu. Leksmu hii ina maana ya “*polisi.*” leksimu *kara* na *dingo* ni haiponimu za neno kuu ambalo ni “*mfanyakazi.*” Leksimu zingine za Sheng ambazo zimetumiwa katika uundaji wa sentensi hii ni pamoja na; “alisanya,” “walenje” na “nganya.” Leksimu hizi zikitafsiriwa zina maana zifuatazo;

- a) Alisanya = aliiba
- b) Walenje = kipochi
- c) Nganya = matatu

3.2 Sinonimia

Usinonimu huwa uhusiano wa kileksika. Katika uhusiano huu maumbo fulani ya maneno katika lugha huwa na maana sawa. Kwa wakati mwingine maumbo haya yenye maana sawa pia huitwa visawe. Kwa hivyo sinonimia ni visawe vya dhana moja (Habwe na Karanja, 2011:209).

TUKI (2009:897) nayo inafasiri maana ya neno sinonimu kwa kusema kuwa sinonimu ni moja kati ya maneno mawili au zaidi yanayokaribiana sana katika maana. Sinonimu na usinonimu ni dhana mbili zenye fasiri zinazooana. Usinonimu huwa uhusiano uliopo baina ya maneno mawila au zaidi ambayo maana zake zinakaribiana sana (Kamusi Sanifu ya Fasihi na Lugh. 1990: 55). Hivyo basi michakato tunayoitumia tunapochambua maana msingi ya neno ”sinonimu” ndiyo ambayo inajulikana kama usinonimu.

Kamus Sanifu ya Isimu na Lugha (1990:55) nayo inafasiri neno sinonimu kwa kusema kuwa; “usinonimu ni uhusiano uliopo baina ya maneno mawili au zaidi ambayo maana zake zinakaribiana sana.” Kwa mfano lugha ya Kiswahili ina mifano ifuatayo ya sinonimu;

Neno	sinonimu zake
Mtu	= mja, mahuluki, binadamu, adinasi, mwanadamu
Pesa	= fedha, hela, darahima, njenje, ngwenje
Shamba	= konde, mgunda
Ogonjwa	= uele, maradhi
Daktari	= tabibu, mganga
Mama	= nina, nyoko
Mungu	= Mola, Mterehemazi, Jalali, Maulana

Sinonimu hufasiriwa kama maneno yenye maana inayokaribiana kwa sababu maana za maneno hayo huwa hazilingani moja kwa moja au kufanana kama shilingi kwa ya pili. Kwa mfano, neno *rafiki* na *mwendani* ni maneno ambayo yana uhusiano wa usinonimu. Hata hivyo maana za maneno haya hazilingani moja kwa moja. Utuftuti finyu uliopo kati ya sinonimu hizi unatokana na fasiri za maneno haya. Yaani, rafiki ni mtu ambaye mna uhusiano naye lakini uhusiano huo ni wa mbali kwa kiasi fulani, lakini mwendani ni mtu ambaye uhusiano uliopo kati yenu ni wa karibu sana.

Kuwepo kwa usinonimia katika lugha fulani huchangiwa na mambo kadha. Mambo haya ni pamoja na ukopaji wa msamiati, jinsia, dini, tofauti za kimaneno, tofauti za kilahaja, taaluma, na wakati.

Katika uchanganuzi wa data yetu tumebaini kwamba Sheng pia inazo sinonimu. Inaaminika kwamba sinonimu za Sheng zimetokana hasa na kule kubadilikabadilika kwa leksimu za lugha

hii kila mara. Jambo lingine ambalo limechangia kuwepo kwa usinonimu katika Sheng ni vijilahaja vyta lugha hii ambavyo huzungumzwa katika mitaa mbalimbali kama vile mashariki, magharibi, kusini na kaskazini mwa jiji la Nairobi. Ifuatayo ni mifano ya sinonimu za Sheng jinsi zilivyojidhihirisha katika data yetu.

Sheng	Tafsiri
a) Shore _____ msupa	a) msichana ----- binti
b) Ndai _____ dinga	b) gari ----- motokaa
c) Buda _____ mbuyu	c) baba ----- abu
d) Ferare _____ Bufee	d) nauli ----- nauli
e) Keroro _____ tei	e) pombe ----- tembo
f) Manyura _____ dedi	f) kufa ----- kuaga

Ingawaje sinonimu za lugha zilizostawi huwa na maana zinazokaribiana sana, hivi sivyo ilivyo na sinonimu za Sheng. Sinonimu za Sheng huwa na maana yenye kulandana hivi kwamba leksimu mbili zenye sifa za usinonimu zinaweza kubadilishana nafasi katika utungo bila ya kulegeza wala kubadili maana msingi ya utungo husika. Ufuatao ni mfano wa sentensi zenye kujumuisha sinonimu za Sheng.

Sheng: a) [Ule [[uchiwa] ulimchocha Kama]]

N² N¹ N⁰

b) [Ule [[usupa] ilimchocha Kama]]

N² N¹ N⁰

Tafsiri: a) [Ule [[urembo] ulimhadaa Kamau]]

N² N¹ N⁰

b) [Ule [[uzuri] ulimhadaa Kamau]]

N² N¹ N⁰

(Uchanganuzi wa sentensi: mbinu ya X=bar)

Sentensi za Sheng za (a) na (b) ni sentensi zenyе usinonimu wa kileksimu. Sinonimu ambazo zimetumika katika uundaji wa sentensi hizi ni / uchiwa / na / usupa /. Leksimu *uchiwa* ni leksimu ya Sheng ambayo imeundwa kwa mbinu ya ubunifu, ikiwa na maana ya *urembo*. leksimu *usupa* ni leksimu ya Sheng imbayo imeundwa kwa mbinu ya ukopaji na utohozi. Mzizi kopwa na toholewa wa leksimu hii ni *-supa* kutokana na neno la Kiingereza *supper* lenye maana ya *uzuri* wa *kupindukia*. Mzizi huu “- supa” umepachikwa kiambishi *u* cha unominishaji ili kuunda nomino, “*usupa*” yenye maana ya ,”*uzuri*” au “*urembo*.” Leksimu *uchiwa* na *usupa* ni sinonimu za Sheng ambazo zina maana sawa. Usawe wa sinonimu hizi unatokana na sababu kwamba leksimu hizi mbili hutumiwa na jamii ya Sheng kwa kurejelea urembo wa msichana pekee. Leksimu hizi mbili zinapotafsiriwa katika Kiswahili tunaishia kupata maneno *urembo* na *uzuri*. Katika Kiswahili maneno haya mawili huwa hayatumwi kwa kurejelea maana moja. Leksimu *urembo* hutumiwa kwa kurejelea jinsia ya kike na leksimu *uzuri* hutumiwa kwa kurejelea jinsia ya kiume. Hivyo basi sinonimu za Sheng huwa na maana sawa. Usawe huu huchangiwa na sababu kwamba maneno katika lugha hii hubadilishwa badilishwa kimakusudi ili kuakisi sifa ya ufichaji wa siri mionganoni mwa wanajamii wa lugha hii.

3.3 Homonimu

Neno Homonimu ni neno la Kigiriki “homonumos” lenye maana ya, “Kuwa na maana sawa.” Neno hili limeundwa kwa maneno mawili. Maneno haya “homo” lenye maana ya “sawa” na “onomo” lenye maana ya “maana”. Maneno haya mawili hivyo basi yanapowekwa pamoja huibua maana ya, “dhana zenyе maana sawa.”

Hivyo basi neno *homonimu* lina maana ya, uhusiano wa kileksia ambapo maneno huwa yanafanana katika maumbo yake lakini maneno haya huwa na maana tofauti. Yaani kufanana huku kwa maneno huwa kwa kisadfa tu. Maneno haya huwa hayana usuli mmoja wa kihistoria. Hivyo basi, maana za maneno haya huwa tofauti kimsingi (Habwe na Karanja, 2011:212). TUKI (2009: 426) inafasiri neno Homonimu kama neno linalofana na jingine lakini lenye maana tofauti. Neno “kufanana” katika fasiri hii lina maana ya maneno yenye umbo au muundo sawa.

Kamusi sanifu ya Isimu na Lugha (1990:30) nayo inatoa fasiri ya homonimu kwa kusema kuwa; homonimu ni leksimu mbili au zaidi katika lugha moja zenyе kuandikwa sawa lakini zenyе

maana tofauti. Kiisimu homonimu ni neno moja kati ya kikundi cha maneno ambayo hushiriki muundo sawa na sauti sawa lakini yenyne maana tafauti.

Kutokana na fasiri hizi za neno “homonimu” tunapata kufahamikiwa kwamba homonimu huwa na uwezo wa kumiliki sifa za homografu na homofoni mtawalia. Lugha kama vile Kiingereza, Kiswahili na Sheng huwa na maneno mengi yenyne sifa za uhomonimu katika jumla ya leksika yazo. Kwa mfano lugha ya Kiingereza ina mifano ifuatayo ya homonimu.

Neno		Maana
Stalk	:	Sehemu ya mmea
	:	Fuata au sumbuu mtu
Row	:	Mzozano
	:	M pangilio wa mwandamano
Left	:	Mkono wa kushoto
	:	Kuondoka/kuacha
Sow	:	Upanzi wa mbegu
	:	Nguruwe wa kike
Head	:	Kichwa
	:	Kuelekea

Nayo lugha ya Kiswahili ina mifano ifuatayo ya homonimu

Neno		Maana
Panda	:	Kutia mbegu udongoni ili ziote
	:	Kukwea

{	Kaa	:	Aina ya mnyama wa majini
	Kaa	:	Kuketi
{	Paa	:	Kitendo cha kwenda juu
	Paa	:	Sehemu ya mbele ya kichwa
{	Meza	:	Kifaa cha kuandalia chakula
	Meza	:	Kupitisha chakula kooni hadi tumboni
{	Kamba	:	Uzi mnene
	Kamba	:	Aina ya samaki wa baharini
{	Mbuzi :	:	Mnyama mdogo wa nyumbani
	Mbuzi	:	Chombo cha kukunia nazi
{	Tembo	:	Ndovu
	Tembo	:	Pombe
{	Shuka	:	Kipande cha nguo. Leso au kitambaa
	Shuka	:	Teremka.

 Nyanya Nyanya	:	Mama mzaa baba au mama Tunda la mnyanya
--	---	--

 Chungu Chungu Chungu Chungu Chungu	:	Kifaa cha mfinyanzi cha kupikio Ainda za madudu Kuwa na maumivu Kwa wingi Ukali wa kitu
---	---	---


Kutokana na mifano hii ya homonimu za Kiswahili na Kiingereza, tunapata kuelewa kwamba katika lugha, kuna maneno ambayo huwa na umbo moja na sauti moja lakini usuli na maana za maneno hayo huwa mambo mawili tofauti. Umbo moja la neno fulani linaweza likawa na maana tofauti zaidi ya moja. Mifano ya madai haya ni kama inavyojibainisha katika mifano iliyopo hapo juu. Hata hivyo kuna wanataluma na kamusi kadhaa ambazo hudai kwamba homonimu huwa maneno yenye maana zaidi ya moja. Mifano ya wanataluma hawa ni Wala Bin Wala (2012: 117).


Sheng pia huwa na leksimu ambazo huakisi fisa za uhomonimu. Homonimu za Sheng hutokana na maneno yaliyokopwa kutoka lugha zingine. Baadhi ya maumbo ya maneno kopwa haya huwa yanafanana. Hivyo basi maumbo hayo ya majina ambayo hufanana, hupewa uwezo wa kumiliki maana toautitofauti. Ifuatayo ni mifano ya homonimu ambayo tuliweza kuibani katika Sheng.

Sheng **Tafsiri**

- a) Chapa kafilisika
 Chapa kukonda
- b) Chuo shule ya chekechea
 Chuo shule ya msingi
 Chuo shule ya upili
 Chuo shule ya anuai
 Chuo chuo kikuu
- c) Keja nyumba ya mtu
 Keja nyumba ya mbwa
 Keja nyumba ya kuku
 Keja nyumba ya mbuzi
- d) Finga Ishara ya kujamiana
 Finga Ishara ya matusi


Lugha ya Sheng humiliki uwezo wa kutunga sentensi zenyе sifa za uhomonimu.wanajamii wa Sheng huzitumia sentensi hizi katika kufanikisha mawasiliano mionganoni mwao. Mifano ya sentensi za Sheng zenyе sifa ya uhomonimia ni pamoja na hizi zifuatazo;





: b) Tene Maish| alikuwanga sonko bat tude amechapa

Kiima Kiarifu



b) Zamani Maina| alikuwa tajiri lakini siku hizi amefilisika

Kiima Kiarifu

(*Uchanganuzi wa sentenzi mbinu za wanamapokeo na wanamiundo*)

Sentensi za (a) na (b) ni sentensi ambazo zimetungwa kwa misingi ya sarufi ya Sheng. Sentensi hizi zimeundwa kwa kutumia homonimu *chapa* ambayo imeibua maana tofauti katika sentensi zote mbili ingawaje umbo la leksimu hii ni moja. Vile vile leksimu hii ni leksimu kopwa. Leksimu hii imekopwa kutoka kwenye lugha ya Kiswahili kwa mbinu ya uundaji wa maneno inayojulikana kama *polisemia*. Upolisemia ni mbinu ya uundaji wa leksimu ambapo leksimu ya lugha fulani hupewa maana nyongeza kando na maana msingi ya neno hilo. Katika Kiswahili, leksimu *chapa* huwa na mana ya, "kitendo *cha* *kutia adabu hasa* kwa kutumia *kifaa* kama *vile kiboko; au* *kitendo cha kurudufisha*." Lakini katika Sheng, leksimu hii imepewa maana nyongeza. Katika Sheng leksimu hii ina maana ya, *kukonda au kufilisika*.

Sentensi za (a) na (b) zote zinajumuisha homonimu, “*chapa*.” Homonimu hii imetumiwa kwa maana tofauti katika sentensi hizo mbili. Katka sentensi ya (a) leksimu *chapa* imetumiwa kwa kuibua maana ya “*kukonda*,” na katika sentensi ya (b) leksimu *chapa* imetumika kwa kuibua maana ya “*kafilisika*.” Mifano hii inatudhihirishia kwamba homonimu huwa maneno yenyе maumbo sawa lakini yenyе kumiliki maana tofauti.

Kuna dhana zingine za kiisimu ambazo huwa na fasiri zinazokaribiana sana na uhomonimu. Mifano ya dhana hizi ni pamoja na homografu, homofoni, heteronimu, heterografu na kapitonimu. Mifano ya dhana hizi za kiisimu haikuweza kujitokeza katika data yetu, hata hivyo ni jambo la busara kuzijadili kwa sababu zina uhusiano sana na dhana ya homonimu ambayo ilijitokeza katika uchanganuzi wa data yetu.

3.3.1 Homografu

Homografu ni maneno ambayo huwa na muundo au umbo sawa bila ya kuzingatia jinsi yanavyotamkwa. Homografu ambazo hutamkwa kwa matamshi sawa lakini yenyе kumiliki maana tofauti huitwa “homofoni.” Homografu ambazo huwa na umbo moja lakini hutamkwa kwa namna tofauti nazo huitwa “heteronimu.” Hivyo basi homofoni na heteronimu huwa sehemu ya homografu. Kamusi Sanifu ya Isimu na Luga (1990:30) inatoa fasiri ya neno homografu kwa kusema kuwa; “homografu ni leksimu mbili au zaidi katika lugha moja zinazoendelezwa kwa namna moja ingawa zina maana tofauti.” Ifuatayo ni mifano ya homografu za Kiingereza.

Homografu

Bow

Bow

Rose

Rose

Maana

sehemu ya mbele ya meli

ala ya kutupia mshale

Aina ya ua

wakati uliopita wa neno *rise*

3.3.2 Homofoni

Homofoni hufasiriwa kama maneno ambayo hutajwa kwa matamshi sawa bila ya kuzingatia maumbo au miundo sawa. Homofoni huwa sehemu ya homografu. Kamusi Sanifu ya Isimu na Luga (1990:30) inasema kuwa; “homofoni ni maneno yenyе kutamkwa sawa lakini yenyе kutofautiana kimaana au kitahajia.” Vile vile, homofoni ni neno ambalo hutumiwa kuelezea

maneno ambayo yana sauti moja au matamshi yanayofanana lakini yana tahajia tofauti (Wamitila 2003:62). Ifuatayo ni mifano ya homofoni za Kiingereza.

Neno		Maana
Bark	=	Sauti ya mbwa
Bark	=	Ngozi ya mti
Threw	=	Wakati uliopita wa neno <i>throw</i>
Through	=	Kuanzia mwanzo hadi mwisho
See	=	Ona
Sea	=	Bahari

3.3.3 Heteronimu

Heteronimu huwa seti za homografu (maneno yenye maumbo sawa) lakini hutamkwa kwa namna tofauti. Vile vile heteronimu huwa na maana tofauti. Mifano ya heteronimu katika Kiingereza ni pamoja na;

Heteronimu		Maana
Desert	=	Ketekeleza
Desert	=	Sehemu kame
Row	=	Pingamizi
Row	=	Kitendo cha kuendesha mashua

Lugha ya Kiswahili nayo ina mfano ufuatao wa heteronimu;

Heteronimu		maana
Barabara	=	njia inayotumiwa na binadamu na magari
Barabara	=	sawasawa

Mifano ya heternimu haikuweza kujitokeza katka data ya utafiti wetu. Hii kwetu ilikuwa na maana kwamba lugha ya Sheng bado haijaanza kukuza leksimu zenye sifa za kiheteronimu. Hivyo basi tulikosa mifano ya kuambatisha au kuorodhesha katika utafiti huu.

3.3.4 Kapitonimu

Kapitonimi ni maneno ambayo huwa na maumbo sawa lakini huwa na maana tofauti yanapoandikwa kwa herufi kubwa. Mifano ya maneno haya katika Kiingereza ni pamoja na;

Neno	Maana
Polish	Raia wa taifa la Poland
Polish	Kufanya viatu vimeremete
March	Kuenda mbele kwa mpangilio maalum
March	mwezi wa tatu katika mwaka

La msingi kueleweka hapa ni kwamba maneno haya yanapoandikwa mwanzoni mwa sentensi basi huwa ni lazima yaanze kwa herufi kubwa. Lakini yanapokuwa katikati au mswishoni mwa sentensi, neno moja huandikwa kwa herufi kubwa au ndogo kwa kutegemea kategoria ya maneno haya. Tazama mifano ya sentensi zifuatazo.

- a. John came to polish your shoes.
- b. John is a Polish tourist.

Mifano ya kapitonimi haikujitoza katika data yetu. Hivyo basi Sheng bado haijawa na leksimu zenye kuakisi sifa za ukapitonimi. Labda sifa za ukapitonimi zitaanza kushuhudiwa katika Sheng jinsi miaka inavyozidi kusonga na jinsi Sheng inavyozidi kupanua mawanda yake ya matumizi.

3.4 Polisemia

Upolisemia ni aina nyingine ya mahusiano ya kifahiwa ambayo tuliweza kuishuhudia katika utafiti wetu. Je, polisemia ni nini? Neno polisemia hutumiwa kwa kuelezea hali ambapo neno moja huwa na maana zaidi ya moja (Wamitila 2003:176). Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha (2003:46) nayo inafasiri neno “polisemia” kwa kusema kuwa; “polisemia ni hali ya neno moja kuwa na maana zaidi ya moja.”

Ni jambo la busara kuelewa kwamba kuna tofauti kubwa sana kati ya polisemia na homonimu. Tunasema hivi kwa sababu kunao wanataluma kadhaa ambao kwao dhana hizi mbili huwa na maana sawa. Hivyo basi wao huzipatia dhana hizi mbili neno moja jumuishi ambalo ni “visawe.” Huu si ukweli. Homonimu huwa maneno yenye maumbo sawa lakini maana na usuli wa maneno

hayo huwa tofauti. Polisemia nazo huwa maneno yenyenye maana zaidi ya moja. Maneno haya huwa na historia moja. Polisemia ni uhusiano ambapo kuna umbo moja la neno lenye maana mbalimbali (Habwe na Karanja 2012: 213). Kwa mfano Kiswahili kina mifano ifuatayo ya polisemia;

Neno	Maana
a) Mdomo	= wa mto
	= wa mtu
	= wa chupa
	= wa pango
	= wa sindano
	= wa jipu
	= wa mtungi
b) Jicho	= la mtu
	= la sindano
	= la Mungu
	= la serikali
	= la kamera

- c) Kiu = ya maji
 = ya uongozi
 = ya mapenzi
- d) Ua = mtu
 = mkataba
 = amani
 = njia
- e) Kiti = cha mamlaka
 = cha kukalia

Sheng pia ina mifano kadhaa ya polisemia. Mifano hii ya polisemia tuliibaini kutokana na uchanganuzi wa data yetu. Tazama mifano ifuatayo:

- i. Bast = Angua kicheko
 = Kupata panchari
 = Kutaniwa
- ii. Finga = Kidole cha mtu
 = ishara ya kujamiana
 = ishara ya matusi

Leksimu hizi zenyе sifa za upolisemia hutumiwa na jamii ya Sheng katika utungaji wa sentensi ambazo wao huzitumia katika mawasiliano yao na katika kuwasilisha hisia na maoni yao kwa kutumia sanaa kama vile sanaa ya nyimbo na uimbaji. Mifano ya sentensi za Sheng zenyе sifa ya upolisemia ni pamoja na hizi zifuatazo;

Sheng : a) Taya ya nganya ya pasi ilibast jana akikam chach.
 : b) Songs zingine za Saajaa zinaweza zikakufanya ubast.



Tafsiri : a) Gurudumu la gari ya mchungaji lilipasuka jana akija kanisani.
 : b) Nyimbo zingine za Mungu zinaweza zikakufanya ucheke.

Leksimu ‘bast’ ni leksimu ambayo ina sifa za upolisemia kwa sababu vitendo vyote vinavyotokana na leksimu hii huhusisha sauti. Yaani, gurudumu linapopasuka ‘bast’ linatoa sauti na mtu anapocheka ‘bast’vile vile anatoa sauti. Leksimu hii ‘bast’ ni leksimu kopwa. Leksimu hii imekopwa kutoka katika lugha ya Kiingereza kwa kutumia mbinu ya uundaji wa maneno inayojulikana kama, “ukopaji na utohozi.” Kwa hivyo katika Sheng leksimu hii huchukuliwa kama mzizi. Mzizi huu huweza kuambishwa mofu za wakati, njeo, nafsi na hali. Mfano wa madai haya ni kama ufuatao;

Sheng:

Taya imebast.

Tafsiri: Gurudumu limepasuka.





(Uchanganuzi wa kirai nomino: nadharia ya x – bar)

Mojawapo ya maana za neno hili ni, “*kupasuka kwa kitu kwa sauti ya juu.*”

Mifano ya polisemia katika Sheng haikujidhihirisdha sana katika data yetu. Jambo hili lilitokana na sababu kwamba Sheng ni lugha ambayo bado inazidi kukua. Yaani kwa sasa Sheng bado ni lugha changa sana. Jinsi muda unavyozidi kuenda ndivyo lugha hii itakavyozidi kukomaa na hivyo basi kuwa na umiliki wa dhana nyingi za kiisimu ambazo kwa sasa haina.

3.5 Antonimia

Kundi lingine la maneno ambalo huonyesha uhusiano wa kifahiwa ni kundi linalojulikana kama ‘antonimia.’ Wamitila (2003: 24) anaifasiri istilahi hii kwa kusema kuwa; “Istilahi hii hutumiwa kwa kuelezea neno ambalo lina maana kinyume na jingine.” Antonimia huwa na umuhimu mkubwa sana katika isimu hivi kwamba huweza kumsaidia mtu kupata maana ya neno moja kwa kutumia kinyume cha neno jingine.

Habwe na Karanja (2010: 213) nao wanaifasiri istilahi hii kwa kusema kwamba; antonimu ni uhusiano wa kumuundo. Huu ni uhusiano ambapo kuna maneno katika lugha ambayo maana zake huwa vinyume. Katika hali hii maneno hupingana. Maelezo na fasiri hizi ziliweza kutuongoza katika kupata mifano ifuatayo ya antonimu za Kiswahili.

Antonimia za Kiswahili

Neno ***kinyume***

Baba = *mama*

Kijana = *mzee*

Shangazi = *mjomba*

Mvulana = *msichana*

Pia tuliweza kubainisha kwamba lugha ya Sheng pia inayo sifa hii ya antonimia. Mifano ya antonimu katika Sheng ni kama ifuatayo.


Antonimia za Sheng

Tafsiri

	<i>Neno</i>	<i>kinyume</i>		<i>neno</i>		<i>kinyume</i>
a)	Hot	=	kul	a)	moto	= baridi
b)	Nakulav	=	nakuhet	b)	nakupenda	= nakuchukia
c)	Kamu	=	zidi	c)	njoo	= nenda
d)	Holijoo	=	ivo	d)	mtakatifu	= mwovu
e)	Dere	=	konkodi	e)	dereva	= utingo
f)	Mbuyu	=	madhee	f)	baba	= mama
g)	Sonko	=	hasla	g)	tajiri	= maskini
h)	Chali	=	manzi	h)	mvulana	= msichana
i)	Udijoo	=	stude	i)	mwalimu	= mwanafunzi

Habwe na Karaja wanatoa maelezo zaidi kuhusu antonimia kwa kusema kuwa; mara nyingi katika lugha huwa kuna vinyume vya viwango na vinyume vya utoano. Mifano ya Vinyume vya

viwango ni kama *moto / baridi*, *juu / chini*, *mbele / nyuma*. Mifano Hii ina maana kwamba haya ni maneno yenye maana ambazo ziko kwenye mkondo mmoja. Tazama mfano huu jinsi unavyojitokeza katika Sheng. Ufuatao ni mfano wa vinyume vya kimtoani katika Sheng.



Aina nyingine ya antonimia huwa antonimia za kimtoano. Mifano ya antonimu za kimtoano ni pamoja na;

Sheng

Tafsiri

<i>Neno</i>	<i>kinyume</i>	<i>neno</i>	<i>kinyume</i>
--------------------	-----------------------	--------------------	-----------------------

- | | | | | |
|----|---------|-------|--------------|-------|
| a) | Dem = | chali | dem = | chali |
| b) | Shagz = | majuu | mashambani = | ulaya |

Sheng huzitumia leksimu hizi zenye sifa za uantonimia kwa kutunga sentensi. Sentensi hizi hutumiwa na wanajamii wa Sheng katika mawasiliano yao ya kila siku. Mifano ya sentensi za Sheng zenye sifa za uantonimia ni pamoja na zifuatazo.

Sheng: a) yakini: Buda analaik njaro za kuzidi na saajaa tu vinoma.

: **b) Kanushi:** Masa anahet njaro za kuzidi na devoo tu vinoma.

Tafsiri: a) yakini: Baba anapenda sana hulka za kutembea na Mungu

: **b) Kanushi:** Mama anachukia sana hulka za kutembea na Shetani.

	Buda	Masa
Sheng	$\left\{ \begin{array}{l} +mtu \\ +hai \\ +mzima \\ +mme \end{array} \right\}$	$\left\{ \begin{array}{l} +mtu \\ + hai \\ + mzima \\ - mme \end{array} \right\}$
	Baba	Mama
Tafsiri	$\left\{ \begin{array}{l} +mtu \\ +hai \\ +mzima \\ +mme \end{array} \right\}$	$\left\{ \begin{array}{l} +mtu \\ + hai \\ + mzima \\ - mme \end{array} \right\}$

(*Mbinu ya uchanganuzi vijenzi*)

Sentensi hii za Sheng zina sifa za uantonimia. Sifa hizi zinajitokeza kama vinyume katika sentensi za (a) na (b). mifano ya antinimia ambazo zimetumika katika sentensi hizi mbili ni kama ifuatayo;

Sheng		Tafsiri	
<i>Leksimu yakini</i>	<i>Leksimu kinyume</i>	<i>leksimu yakini</i>	<i>leksimu kinyume</i>
a) Buda = Masa		a) Baba = Mama	
b) Analeik = Anahet		b) Anapenda = Anachukia	
c) Saajaa = Devoo		c) Mungu = Shetani	

Leksimu hizi ni leksimu kopwa kutoka katika lugha za Kiingereza na Kiswahili. Leksimu “buda” ni leksimu ambayo imekopwa kutoka katika lugha ya Kiswahili. Leksimu hii imeundwa kwa mbinu mbili tofauti za uundaji wa maneno. Mbinu hizi ni *ukopaji sisisi na upolisemia*.

Ukopaji sisisi ni mbinu ya uundaji wa maneno ambapo neno kopwa huingizwa katika leksimu za lugha kopa bila ya neno hilo kufanyiwa mabadiliko yoyote ya kimofolojia au uhawilishaji. Sifa za upolisemia ambazo zinahusishwa na neno hili ni kwamba, neno hili limepewa maana mpya au maana ya ziada kando na maana yake ya msingi. Maana nyongeza ya neno hili ni “baba” au “mzee.”

Leksimu ‘masa’ ni leksimu ya Sheng ambayo imeundwa kwa mbinu ya ‘ubunifu.’ ‘Analeik’ nayo ni leksimu ya Sheng ambayo imeundwa kwa mbinu ya ukopaji na utohozi. Hili ni neno la Kiingereza ‘like’ lenye maana ya ‘penda.’ Neno hili hutumiwa na Sheng kama mzizi. Mzizi huu huambishwa mofu za njeo, wakati, nafsi, na hali. Mzizi huu huweza kuchukua viambishi awali na viambishi tamati. Viambishi ambavyo vimewekwa kwenye mzizi huu “leik” ni viambishi awali vya nafsi na njeo. Neno hili vile vile limefanyiwa uhawilishaji ili liweza kuchukua muundo wa mofolojia ya Sheng.

Leksimu “saajaa” ni leksimu ya Sheng ambayo imeundwa kwa mbinu ya uambatishaji. Katika mbinu hii, maneno mawili yenye maana tofauti kimsingi, huunganishwa ili kuunda neno jipya na lenye maana mpya vile vile. Kwa hivyo, neno la Sheng “saa” ni neno la Kiingereza “sir” lenye maana ya “bwana.” Neno hili limeambatanishwa na neno lingine la Kijamaika “jah” lenye maana ya “Mungu.” Neno jipya ambalo limeundwa kutokana na uambatishaji wa leksimu hizi mbili ni ‘saajaa.’ Leksimu hii imekopwa, ikatoholewa kabla ya kufanyiwa uhawilishaji ili ikubaliane na muundo wa mofolojia ya Sheng.

Leksimu “divoo” ni leksimu ambayo imeundwa kwa mbinu ya ukopaji na utohozi. Leksimu hii ni ya Kiingereza “devil” yenye maana ya “Shetani.” Leksimu hii vile vile imefanyiwa uhawilishaji ili ikubaliane na muundo wa mofolojia ya Sheng.

HITIMISHO

Katika sura hii ya tatu, tumeshughulikia maana za leksimu za Sheng jinsi *zinavyojitokeza* katika kitengo cha vifahiwa na sentensi. Yaani tathmini yetu katika swala hili ilijikita katika misingi ya vifahiwa vya Sheng na sentensi za Sheng ambazo huundwa kutokana na vifahiwa hivyo. Uchambuzi wa data yetu umetubainishia kwamba maneno na sentensi za lugha hii humiliki na kuchangia kuwapo kwa mahusiano na hali mbalimbali zinazoathiri mikondo ya maana katika

sentensi. Mahusiano tuliyoyashughulikia katika kitengo hiki ni mahusiano ya vifahiwa. Chini ya kigezo hiki cha mahusiano ya vifahiwa, tumeweza kuyashughulikia na kuyatathmini mambo muhimu kama vile vikoa vya maana (haiponimia), sinonimia, homonimia, polisemia na antonimia. Vifahiwa hivi tumevitathmini kwa kuviandamizia mifano ya Sentensi kwa minajili ya kuonyesha jinsi ambavyo vifahiwa hivyo hutumiwa na jamiilugha ya Sheng katika utungaji wa sentensi ambazo wao huzitumia katika mawasiliano yao.

Kutokana na uchanganuzi na tathmini ya vigezo hivi muhimu vya kisemantiki, tumepata kufahamikiwa kwamba lugha hii ya Sheng ina uwezo wa kusababisha athari zozote zile katika asasi mbalimbali za jamii, ikiwemo asasi ya dini ya Kikristo. Vile vile tumepata kuelewa kwamba jamii ya Sheng inao uwezo wa kujitambulisha na au kwa makundi mengine katika jamii kwa kuyatumia mazungumzo ya kisiri ya lugha hii ya Sheng. Sheng ni lugha ya vijana na iwapo mtu ambaye si kijana atajaribu kuzungumza lugha hii katika muktadha wowote ule, Jambo hili huenda likazua hisia tofauti tofauti mionganoni mwa vijana, wazee au jamii yoyote ile husika. Ni katika muktadha kama hu ambapo swala la ujitalishaji litajitokeza. Yaani vijana wa jamiilugha ya Sheng huenda wakajitambulisha na mtu huyo au wakajitenga naye.

Haiponimia na vikoa vya maana ni dhana mbili za kiisimu ambazo tumbaini kuwa zina maana sawa. Kama kuna tofauti yoyote kati ya dhana hizi mbili, basi tofauti hiyo ni finyu sana na hatukuweza kuishuhudia katika data za utafiti wetu aidha kwa kusoma vitabu au kwa majibu tuliyopokea kutoka kwa wanataluma kadhaa tuliohajoji. Hii ina mana kwamba tunapozungumzia dhana ya vikoa vya maana, kwa kiwango kikubwa bado tutakuwa tunazungumzia dhana ya haiponimia. Kwa hivyo, lilikuwa jambo la busara sana kwetu kuielewa historia ya nadharia ya vikoa vya maana kwanza kabla ya kuendelea na uchanganuzi wetu.

Asili ya nadharia ya vikoa vya maana ni nadharia ya vikoa vya maneno, iliyotangulizwa na Jost Trier katika miaka ya 1930. Lakini kulingana na John Lyons mnamo mwaka huu huu, nadharia ya vikoa vya maaana ina mizizi yake ya kihistoria katika nadharia zao Wilhem von Humboldt na Johann Gottfried Herder mnamo miaka ya 1926 na 1928 mtawalia.

Katika miaka ya 1960 Stephen Ullman aliviona vikoa vya maana kama vifaa vya kiisimu vilivyokuwa na jukumu la kudhihirisha na kuendeleza thamani za jamii.

Kulingana na John Lyons katika miaka ya 1970, maneno yanayohusiana katika wazo lolote yalihusishwa na kikundi kimoja cha kikoa cha maana, na kikoa cha maana kilikuwa kategoria moja ya leksimu, aliyoifafanua kama kikoa cha leksimu.

Lyons alitilia mkazo sana tofauti iliyopo kati ya vikoa vya maana na mfumo wa mtandao wa maana.

Katika miaka ya 1980 Eva Kittay aliunda nadharia ya vikoa vya maana yenye sitiari. Mtazamo huu uliundwa kwenye msingi wa dhana kwamba vifaa katika vikoa vya maana huwa na uhusiano mahususi na vifaa vingine katika kikao hicho hicho, na kwamba sitiari hufanya kazi kwa kupangilia upya mahusiano ya kikoa kwa kuyapanga kwenye mahusiano ya kikoa kingine ambacho tayari kipo.

Sue Atkins na Charles Fillmore katika miaka ya 1990 walipendekeza umbo la maana kama mbadala wa nadharia ya kikoa cha maana.

Sentensi tulizojumuisha katika uchanganuzi wa vifahiwa hivi vya Sheng, ni sentensi ambazo zilijitokeza katika data yetu. Sentensi hizi tumezichanganua kwa kutumia vigezo vya sintaksia, lakini hutukuzama ndani ya uchanganuzi wa sentensi hizo kwa sababu utafiti wetu haukukita kwenye sintaksia ila kwenye semantiki.

Umuhimu wa sura hii kwetu kama watafiti ni kwamba, utafiti huu umetuwezesha kufahamu kwamba Sheng kama lugha, pia ina uwezo wa kumiliki vifahiwa na kujitungia sentensi kwa kutumia vifahiwa hivyo. Vifahiwa hivi pamoja na sentensi ambazo jamiilugha hii ya Sheng hujiundia ni mojawapo ya vifaa muhimu ambavyo jamii hii ya Sheng huvitumia katika kufanikisha mawasiliano yao ya kila siku katika kueleza hisia na maoni yao hasa kupitia kwa sanaa ya nyimbo na uimbaji.

Katika sura ifuatayo tunaenda kutathmini na kuchanganua jinsi ambavyo Sheng huweza kutumia, leksimu, vifahiwa na sentensi ambazo hujiundia katika uwasilishaji wa hisia, maoni na mitazamo yao hasa kuhusiana na usambazaji na utangazaji wa injili ya dini ya Kikristo. Katika kuhubiri injili ya dini ya Kikristo, jamiilugha hii ya Sheng hukita katika mbinu ya nyimbo na uimbaji. Yaani wao huhubiri hasa kwa kutumia njia ya uimbaji. Nyimbo hizo za kiinjili huwa zimeimbwa katika lugha ya Sheng. Hivyo basi ujumbe wa kiinjili ambao huwa katika nyimbo hizo huweza

kuwafikia na kuelewaka na watu wachache tu katika jamii. Watu wengine (hasa wale wa jamii ya Wakristo) huwa wanafungiwa nje ya uelewa wa nyimbo hizo. Hali hii hutokana na sababu kwamba wao huwa hawaelewi maneno ambayo hutumiwa katika nyimbo hizo kibayana.

SURA YA NNE

4.0 SHENG NA MAHUBIRI YA INJILI.

Utangulizi

Katika sura ya pili tulitathmini na tukabaini kwamba lugha ya Sheng hujundi leksimu ili kuirutubisha lugha hiyo kwa leksimu nyingi zenye uwezo wa kurahihisha mawasiliano mionganoni mwa jamii hiyo ya Sheng. Katika sura ya tatu tulitathmini data yetu vile vile, na mwishowe tukabaini kwamba lugha ya Sheng ina uwezo wa kumiliki vikoa vya maana hasa katika kitengo cha kifahiwa. Hivyo basi Sheng huvitumia vifahiwa hivi pamoja na maneno iliyojiundi ili kujitungia sentensi mbalimbali katika kiwango cha Semantiki, sawa na jinsi ilivyo tu katika lugha zingine za ulimwengu huu. Hivyo basi lugha hii hujihakikishia kuwa na uwezo wa kusababisha athari chanya na hasi katika asasi zote za kijamii kama vile dini.

Baada ya kuyabaini haya mambo muhimu, vile vile tuliweza kubaini kwamba jamii hii ya lugha ya Sheng huweza kuutumia uwezo huo wao wa kujiundai leksimu na kujitungia sentensi zenye maana za kisemantiki katika kujieleza kwa kutumia vipaji vyao mbalimbali. Wao huvitumia vipaji hivyo vyao ili kuweza kujilinganisha na makundi mengine katika jamii. Vipaji hivi ni pamoja na: utungaji wa mashairi, uigizaji, uimbaji, na mahubiri. Hata hivyo tulibaini kwamba kati ya vipaji hivi vyote walivyo navyo vijana hawa wa jamii hii ya Sheng, uimbaji na uhubiri ndivyo vipaji maalum na vya kipekee ambavyo wao huvitumia pakubwa. Vijana hawa huvitumia vipaji hivi hasa kwa minajili ya kujilinganisha na makundi mengine katika jamii ambayo pia hutumia sanaa ya uimbaji katika usambazaji wa injili. Yaani, Jamii ya Wakristo pia huvitumia vipaji hivi katika kuihubiri injili ya Mungu.

Kabla ya kuendelea na uchanganuzi wa data yetu litakuwa jambo la busara kama tutaitoa fasiri ya neno wimbo. Je, wimbo au sanaa ya uimbaji ni nini? Wapo wataalamu wengi ambao wametoa fasiri za neno “wimbo.” Miongoni mwa wataalamu hawa ni Matei K. (2011:92). Mwanataaluma huyu anafasiri neno wimbo kama tungo za kishairi zenye mahadhi ya kupanda na kushuka kwa sauti, muwala na mapigo ya kimuziki na huwasilishwa kwa kuimba. Ngure (2004) naye anasema kwamba wimbo ni utungo ulio na mdundo na mahadhi ambayo hutamkwa kwa sauti ya kimuziki. Thonya (1978) pia anasema kuwa wimbo ni aina ya ushairi uliotiwa sauti na uliokusudiwa kuimbwa na kuleta maana ya ujumbe kwa jamii.

Maoni haya yanayotolewa na wasomi hawa kwa kweli yanaoana vyema katika ufasiri wa maana ya neno wimbo. Nyimbo na ushairi angalau zote huwa na upandaji na ushukaji wa sauti. Mdundo na mapigo pia ni sifa ambayo huambatanishwa na uimbaji. Maelezo ya wataalamu hawa vile vile yanatufafanulia kwamba nyimbo huimbwa katika muktadha fulani ili maana kusudiwa ipate kueleweka vyema.

Wamitila (2003:109) anasema kwamba nyimbo zina umuhimu wake katika jamii za waafrika kwa sababu hutambulisha jamii kwa kusawiri shughuli na maisha ya jamii iliyobuni nyimbo husika. Kwa mfano, nyimbo kutoka jamii ya wafugaji husheheni msamiati unaohusu shughuli za ufugaji kama vile zizi, mbuzi, ng’ombe, malisho, maji, ukame, magonjwa, mvua na hata kamba. Nyimbo humsaidia binadamu kutakasa hisia zake na pia kutoa hisia za moyoni kama vile kujutia kosa alilofanya, mapenzi, huzuni, furaha, ama ahadi iliyovunjika. (Kamusi ya Karne ya 21 2011)

inafasiri maana ya neno wimbo kwa kusema kuwa; “*wimbo ni maneno na sauti zilizopangwa na zinazopigwa kama ngoma ambazo huwa ni muziki; ni sauti zilizopangwa kimuziki.*”

Nyimbo huwa mbinu majawapo ya kuhifadhi na kuendeleza utamaduni wa jamii husika. Kumbukumbu za matukio muhimu katika jamii huweza kuhifahidhiwa katika nyimbo na zikapitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Nyimbo hutumiwa kwa kuburudisha, kustarehesha, kuelimisha, kuonya na hata kusisimua. Nyimbo hutumiwa kwa kupitisha amali na mambo ambayo jamii inayadhamini.

Kamusi ya Oxford Advanced Learners (2010) nayo inatoa fasiri ya “wimbo” kwa kusema kuwa; “*wimbo ni kifungu kifupi cha muziki kilicho na maneno ya kuimbwa.*” Nyimbo hutumiwa kwa kuwahamasisha watu na kuchochea hisia za kuchangamkia jambo fulani. Kwa mfano nyimbo za kisiasa huweza kuchochea hisia za kuungana pamoja, kutetea haki au kuunga mkono jambo fulani. Nyimbo huakisi ukwasi wa tamaduni na jamii. Ufasaha wa kujieleza (umbuji) na mvuto au uzuri wa kazi ya sanaa (ujumi) ya jamii hujitokeza katika nyimbo. Uteuzi wa maneno, ishara na ujumbe katika nyimbo huonyesha ukwasi wa jamii hiyo kifani. Nyimbo hukuza ubunifu mionganoni mwa wanajamii, uimbaji ni kipawa ambacho hupaliliwa na nyimbo.

Kuna aina tofauti za nyimbo. Yamkini kila jamii huwa na nyimbo zake ambazo hutofautiana na nyimbo za jamii nyingine. Si jambo la kawaida kusikia wimbo wa jamii moja ukiimbwa na jamii nyingine kama hakuna jambo mahususi la kitajriba linalozioanisha jamii hizo mbili. Hii ni kwa sababu wimbo wa jamii katika jamii moja unaweza ukawa matusi au chukizo katika jamii nyingine. Kwa mfano si jambo la kawaida kuusikia wimbo *bufallo soldier* (ulioimbwa na marehemu Bob Marley) ukiimbwa katika ibada za Wakristo. Na iwapo jambo kama hili litatokea basi litazua mjadala fulani mionganoni mwa jamii ya Wakristo na wasiokuwa Wakristo. Baadhi ya nyimbo ambazo hupatikana katika jamii ni pamoja na: -

- a) Nyimbo za kumpa mtoto jina
- b) Nyimbo za bembezi au bembeleza
- c) Nyimbo za chekechea
- d) Nyimbo za tohara

- e) Nyimbo za sifa
- f) Nyimbo za kazi
- g) Nyimbo za mapenzi
- h) Nyimbo za harusi
- i) Nyimbo za kuomboleza
- j) Nyimbo za dini

Utafiti wetu haukukita katika aina hizi zote za nyimbo ila tu katika nyimbo za dini. Hivyo basi tulilenga kuchanganua na kutathmini athari za nyimbo za Sheng katika dini ya Kikristo.

Nyimbo za dini ya kikristo ni nyimbo ambazo huwa na uhusiano na Mungu. Nyimbo hizi huweza kuimbwa na mtu binafsi au makundi ya watu. Ujumbe katika nyimbo hizi hutegemea matukio yaliyopita, yaliyopo au yajayo. Nyimbo hizi (za dini ya kikristo) hunuiwa kuwaelekeza, kuwakumbusha, kuwatia moyo na kuwaelimisha watu katika jamii.

Mwimbaji huweza kutumia lugha kwa ufundi akirejelea tamathali za usemi kama vile methali, mafumbo, nahau, tasfida, sitiari, tanakali za sauti na misemo katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira yake. Nyimbo za dini ya kikristo haswa hutumika na watu kila wanapotaka kunyenyekea mbele za Mungu. Nyimbo hizi huimbwa katika maeneo mengi kama vile makanisani, harusini, mazishini na pia katika nyakati ngumu za kiuchumi zinapotokea kuwalemea wanadamu hasa wale wenye imani ya kikristo. Kwa mfano wimbo ufuatao ni wimbo wa dini ya Kikristo ambao una maudhui ya kumfariji Mkristo.

Cha kutumaini sina

Cha kutumaini sina

Ila damu yake yesu

Sina wema wa kutosha

Dhambi zangu kuziosha

Kwake yesu nasimama

Ndiye mwamba ni salama

Ndiye mwamba ni salama

Ndiye mwamba ni salama

Njia yangu iwe ndefu

Yeye hunipa wokovu

Mawimbi yakinipiga

Nguvu zake ndizo nanga

Damu yake na sadaka

Nategemea daima

Yote chini yakiisha

Mwokozi atanitosha

Nikiitwa hukumuni

Rohoni nina amani

Nikivishwa haki yake

Sina hofu mbele zake

Huu ni wimbo wa dini ya Kikristo wenye lengo la kuwahimiza wakristo kwamba wasizitegemee nguvu au uelewa wao wa mambo ila wamtegemee Yesu kristo. Wimbo huu umeimbwa kwa kutumia rejista ya dini ya kikristo. Yaani, lugha ambayo imetumiwa katika wimbo huu ni lugha ya dini ya kikristo inayoelewaka bayana na wakristo na hata wale wasiokuwa wakristo. Lakini nyimbo zilizoimbwa katika lugha ya Sheng huwa hazieleweki bayana na wakristo wote. Maneno ambayo hutumiwa katika nyimbo hizi huwa na kasoro zake kadha wa kadha za kiisimu

Sanaa ya uimbaji ni sanaa ambayo huwasilishwa katika mitindo mbalimbali ya kimuziki. Mifano ya mitindo hii ni pamoja na: mitindo ya Rege, Rumba, jazz, Afrofusion, na Ufokaji. Hata hivyo utafiti wetu ulibaini kwamba waimbaji wengi wa nyimbo za kiinjili katika lugha ya Sheng hujitambulisha sana kwa uimbaji wa mitindo ya ufokaji (hip hop), Rege na “Afrofusion.” Vile vile tulipata kubaini kwamba mitindo hii ya uimbaji ndiyo iliyo na umaarufu mkubwa mionganoni mwa vijana katika eneo hili la Umoja. Hivyo basi jamii hii ya Sheng huihubiri injili ya dini ya kikristo hususan kwa kutumia mitindo hii ya uimbaji. Mitindo hii ya uimbaji (muziki) ina historia ya chimbuko yazo isiyooana na maadili ya jamii ya Wakristo. Maneno wayatumiayo vijana hawa katika nyimbo hizo zao za kiinjili huzua utata na miigogoro mionganoni mwa wasikilizaji hasa wale wa jamii ya dini ya kikristo.

Kutokana na uchanganuzi wa data yetu, tuliweza kubaini kwamba kuna makundi mawili kinzani katika jamii ya Wakristo. Jambo ambalo limechangia kuwepo kwa makundi haya kinzani katika jamii hii ni matumizi ya Sheng katika kaida za Wakristo. Yaani kuna kundi ambalo hupenda kuabudu kwa lugha ya Sheng na kuna kundi ambalo halipendi kuabudu kwa lugha ya Sheng ila kwa lugha yenyeye kusheheni sajili ya dini ya Kikristo. Mahubiri na nyimbo ni vigezo muhimu sana katika makundi haya mawili. Kundi la Sheng hupendelea sana kuimba na kumsifu Mungu kwa kutumia Sheng nalo kundi ambalo halipendi Sheng hupendelea sana kuimba na kumsifu Mungu kwa kutumia rejista ya dini ya Kikristo. Ukinzani huu wa makundi haya mawili ulianzia mitaani, shulenii na katika sehemu za burudani, lakini leo hii ukinzani huu sasa umeanza kushuhudiwa katika maeneo kama vile makanisani, makongamanoni na katika vyombo vyahabari.

Kulingna na utafiti wetu, tuliweza kubaini kwamba makanisa mengi hasa yale ya kale katu huwa hayakubali mahubiri na nyimbo za injili zilizoimbwa katika Sheng katika utaratibu wa ibada zao. Mifano ya makanisa haya ni pamoja na;

- a) Kanisa la Katoliki,
- b) Seventh Day Adventist,
- c) Anglicana,
- d) P.C.E.A,
- e) Quakers
- f) A.C.K.

Taratibu zote za ibada katika makanisa haya huendeshwa kwa kutumia rejista ya dini ya Kikristo. Mahubiri na nyimbo za kiinjili katika mtindo wa Sheng ni vitu viwili ambavyo havijakubalika kamwe katika makanisa haya. Nafasi ambayo vijana wa jamii hii ya Sheng huipata ili kuitumia lugha hiyo yao katika maswala yanayohusiana na kanisa huwa tu pale wanapokongamana katika makundi yao mbalimbali ya kategoria za waumini.

Mahubiri na nyimbo katika muktadha huu wa dini ya kikristo ni mambo mawili ambayo yana mwingiliano mkubwa hivi kwamba si rahisi kuvitenganisha. Hii ni kwa sababu mtu anapoimba anahubiri, na anapohubiri, anaimba. Mahubiri ya vijana hususan wale walioko katika jamii ya Sheng sana sana huwa yamekita katika kina cha nyimbo na uimbaji.

Umaarufu wa nyimbo hizi jinsi tulivyobaini umekita sana katika sehemu zifuatazo;

- a) Makanisa ya kisasa
- b) Kwenye mikusanyiko ya kiinjili
- c) Katika redio
- d) Katika televisheni
- e) Katika mtandao.

Majukwaa haya ambayo tumeyataja hapo juu yamekuwa yakitumiwa tangu jadi na wafuasi wa dini ya kikristo katika kuihubiri na kuisambaza injili ya dini yao. Luga ambayo wamekuwa wakiitumia katika mahubiri ni lugha yenyeye wingi wa sajili ya dini ya kikristo. Aina hii ya lugha huwa inaeleweka bayana na wafuasi wote wa Kikristo. Hata hivyo, hivi sivyo ilivyo lugha ya Sheng. Lugha ya Sheng ni lugha ambayo huwa haieleweki bayana na wakristo karibu wote katika eneo hili la Umoja. Lugha hii kwa sasa imeyavamia na kuyatamalaki karibu maeneo yote ambayo yamekuwa yakitumiwa na wakristo hapo awali katika kuihubiri injili ya Kikristo. Maeneo haya ni pamoja na yale ambayo tumeyataja hapo juu. Lakini badala ya kuyatumia maeneo haya kwa upkee fulani ambao unaweza ukaleta hisia fulani za utakatifu, lugha ya Sheng hukubalia uchanganyaji wa mambo ya kidini na ya kidunia katika vipindi vya maonyesho yao, ambayo hasa huyawakilisha kupitia vyombo vya habari. Na hivi ndivyo jamii hii ya Sheng huweza kujilinganisha na makundi mengine katika jamii, hususan makundi yaliyomo katika jamii ya dini ya kikristo. Ifuatayo ni mifano ya athari za Sheng jinsi zinavyojidhihirisha katika asasi kadhaa za jamii.

4.1 Sheng na Injili: Kiwango cha kanisani.


Tangu zamani, kanisa limekuwa mahali patakatifu pa kuhubiria injili ya dini ya kikristo. Lugha ambayo imekuwa ikitumiwa imekuwa lugha ya dini hii ya kikristo. Lugha hii hueleweka bayana na wafuasi wote wa dini hii. Sasa tatizo ibuka ni kwamba, imezuka lugha nyingine katika jamii. Lugha hii mpya imepata nafasi ya kujipenyeza na kuingiza leksimu zake katika rejista ya dini ya Wakristo. Lugha hii ina sifa ya kutoeleweka bayana na wafuasi wote wa imani ya Kikristo. Jinsi ilivyo tu na lugha ya dini ya kikristo, lugha hii pia inapigania nafasi yake kanisani ili iweze kukubaliwa na kutumiwa katika taratibu za usambazaji wa neno la Mungu. Mhimili mkuu wa dini ya kikristo ambao umevamiwa ni kanisa. Je kanisa ni nini? Kamusi ya Kiswahili sanifu inafasili neno kanisa kama; *Jengo linalotumiwa na wakristo kufanya ibada; Kanisa ni jumuia ya wakristo.*

Kwa hivyo kutokana na fasiri hii ya neno “kanisa,” tunaweza tukasema kwamba kanisa ni mahali patakatifu wanapozifanya ibada zao wakristo. Katika utafiti wetu, tuliweza kubaini kwamba makanisa ya awali kama vile; Kanisa la Katoliki, Seventh Day Adventist, P.C.E.A, Anglikana na kadhalika kwa kiwango kikubwa huwa hayaruhusu matumizi au utumiaji wa lugha ya Sheng katika taratibu za ibada zao. Vile vile utafiti wetu ulibainisha kwamba makanisa mengi ya kisasa

ndiyo ambayo huipatia Sheng jukwaa kubwa la kufanikisha tartibu za ibada za Kikristo. Mifano ya makanisa haya ni pamoja na;

- a) Jesus is Alive Ministry.
- b) Neno Evangelism Centre.
- c) The Harvest Centre.
- d) Gospel Fire Ministry.

Ufuatayo ni mchoro ambao unafafanua kwa mukhtasari athari za Sheng kama zinavyojidhihirisha katika aina hizi mbili za makanisa: makanisa ambayo yamekuwepo tangu zama za mkoloni na makanisa ambayo yameanza kuchipuza hivi karibuni.



4.1.1 Sheng na Injili: Makanisa ya Zamani.

Utafiti wetu uliweza kutubainishia kwamba matumizi ya Sheng katika makanisa haya bado hayajashika kasi. Sababu ni kwamba makanisa haya bado yanaongozwa na sheria na kaida za zamani kama zilivyotangulizwa na waasisi wa makanisa hayo. Sheria na kaida hizi hupokezwa kutoka kwa kizazi kimoja hadi kizazi kingine. Kwa hivyo, tamaduni hizi ambazo huendelezwa na kuhuishwa na makanisa haya, huinyima Sheng nafasi ya kuzipenyeza leksimu zake katika

sajili ya madhehebu haya ya zamani. Madhehebu haya huwa sehemu ya dini ya Kikristo. Jambo hili ndilo huwanyima vijana wapenda Sheng nafasi ya kujitambulisha na kujilinganisha na makundi mengine ambayo huwa hayapendi kuabudu kwa Sheng katika madhehebu haya ya Kikristo. Hivyo, vijana katika madhehebu haya wameikosa nafasi ya kujieleza kwa kutumia Sheng.

Maoni ya Wachungaji Kuhusiana na Matumizi ya Sheng Kanisani

Katika utafiti wetu tulitaka kuyajua maoni ya Wachungaji wa makanisa haya kuhusiana na ukubalifu wa matumuzi ya Sheng katika ibada za makanisa yao. Tulipowauliza swali hili, asilimia 70% ya Wachungaji wa makanisa haya ilikuwa na maoni kwamba Sheng si lugha inayoweza kutumiwa katika kuakisi taratibu za ibada makanisani mwao.

“Sheng ni lugha ambayo huwa haieleweki kibayana na wafuasi wote wa dini ya kikristo. Nyimbo za injili ambazo huwa zimeimbwa katika lugha hii pia huwa henzieleweki moja kwa moja. Hali hii ni kinyume na sifa za lugha ya dini ya kikristo. Lugha ya dini ya Wakristo ni lugha ambayo inastahili kueleweka bayana na wafuasi wote . Lugha hii ya dini ndiyo ambayo sisi hutumia kwa kuwaelimisha, kuwakosoa na kuwaelekeza waumini wa makanisa yetu,” walisema

Kulingana na Wachungaji hawa, nyimbo za injili zilizoimbwa katika lugha ya Sheng huwa na ‘kasoro’ zifuatazo’;

- a) Nyimbo hizo huwa henzieleweki bayana,
- b) Huwa na upungufu wa mafundisho ya maadili mema hasa kwa misingi ya dini ya kikristo
- c) Huchanganya jumbe za kidini na za kidunia kwa pamoja. Jambo hili walilichukulia kuwa sawa na kuyachanganya mambo maovu na mambo mema.

4.1.1.2 Maoni ya Wafuasi Wazima Kuhusiana na Matumizi ya Sheng Kanisani.

Swali hili pia tulilielekeza kwa wafuasi wa makanisa haya. Wafuasi tuliwalenga walikuwa wale walio na umri wa miaka 35 na kuendelea. Asilimia 60% ya wafuasi hawa ilikuwa na maoni hasi yaliyohusiana na matumizi ya Sheng katika ibada za makanisa hayo yao. Asilimia hii ilikuwa na maoni kwamba Sheng ni lugha ambayo huwa inatumia na makundi yenye sifa mbaya katika jamii. Mifano ya makundi (ambayo hutumia Sheng) tuliyotajiwa ni pamoja na;

- a) Wevi
- b) Wabakaji
- c) Walanguzi wa dawa za kulevya
- d) Makahaba
- e) Waraibu wa dawa za kulevya
- f) wahuni

Kulingana na wafuasi wenye umri huu, nia ya makundi haya ambayo huwafanya kuwasiliana kwa Sheng huwa kuficha siri za mazungumzo yao ili yasipate kueleweka na watu wasiokusudiwa. Mengi ya makundi haya huwa yanamilikiwa na vijana kuliko wazee. Makundi haya huchukuliwa kama makundi maovu katika jamii. Na kwa vile Sheng inahusishwa na makundi haya mabaya, basi si vizuri kwa lugha hii kutimiwa katika ibada za makanisani.

Asilimia 40% ya wafuasi wenye umri huu ilikuwa na maoni kwamba Sheng inastahili kupewa fursa ya kutumika katika ibada za makanisani. Sababu waliyoitoa ni kwamba Sheng ni lugha ya vijana na iwapo Sheng itakubaliwa kufanikisha taratibu za kuendesha ibada za makanisani, basi mambo yafuatayo yangetendeka;

- a) Vijana wengi watavutiwa kushiriki ibada za makanisa
- b) Vijana hawa watahisi kuwa wao pia ni sehemu muhimu ya makanisa haya
- c) Vijana watapata fursa ya kujieleza kwa kutumia Sheng na hivyo basi wataweza kuwafikia vijana wengine wengi na kuwashawishi ili waweze kuachana na mienendo yao mibaya katika jamii.

4.1.1.3 Maoni ya Vijana Kuhusiana na Matumizi ya Sheng Kanisani.

Kuhusiana na swali hili, vijana ambao ni wafuasi wa makanisa haya nao walikuwa na maoni ya aina mbili: kuna wale waliokuwa na maoni hasi na kuna wale walipkuwa na maoni chanya kuhusiana na matumizi ya Sheng katika ibada za makanisa. Asilimia 52% ya vijana hawa ilikuwa na maoni kwamba Sheng haistahili kutumiwa katika ibada za makanisa. Vijana hawa walikuwa na sababu zifuatazo za kuiunga mkono kauli hiyo yao;

- a) Sheng ni lugha ambayo huwa haieleweki bayana na wafuasi wote wa makanisa yao.
- b) Watu wengi huihusisha Sheng na watu ambao hutenda mambo mabaya katika jamii.

Kulingana na vijana hawa, Sheng ikianza kutumiwa katika kufanikisha taratibu za ibada makanisani, basi jambo hili litakuwa na maana kwamba kanisa limeanza kuyachanganya mambo ya kidunia ya yale ya dini katika taratibu za kumwabudu Mungu.


Asilimia 49% ya vijana hawa nayo ilikuwa na maoni kwamba Sheng inastahili kupewa fursa ya kutekeleza majukumu kadha ya kufanikisha taratibu za makanisani. Kulingana nao, Sheng ni lugha ambayo ina umaarufu mkubwa sana mionganini mwa vijana wa eneo la Umoja. Kwa hivyo ni bora Sheng ikubaliwe kutumika katika kufanikisha taratibu za ibada ili vijana wengi wapate mvuto wa kujiunga na makanisa haya. Kwa maoni yao, Jambo hili lisipotendeka basi makanisa haya yatawapoteza vijana kwa makanisa mengine.

Asilimia hii (49%) ya vijana ilikuwa na maoni yaliyowiana pakubwa na yale ya Viongozi na washiriki wazee katika makanisa haya. Labda hii ilitokana na malezi na mafunzo ambayo wameyapokea kutoka kwa wazazi hao wao ambao pia ni waumini wa aina hii ya makanisa. Hata hivyo, kunao wale waliopendekeza kwamba wanastahili kupewa fursa kwa asilimia fulani ili waweze kuziendesha taratibu fulani za ibada kwa kuitumia lugha ya Sheng. Tulipowauliza kama wanawajua wanamuziki wa nyimbo za kiinjili ambao huimba katika lugha ya Sheng, jibu lao lilikuwa “ndiyo.” Mifano ya wanamuziki hao tuliotajiwa ni pamoja na;

- a) Juliani
- b) Jimmy Gait
- c) Eko Dida
- d) M.O.G.

- e) Kambabas,
- f) Verbal

Ingawaje vijana hawa (ambao huabudu katika makanisa haya ya zamani) bado hawajaathiriwa na matumizi ya Sheng katika taratibu za kutekeleza ibada za makanisa yao, jambo hili li njiani. Jambo hili tuliweza kulibaini kutokana na jinsi ambavyo vijana hao waliweza kututajia majina ya wanamuziki ambao wameimba nyimbo za injili kwa lugha ya Sheng. Uwezo wao wa kuwataja wanamuziki hawa una maana kwamba vijana hawa tayari wamewahi kuzisikiliza nyimbo za wanamuziki hao na, tayari wameanza kuvutiwa na wanamuziki hao pamoja na lugha yao (Sheng) wanayoitumia katika sanaa hiyo yao ya uimbaji. Ufuatao ni mnara unaofafanua kwa mukhtasari maoni ya waumini wa dini za Kikristo ambazo zimekuwepo tangu zamani.



4.1.2 Sheng na Injili: Makanisa ya Kisasa.

Utafiti wetu ulitubainishia kwamba Sheng ina nafasi kubwa sana ya kufanikisha taratibu za ibada katika makanisa ya kisasa. Makanisa haya huwapatia vijana nafasi ya kutekeleza majukumu kadha ya ibada kwa kutumia Sheng. Majukumu haya ni pamoja na;

- a) Kuhuburi

- b) Kuongoza maombi
- c) Kuimba nyimbo za ibada
- d) kukariri mashairi

Makanisa haya ya kisasa huwa na ibada zaidi ya moja. Kati ya ibada hizi kuna zile ambazo huwa zimeratibiwa kuongozwa na vijana, kuna zile ambazo huwa zimeratibiwa kuongozwa na watu wazima na kuna zile ambazo huwa zimeratibiwa kuongozwa na vijana na watu wazima kwa pamoja. Ibada za vijana hutekelezwa pakubwa kwa lugha ya Sheng kuliko ibada za watu wazima. Mifano ya makanisa haya ni pamoja na;

- a) Maximum Miracle Centre
- b) Jesus is Alive Ministry
- c) Overcomers Evangelistic ministries
- d) God's favour ministry

Katika makanisa haya, vijana hupewa fursa ya kujieleza kwa kutumia Sheng katika taratibu kadhaa za ibada kama vile; uimbaji na katika mijadala ya makundi yao kama vijana.

4.1.2.1 Maoni ya Wachungaji Kuhusiana na Matumizi ya Sheng Kanisani.

Ili kuzitathmini athari za lugha hii katika makanisa haya ya kisasa, tulilenga kupata maoni kutoka kwa makunde matatu ya wafuasi wa aina hizi za makanisa. Makundi haya ni pamoja na wachungaji wa makanisa haya, watu wazima, na vijana.

Asilimia 70% ya wachungaji katika makanisa haya ilikuwa na maoni kwamba ukubalifu wa utumiaji wa Sheng katika makanisa haya ya kisasa umewavutia vijana wengi katika makanisa haya na hivyo basi kuwalazimu kuzihudhuria ibada za makanisa. Wachungaji hawa walikuwa na maoni haya yaliyowiana;

"Jinsi dunia inavyobadilika kila kuchao ndivyo mambo yanavyostahili kubadilika vile vile, Ili kuweza kuyaafikia mahitaji ya mabadiliko hayo. Hivyo basi kanisa halistahili kuachwa nyuma na mabadiliko hayo. Lugha ya Sheng ni mojawapo ya mabadiliko haya ya kidunia. Hivyo basi

kanisa linastahili kuyakubalia matumizi ya lugha hii katika kaida na ibada za dini ya kikristo. Inastahili kuwapa vijana fursa ya kujieleza na kuhubiri neno la Mungu kwa njia wanayoilewa vyema,” walisema.

Hata hivyo wachungaji hawa wote walikiri kuwa huwa hawazielewi bayana jumbe na mafunzo ambayo hupatikana katika mazungumzo na nyimbo za kiinjili ambazo huimbwa na vijana hao.


4.1.2.2 Maoni ya Watu Wazima Kuhusiana na Matumizi ya Sheng Makanisani.

Kuhusiana na matumizi ya Sheng katika makanisa haya ya kisasa, asilimia 40% ya watu wazima ambao huabudu katika aina hizi za makanisa walikuwa na maoni kwamba, viongozi wa makanisa wanastahili kuikubalia Sheng kuanza kutumika katika taratibu za kuendesha ibada za makanisani. Kulingana nao, vijana wanahudhuria ibada za makanisa ya kisasa kwa sababu viongozi wa makanisa haya waikubalia lugha ya Sheng kutumika kwa kiasi fulani katika kufanikisha taratibu kadha za ibada. Asilimia hii ya wazazi ilikiri kwamba vijana wao huongea Sheng na wao hupenda sana kusikiliza nyimbo za injili zilizoimbwa katika Sheng. Vile vile asilimia hii (40%) ya watu wazima ilikiri kwamba wao huwa hawaelewi ujumbe ambao huwa katika nyimbo za injili zilizoimbwa katika Sheng.

4.1.2.3 Maoni ya Vijana Kuhusiana na Matumizi ya Sheng Kanisani

Asilimia 75% ya vijana (ambao ni wafuasi wa makanisa haya) tuliowahoji kuhusiana na matumizi ya Sheng hasa katika uendeshaji wa taratibu na kaida za dini ya kikristo walikuwa na maoni kwamba, ukubalifu wa utumiaji wa lugha ya Sheng katika makanisa haya umewafanya wawe wafuasi wa dhati wa makanisa hayo. Wao huhisi kwamba viongozi wa makanisa hayo, wanautambua umuhimu wao (kama vijana) wa kuwepo makanisani, na hivyo basi kuutambua umuhimu wa lugha yao (Sheng) katika maswala ya kuihubiri injili. Katika muktadha huu, wao wameweza kuihubiri injili kwa misingi ya uelewa wao. Vile vile, wao wamefaulu kuwavutia vijana wengine katika makanisa haya kupitia kwa huduma zao za uimbaji wa nyimbo za kiinjili, kwa kutumia lugha ya Sheng. Walinukuu kifungu cha Biblia cha “*Mark 6: 6-29*”.

Aslimia 20% ya vijana hawa ilikuwa na maoni yaliyokinzana na yale yaliyotolewa na vijana hao wengine. Aslimia hii ya vijana ilikuwa na maoni kwamba, ukubalifu wa utumiaji wa lugha ya Sheng katika taratibu za ibada ni sawa na kuikosea kanisa heshima na hadhi yake. Wao walinuu kifungu cha Biblia cha “*Mathew 21:12-13*”. Ufuatao ni mnara unaofafanua kwa mukhtasari maoni ya waumini wa dini za Kikristo kuhusiana na matumizi ya Sheng katika makanisa ya kisasa.



4.2 Sheng na Injili: Kiwango cha Redioni

Ingawaje Sheng (pamoja na utenda kazi wake) haina jukwaa kubwa la utenda kazi katika kanisa (hasa makanisa ya awali), matumizi ya lugha hii yana jukwaa kubwa kubwa sana la utenda kazi katika chombo cha habari cha redio. Yaani, vijana wazungumza Sheng hupata nafasi ya kujitambulisha na kujianisha na makundi mengine katika jamii kuititia kwa chombo cha habari cha redio. Hii ni kulingana na uchanganuzi wa data yetu.

Je, redio ni nini?

Kamusi ya karne ya 21 (2011:) inatoa fasiri ya neno redio kwa kusema kuwa;

Redio ni chombo kinachopokea mawimbi ya sauti kutoka hewani k.m. utangazaji ili mtu asikie habari, ujumbe au muziki unaochezwa katika kituo hicho cha redio; utaratibu wa utangazaji unaotumia mawimbi ya sauti na kuyarusha hewani.

Kutokana na fasiri hii ya neno redio, tuliweza kubaini kwamba redio ni mojawapo ya vyombo vya habari ambavyo huwezesha na kufanikisha mawasiliano kupitia njia ya mawimbi.

4.2.1 Maoni ya Watu Wazima Kuhusiana na Matumizi ya Sheng Redioni.

Asilimia 54% ya watu wazima tuliohaji ilikiri kwamba wamewahi kuzisikia nyimbo za injili zilizoimbwa katika Sheng zikichezwa kwenye chombo cha habari cha redio. Kulingana nao wanamuziki ambao huimba aina hizi za nyimbo huwa vijana. Vile vile, vijana ndio huwa wafuasi wa nyimbo za aina hiyo ambazo huchezwa kwenye redio. Majina ya wanamuziki ambao wameimba nyimbo za aina hii hawakuyaelewa sana. Kwa jumla majina matatu tu ya wanamuziki ambao wameimba nyimbo za injili katika Sheng ndiyo yaliyojitekeza katika data yetu. Majina haya ni pamoja na;

- a) Jimmy Gait
- b) Daddy Owen
- c) Rough tone

Asilimia hii ya watu wazima ilisema kuwa wao huwa hawazieawi bayana nyimbo za injili ambazo huwa zimeimbwa katika Sheng.

Pia tulipata kubainisha kwamba kati ya vipindi hivi ambavyo huchenza nyimbo za injili katika redio kuna vile ambavyo huzicheza nyimbo za kiinjili (zilizoimbwa katika lugha ya Sheng) na zile za kidunia kwa pamoja au katika kipindi kimoja. Kulihusu jambo hili watu wazima hawa walikuwa na maoni kwamba; jambo hilo la kuzicheza kwa pamoja nyimbo za kidunia na zile za kiinjili halikuwa jambo zuri. Kulingana nao kufanya hivyo kulikuwa sawa na kuikosea injili adabu na hivyo basi kuipunguzia hadhi yake ya utakatifu.

4.2.2 Maoni ya Vijana Kuhusiana na Matumizi ya Sheng Redioni

Asilimia 78% ya vijana tuliohaji walikiri kwamba wao husikiliza nyimbo za injili (zilizoimbwa kwa lugha ya Sheng) kwenye vipindi vya redio. Mifano ya vipindi hivi vya redio walivyotutajia ni pamoja na;

Jina la kipindi

kituo cha redio

- a) Rausha = Citizen Radio
- b) Gospel Sunday = Radio Milele
- c) Goteana. = Ghetto Redio

Uchanganuzi wa data yetu ulitufahamisha kuwa asilimia hii ya vijana inawafahamu na kujitambulisha na wanamuziki wengi ambao wameimba kwa lugha ya Sheng kuliko wale ambao wameimba nyimbo za kinjili katika lugha ya Kiswahili sanifu. Wengi wao walikuwa na uwezo wa kuziimba na hata kuzikariri nyimbo hizo kutoka akilini mwao. Ufuatao ni mfano wa kibwagizo cha wimbo wa kinjili ulioimbwa na Juliani. Kibwagizo hiki kilikuwa mionganoni mwa vibwagizo vingine vilivyojitekeza katika data yetu.


Sheng: “*Siku hizi nadara pejez za Baibo bavololo na inakuanga ivyo oh no. Siku hizi looking at the bible get to be a true disciple kila mtu ana zero decimal point lazima iko.*”

Tafsiri: “*Siku hizi ninasoma kurasa za Biblia, hapo zamani mambo hayakuwa hivyo. Siku hizi nikitazama Biblia napata kuwa mfuasi wa kweli. Kila mtu ametenda dhambi kwa kiwango fulani.*”

Vijana hawa walikuwa na uwezo wa kuziimba nyimbo hizi za Sheng kuliko jinsi walivyokuwa na uwezo wa kuziimba nyimbo za kinjili zilizoimbwa kwa Kiswahili sanifu.

Tulipowauliza vijana hawa maoni yao kuhusu uchezaji wa nyimbo za kidunia na zile za kidini katika kipindi kimoja, asilimia 78% ya vijana ilikuwa na maoni kwamba; si vibaya kufanya vile, kusudi kubwa la vipindi hivyo huwa kuwaburudisha wapenzi wa vipindi hivyo. Vile vile walikuwa na maoni kwamba, lugha ya Sheng – pamoja na utenda kazi wake – imeboresha na kurahihisha maisha hasa kwa kulifunga pengo la utofauti ambao umekuwepo kati ya mambo ya kidini na yale ambayo yanaaminika kuwa ya kidunia, kwa muda mrefu sasa. Kwa kufanya hivi, mambo ya kidunia na yale ya kidini yamefaulishwa kuwekwa pamoja kwenye jukwaa moja la utendakazi. Kifaulishi cha haya ni lugha ya Sheng. Ufuatao ni mchoro ambao unafafanua kwa kina maoni ya Wakristo kuhusiana na matumizi ya Sheng katika kuihubiri injili hasa kupitia kwa chombo cha habari cha redio.

Kauli za matumizi ya Sheng redioni



4.3 Sheng na Injili: Kiwango cha Televisheni.

Data za utafiti wetu vile vile zilitubainishia kwamba Sheng - pamoja na utenda kazi wake - ina ufuasi na jukwaa kubwa sana la utenda kazi katika chombo cha habari cha Televisheni. Je, televisheni ni nini? Televisheni ni neno la kiingereza, “television” lenye maana ya:

Chombo ambacho hunasa picha, sauti na maandishi kutoka kituo kimoja cha mawasiliano na kuziwasilisha kwa mtazamaji katika sehemu nyingine.(kamusi ya karne ya 21)

4.3.1 Maoni ya Watu Wazima Kuhusiana na Matumizi ya Sheng Kwenye Televisheni.

Asilimia 55% ya watu wazima tuliowahoji walikiri kwamba nyimbo za kiinjili zilizoimbwa kwa Sheng huletwa kwenye televisheni. Hata hivyo asilimia hii ya watu wazima huwa haivitazami vipindi hivyo kwani wao huwa wameenda makanisani masaa hayo ya asubuhi. Asilimia hii pia ilikiri kwamba kuna vipindi fulani vya nyimbo kwenye televisheni ambavyo huzicheza nyimbo za kidunia na zile za kiinjili kwa pamoja katika onyesho moja. Kulingana nao, jambo hilo lilikuwa sawa na makufuru mbele za Mungu. Hii ilikuwa mojawapo ya sababu ambazo huwafanya wao wasipende kuvitazama vipindi hivyo. Vile vile asilimia hii ilikiri kwamba huwa hawazielewi bayana nyimbo hizo za Sheng ambazo hudaiwa kuwa za Mungu. Hii inatokana na

sababu kwamba, leksimu ambazo vijana hao huzitumia katika nyimbo hizo huwa leksimu ambazo zina maana yasiyoeleweka bayana na watu wazima hawa.

4.3.2 Maoni ya Vijana Kuhusiana na Matumizi ya Sheng Kwenye Televisheni.

Utafiti wetu katika kiwango hiki cha televisheni pia ulitubainishia kwamba asilimia 65% ya vijana huvitazama vipindi vya nyimbo za “kiinjili” zilizoimbwa katika lugha ya Sheng kwenye televisheni. Wao wanavijua na kuvifahamu vipindi hivi vyema zaidi kuliko jinsi wanavyovifahamu vile vipindi ambavyo huzicheza nyimbo za kiinjili zilizoimbwa katika Kiswahili sanifu. Mifano ya vipindi walivyotutajia na ambavyo huletwa kwenye televisheni ni pamoja na;

Chombo cha televisheni	jina la kipindi
a) KTN	TUKUZA
b) CITIZEN	RAUKA
c) NTV	Crossover
d) CITIZEN	KUBAMBA

Asilimia kubwa ya nyimbo za kiinjili ambazo huchezwa katika chombo hiki cha habari huwa nyimbo za kiinjili zilizoimbwa katika lugha ya Sheng. Tulipowahoji vijana hawa kama kweli wanawaelewa wasanii ambao huziimba nyimbo hizo kwa majina yao, jibu lao lilikuwa “ndiyo.” Mifano ya wasanii tuliotajiwa ni pamoja na:

Jina la msanii	Jina la wimbo
a) Juliani =	Barua ya ocampo
b) Juliani =	Exportial portantial
c) Verbal =	Love cam mi way
d) M.O.G =	Confusion
e) Jimmy Gait =	Furi furi
f) Dady Owen =	Tobina
g) Eco Dydda =	Ghettto

Kulingana na utafiti wetu, jambo hili kwetu llikuwa na maana kwamba vijana wameanza kuasi kuhudhuria ibada za makanisani na sasa wameanza kuhudhuria ibada zinazofanyika kwenye televisheni. Sababu inayochangia vijana hawa kukimbilia ibada zinazofanyika kwenye televisheni ni kwamba ibada hizo hufanyika hasa katika lugha ya Sheng. Hii ndiyo lugha ambayo vijana hujitambulisha nayo katika jamii. Wenyе kuziimba hizi nyimbo na wenyе kuziendesha hizo ibada huwa vijana kama wao. Hii ndiyo sababu vijana wameanza kuhudhuria ibada zinazofanyika kwenye televisheni kuliko zile zinazofanyika kwenye makanisa.

Jambo bayana tulilotambua kutokana na wanamuziki hawa (wa nyimbo za injili za mtindo wa Sheng) ni kwamba, karibu wote huwa na majina ya kimajazi. Wafuasi wao vile vile wanawajua kwa majina hayo. Wengi wao hawawajui kwa majina yao halisi. Jambo hili tulilichukulia kama njia nyingine ya ufichaji wa siri mionganoni mwa vijana. Jambo lingine ni kwamba vitambulishi vya majina ya nyimbo hizo zao za “kiinjili” havina sajili yoyote ya kidini kama vile Mungu, Roho Mtakatifu, kanisa, dhambi, Yesu, Shetani, mbinguni na Jerusalem. Ni nyimbo zenye vichwa vya majina ya kawaida ambayo ni ya kidunia tu! Hivi sivyo ilivyo na nyimbo za kiinjili zilizoimbwa na wasanii kama vile, Rose Muhando, Munishi, Kiande, Mary Wambui na kadhalika. Utafiti wetu ulibaini kwamba wasanii hawa huitwa na hujulikana kwa majina yao halisi wala sio kwa lakabu zao. Majina ya nyimbo zao huwa yamekita katika sajili ya dini ya kikristo. Tazama mfano huu kama ulivyojitokeza katika data yetu;

Jina la mwimbaji

- a) Rose Muhando
- b) Munishi
- c) Kiande ask
- d) Christine Shusho

Jina la wimbo

- Mungu alinena naye Musa
- Yesu ndiye njia
- Wana wa Israeli
- Wa kuabudiwa

Tulipowauliza vijana, kati ya aina hizo mbili zanyimbo,(zile zilizoimbw katika Sheng na zile zilizoimbwa katika Kiswahili sanifu) ni zipi walizozipenda sana kila zinapoletwa kwenye televisheni, jibu la asilimia hii (65%) ya vijana hao lilikuwa na maoni kwamba wanazipenda nyimbo hizo za kiinjili zilizoimbwa katika Kiswahili sanifu – au rejista ya kidini - lakini

wanazienzi zile zilizoimbwa katika lugha ya Sheng. Sababu kuu waliyotoa ni kwamba Sheng ni lugha ambayo wanajitambulisha na kujiainisha kwayo kinyume na lugha ya dini ambayo mara nyingi hutumiwa kwa kuwasuta wao pamoja na matendo yao yanayoaminika kuwa maovu au chukizo mbele za jamii.

Vile vile tulibaini kwamba kunavyo vipindi kadhaa visivyokuwa vya kiinjili ambavyo huzicheza kwa pamoja nyimbo za kidunia na zile za kiinjili - hasa zile zilizoimbwa kwa lugha ya Sheng. Maoni ya vijana hawa kulihusu jambo hili yalikuwa kwamba: -

“Hakuna ubaya! Nyimbo zote ni nyimbo tu! Hakuna wimbo wa Mungu na wimbo wa Shetani. Nyimbo zote ni za Mungu”.

Wazo hili la vijana hawa tuliweza kulibaini kutokana na kuwapo kwa wasanii kadhaa ambaa huimba nyimbo za kidunia katika msimu mmoja kisha wakaimba nyimbo za kiinjili katika msimu mwengine. Mifano ya majina ya wasanii tuliopewa na ambaa huwa na sifa za uimbaji wa aina hii ni pamoja na;

- a) Size Eight
- b) Jimmy Gait
- c) Juliani
- d) Octopizzo
- e) Daddy Owen


Ukweli wa madai haya ulijidhihirisha katika mifano ya vibwagizo hivi tulivvoorodhesewa katika data yetu. (Mfano huu ni wa kibwagizo cha wimbo ulioimbwa na Octopizzo)

Sheng: *Saja tunajipa lembe zako ka masafara, maganja user na madre zote kama utatuokolea ili tuchore hizi sins.*

Tafsiri: *Mungu tunakuja mbele zako kama maskini wavutaji bangi na dawa zote kama utatuokoa ili tuache hizi dhambi.*

Kwa kiwango kikubwa wimbo huu huchukuliwa kuwa wa “kiinjili”. Lakini upo wimbo mwingine wa kidunia tuliopewa ambao umeimbwa na mwanamuziki yuyu huyu. Jina la wimbo huu ni “ivo, ivo ivo”, likiwa na maana ya neno la Kiingereza “evil, evil, evil” wala sio kwa maana ya neno la Kiswahili lenye maana ya, “hivyo hivyo hivyo” jinsi inavyodhaniwa na watu wengi. Katika wimbo huu, (wa ivo, ivo, ivo) mwanamuziki huyu anajitambulisha kama rafiki wa “lucifer” yani shetani. Hivyo basi mwanamuziki huyu alijibainisha kama mwanamuziki ambaye huziimba nyimbo za Mungu katika msimu mmoja na akaziimba nyimbo za kidunia katika msimu mwingine. Labda hii ndiyo sababu ya watu wengi wazima tuliowahoji, kuhusiana na jambo hili (la mwanamuziki mmoja kuimba nyimbo za kiinjili na kidunia kwa pamoja), kuihusisha lugha ya Sheng- pamoja na wanamuziki ambao huimba katika lugha hii- na ushetani au uozo katika jamii ya dini ya kikristo.

Asilimia 35% ya vijana tuliowahoji ilikiri kwamba vipindi vyta nyimbo za kiinjili hule twa kwenye televisheni. Hata hivyo wao huwa hawavitazami vipindi hivyo kwa sababu wao aidha huandamana na wazazi wao kuenda makanisani au huenda huko makanisani peke yao. Ufuatao ni mnara ambao unafafanua kwa kina maoni ya Wakristo kuhusiana na matumizi ya Sheng katika kuihubiri injili hasa kupitia kwa chombo cha habari cha televisheni.



4.4 Sheng na Injili: kiwango cha vijisahani vyta Santuri (CD ROM)

Santuri ni kifaa chembamba chenye umbo la mviringo. (*Oxford Advanced Learners* 2010 8th edition). Kifaa hiki cha kisayansi huwa na uwezo wa kuhifadhi habari au data msingi kwa matumizi ya baadaye. Jinsi kifaa hiki kilivyo na umuhimu kwa wanataalamu wengi ndivyo kilivyo na umuhimu kwa wasanii wa taaluma mbali mbali. Miongoni mwa wasanii hawa ni pamoja na wanamuziki wa nyimbo za kiinjili za dini ya kikristo. Ingawaje nyimbo za kidunia na zile za kiinjili zina uwezo wa kuhifadhiwa kwenye kifaa hiki, ni vyema ielevweke kwamba hapo awali, ulikuwepo mpaka uliyozitenga nyimbo za kiinjili na zile za kidunia. Nyimbo za kidunia na zile za kiinjili zilihifadhiwa kwenye sahani tofauti za santuri, wala hazikuchanganywa kwa pamoja. Haya tuliyabaini kutokana na uchanganuzi wa data yetu.

Vile vile, utafiti wetu ulitubainishia kwamba wapo wacheza santuri amba wazichanganya aina hizi mbili za nyimbo kwenye sahani moja ya santuri- labda kwa minajili ya biashara-. Katika utafiti wetu, tulitaka kubaini maoni ya wafuasi wa dini ya Kikristo kulihusu jambo hili linalotendeka leo hii katika jamii. Wale amba wazichanganya aina hii huuzwa hasa na vijana katika maeneo mbalimbali ya Umoja. Maeneo haya ni pamoja na vilabuni, masokoni, kwenye magari ya usafiri na hata barabarani. Vile vile sahani hizi huchewa kwenye maneo yafuatayo;

- a) Kwenye magari ya usafiri
- b) Kwenye vilabu vya pombe
- c) Kwenye makongamano
- d) Kwenye sherehe kama vile za harusi
- e) Majumbani.

Kuzihusu nyimbo hizi, wao walikuwa na maoni kwamba sahani za aina hiyo zilikosa kuhifadhi maadili mema ya dini ya kikristo. Ufuatao ni mfano wa maoni yanayowiana ambayo yalitolewa na watu hawa wazima;

“Mimi sizipendi sahani za aina hiyo. Ni za kupotosha na hazina heshima kwa Mungu wala kwa dini ya kikristo.”

Kulingana na watu wazima hawa, sahani za santuri zenye sifa hii zinastahili kupigwa marufuku kwa sababu zikiendelea kuwepo katika jamii basi kwa miaka ijayo, sahani za aina hii zitakuwa zimewachanganya na kuwakanganya watu wazima pamoja na vijana hivi kwamba hawatajua tofauti iliyopo kati ya nyimbo za kiinjili na zile za kidunia au kati ya mafunzo ya kikristo na yale yasiyokuwa ya kikristo.

4.4.2 Maoni ya Vijana Kuhusiana na Matumizi ya Vijisahani Mseto vya Santuri


Asilimia 80% ya vijana tulio wahoji kuhusiana na swala hili walikuwa na maoni kwamba sahani za santuri zenye sifa ya kuzichanganya nyimbo za kidini na zile za kidunia zipo. Asilimia hii ya vijana ilizipenda na kuzienzi sahani za santuri zenye sifa hii ya kuzichanganya nyimbo za kiinjili na zile za kidunia kwa pamoja. Wao huwa hawaoni ubaya wowote kuhusiana na jambo hilo. Sababu yao kubwa ya kuzisikiliza nyimbo hizo huwa kupata burudani tu. Kwao nyimbo zote ambazo hupatikana kwenye sahani za aina hiyo huwapa burudani tosha. Tulipowahoji kuhusu maeneo ambayo wao hupata kuzisikiliza sahani za santuri za aina hii walitutajia maeneo kama vile: nyumbani, vilabuni, makongamanoni, na kwenye magari ya usafiri. Asilimia iliyosalia ya vijana hawa ilikuwa na maoni kwamba wao huwa hawazipendi sahani za santuri ambazo huwa zimezichanganya nyimbo za injili na zile za kidunia kwa pamoja. Hisia hizo zao huwa zimechangiwa na maoni ya wazazi wao kuhusiana na sahani zenye sifa hizo. Wazazi wao huwa hawazipendi sahani za santuri (CD ROM) zenye sifa hiyo. Wao hupenda kununua sahani za santuri zilizo na nyimbo za injili kando, na zile zilizo na nyimbo za kidunia kando. Asilimia hii ya vijana ilikuwa na maoni haya yafuatayo yaliyowiana;

- a) “Nyimbo zingine katika sahani hizo hudaiwa kuwa za kiinjili lakini kwa kawaida huwa sio za kiinjili. Sababu ni kwamba, nyimbo hizo huwa hazitaji mambo ya kibiblia yanayochukuliwa kuwa matakatifu kama vile Mungu, Yesu, mbinguni na kadhalika. Huwa

zinataja tu mambo ya kijumla ambayo yaweza yakawa au yasiwe katika sajili ya dini ya kikristo,” w alisema.

b) “Mimi sizipendi hizo sahani ambazo huzichanganya nyimbo za kidunia na zile za kiinjili kwa pamoja. Hata huwa ninaona aibu nikizicheza sahani kama hizo mbele ya wazazi wangu. Wasanii wengine katika sahani hizo huwa na maongezi mabaya; mara nyingi wao huyataja mambo yasiyolewaka au yasiyostahili kutajwa mbele za wazazi,” Walisema.

Kulingana na maoni yaliyotolewa na makundi haya mawili (ya vijana na watu wazima) ni bayana kwamba vijana wameanza kuzienzi nyimbo za injili za lugha ya Sheng kuliko zile za injili zilizoimbwa katika Kiswahili sanifu. Hali hii inatokana na sababu kwamba Sheng ni lugha ambayo vijana hawa hujitambulisha kwayo. Kwa hivyo mtu ye yote anayetaka kuwasiliana na vijana, atafaulu pakubwa iwapo atatumia lugha ya Sheng katika juhudhi hizo zake kuliko lugha nyingine. Ni kutokana na sababu hii ambapo vijana ambao ni wanamuziki wa kiinjili hupendelea kuimba kwa lugha ya Sheng ili nyimbo zao zipate kupokelewa vyema na vijana. Ufuatao ni mnara ambao unafafanua kwa kina maoni ya Wakristo kuhusiana na matumizi ya Sheng katika kuihubiri injili hasa kuitopia kwa chombo cha sahani mseto za santuri.



HITIMISHO

Katika sura hii ya nne tumetathmini athari kadha wa kadha za Sheng katika dini ya kikristo. Kigezo tulichojikita kwacho kilikuwa kigezo cha Sanaa ya uimbaji. Hii ilitokana na sababu kwamba utafiti wetu ulitudhihirishia kuwa, kati ya sanaa nyingi ambazo vijana wengi huzitumia katika kujieleza, sanaa ya uimbaji na utangazaji ndiyo sanaa ambayo imetia fora sana miongoni mwao. Vijana wengi wanaitumia sanaa hii sana katika harakati zao za kuihubiri injili. Vile vile tulibaini kwamba matangazo na nyimbo hizo huwa hazieleweki bayana na wengi wa wazazi wa vijana hawa au hata na vijana wengine. Hii inatokana na sababu kwamba maneno ambayo vijana hawa huyatumia katika matangazo na nyimbo hizo huwa ya kiSheng au ya kisiri. Hali hii ndiyo imezua mtafaruku fulani miongoni mwa wafuasi wa dini hii ya kikristo.

Vile vile utafiti wetu ulitubainishia kwamba athari za Sheng hazijidhihirishi mno katika makanisa ya awali kama vile katoliki na Anglikana ila tu, katika makanisa ya kisasa kama vile “The Temple of Christ”, na “The Holy Ghost Fire Ministry.” Katika utafiti huo wetu, tuliweza pia kubaini kwamba nyimbo hizi za kiinjili zilizoimbwa katika mtindo wa Sheng zina nafasi kubwa sana katika vyombo vya habari. Vyombo hivi ni pamoja na: redio, televisheni, na disk (au vijisahani vya santuri). Hapo awali, vyombo vya habari kama vile redio na televisheni vimekuwa vikitumiwa na wakristo katika kuieneza injili ya imani yao ya kikristo. Wao wamekuwa na vipindi maalum katika vyombo hivi vya habari. Vipindi hivyo havikuzicheza wala kuzichanganya nyimbo za kidunia na zile za kiinjili kwa pamoja. Lakini leo hii vingi vya vipindi kama hivi vinazichanganya na kuzicheza nyimbo hizi kwa pamoja. Jambo hili hutekelezwa hasa na watangazaji ambao huviwasilisha vipindi hivyo kwenye vyombo vya habari. Mara nyingi watangazji hawa pia huwa wa jamii ya Sheng. Hali hii imetubainishia kwamba lugha ya Sheng imezua ushawishi na ukinzani mkubwa sana katika dini ya kikristo (hasa kupitia kwa vyombo vya habari) na hivyo basi imeathiri pakubwa mikondo, misingi, imani na kaida za Kikristo.

Vile vile tumbaini kwamba vijana wa mtaa huu wa Umoja hupenda sana kuwasiliana kwa kutumia Sheng. Vijana wa mtaa huu ambao huwasiliana kwa Sheng hujihisi kwamaba wao wana ufahamu mkubwa sana wa jiji, wa kiteknolojia, wa kisayansi na wa maisha kuliko wale ambao huwa hawaijui au hawaizungumzi Sheng. Yaani, vijana ambao huizungumza Sheng hujiona kuwa wastaarabu. Vijana hawa huwaona wale wasioijua au kuizungumza Sheng kama limbukeni au fala. Hivyo basi Sheng huinua na kudumisha hadhi ya vijana katika jamii. Kijana yejote

anapoitwa fala na vijana wengine labda kwa sababu ya kutojua Sheng, jambo hilo humkera sana kijana huyo. Hali hii humsukuma kijana huyo kujifunza Sheng ili siku nyingine asipate kuitwa fala tena. Kwa hivyo vijana katika maeneo haya ya Umoja hujiainisha kama vijana halisi na wanaolielewa jiji kwa misingi ya uwiji wao wa kuizungumza Sheng. Baada ya vijana hawa kujiainisha kama wanajamii wa lugha ya Sheng, sasa wao huweza kujitambulisha kwa makundi mengine yaliyomo katika jamii kama wanajamii wa lugha ya Sheng. Jamii hii ya Sheng hujitambulisha kwa makundi hayo mengine hasa kwa kutumia njia zifuatazo;

- a. Kuwasiliana kwa Sheng na makundi mengine katika jamii ambayo pia huizungumza Sheng.
- b. Kujitenga na kuyadunisha makundi mengine katika jamii ambayo huwa hayazungumzi kwa Sheng.
- c. Kuiga matendo na nyimbo za wasanii ambao huimba nyimbo za Sheng, iwe ni za kiinjili au za kidunia.

Baada ya vijana hawa (wanajamii ya Sheng) kujitambulisha kwa makundi hayo mengine yaliyomo katika jamii, vijana hawa sasa huweza kujilinganisha na makundi hayo. Ujilinganishaji huu hutendeka hasa kupertia kwa mazungumzo na sanaa. Kwa kutumia mazungumzo, vijana hawa wa jamii ya Sheng huweza kuwasiliana na vijana wengine wa jamii ya Sheng bila ya watu au vijana wengine wasioielewa Sheng kuyaelewa mazungumzo yao. Kwa kutumia sanaa ya uimbaji, vijana hawa huweza kujilinganisha na makundi mengine katika jamii ambayo huimba kwa lugha ya Sheng ama kwa kuimba nyimbo katika Sheng au kwa kuwasilisha vipindi vyta Sheng kupertia kwa vyombo vyta habari.

Ifahamike kwamba vijana walio katika jamii ya Sheng hujilinganisha na makundi mengine katika jamii hasa kwa kutumia aina mbili kuu za sanaa. Sanaa hizi ni sanaa ya uimbaji na sanaa ya utangazaji. Katika sanaa ya uimbaji, kuna wanamuziki ambao huimba kwa Kiswahili, Kiingereza au Sheng na katika sanaa ya utangazaji kuna watangazaji ambao hutangaza kwa Kiingereza, Kiswahili na Sheng. Hivyo basi wanajamiilugha ya Sheng hujiainisha, wakajitambulisha na kujilinganisha na makundi haya yaliyomo katika jamii ambayo tumeyataja hapo juu. Makundi haya hasa huwa yale yanayohusishwa na mambo ya dini ya Kikristo katika utenda kazi wayo.

SURA YA TANO

5.0 MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Utangulizi.

Katika sura ya tano, tumeangazia matokeo ya utafiti wetu pamoja na maswala mengine ambayo yalichipuka katika mchakato mzima wa shughuli yetu ya utafiti. Yote haya yalifungamana na malengo ya utafiti wetu ambayo tulitaka kuyafikia mwishoni mwa utafiti wetu. Athari za Sheng katika asasi mbalimbali za kijamii ni nyingi, na zinaendelea kumea na kukita mizizi katika asasi hizi kila kuchao. Ingawaje asasi hizi - ambazo zimeathiriwa na Sheng - ni nyingi, tuliamua kukita katika asasi ya dini hasa dini ya Kikristo. Hivyo, tuliamua kukita katika dini ya kikristo kwa sababu, asilimia 80% ya wakenya ni wa imani ya kikristo. Kwa muda mrefu sasa, jamii hii ya Wakristo imekuwa ikizitenda taratibu za ibada aidha kwa lugha sanifu ya Kiingereza au kwa lugha sanifu za kiasili. Katika mji wa Nairobi, angalau taratibu zote za ibada huendeshwa kwa lugha mbili mahususi. Kingereza sanifu au Kiswahili sanifu. Katika mtaa wa Umoja – pamoja na maeneo jirani -, angalau ibada za makanisani hugawanywa katika vipindi viwili au zaidi. Kati ya vipindi hivi vya kuendesha ibada, kuna vile ambavyo huendeshwa kwa Kingereza au kwa Kiswahili. Vile vile, ibada hizi huhudhuriwa na watu wenye umri tofauti tofauti. Wote hawa huwa wa jinsia zote mbili: jinsia ya kike na ile ya kiume.

La ajabu ni kwamba, imezuka lugha nyingine katika jamii ambayo haileweki bayana hasa na wafuasi wote wa dini ya Kikristo. Lugha hii inajulikana kama Sheng na inaenziwa sana na wanajamii wa umri wa chini au vijana. Lugha hii huwa na lengo moja muhali la utendakazi wake. Lengo hili huwa ni ukichaji wa siri kati ya watu wanaoizungumza. Ni kutokana na sababu hii ambapo lugha hii huaminika kutumiwa pakubwa na makundi yenye sifa mbaya katika jamii

kama vile wezi, walanguzi wa mihadarati, makahaba, waraibu wa dawa za kulevyta, wahuni, utoinga na madereva wa matatus. Ingawaje lugha hii ya Sheng inahusishwa na sifa na makundi mabaya katika jamii ni vyema kuelewa kuwa asilimia kubwa ya makundi hayo tuliyoyataja inamiliikiwa na vijana. Hii ina maana kwamba Sheng ni lugha ya vijana au ni lugha ambayo ina ufuasi na umaarufu mkubwa sana mionganini mwa vijana, hasa vijana wa mjini. Vile vile, ni vyema ielewewe kimbele kwamba vijana hawa – ambao ni wanajamii lugha ya Sheng – ni Wakristo. Hivyo, vijana hawa wameibeba Sheng na wakaingia nayo makanisani. Leo hii wengi wao wanapenda sana kuziendesha taratibu za ibada (kama vile uimbaji) kwa kuitumia Sheng. Jambo hili ndilo ambalo limechangia kuwepo kwa mtafaruku na mgogoro mionganini mwa wanajamii hii ya dini ya kikristo. yaani wafuasi wote wa dini ya Kikristo wana lengo na nia moja ya kuabudu Mungu katika jukwaa moja lakini lugha wanazozitumia ili kuafikia lengo hili aidha hazieleweki bayana na Wakristo wote au hazipendwi kwa dharti na wafuasi wote wa dini hii. Mtafaruku huu ndio ambao umepelekea kuibuka kwa makundi mawili kinzani katika jamii ya Wakristo. Makundi hayo kinzani ni pamoja na kundi linalopenda kuabudu kwa Sheng na kundi linalopenda kuabudu kwa lugha ilijoja sajili ya dini ya Kikristo

Utafiti wetu ulichukulia mwelekeo ambao ungefumbata maswala kadhaa ambayo ni muhimu kwa kutoa taswira bayana ya athari za Sheng katika dini ya Kikristo kwa jumla. Hivyo basi, katika sura ya kwanza tumetanguliza utafiti wetu kwa kuangazia maswala ya kijumla ambayo yangetoa mwongozo wa kuyaafiki malengo ya utafiti wetu.

Katika sura ya pili tumeangazia mbinu mablimbali za kimofologia ambazo Sheng huzitumia katika uundaji wa leksimu zake. Mbinu hizi za uundaji wa maneno huwa mbinu bia na hivyo basi hutumiwa angalau na lugha zote za ulimwengu kwa kuijundia leksimu ili ziweze kujitosheleza kimsamiati. Sheng kama lugha ya vijana haikuwachwa nyuma na utaratibu na mchakato huu wa uundaji wa maneno. Sheng imezitumia mbinu hizi kwa kuijundia leksimu zake. Mifano ya mbinu hizi za uundaji wa maneno tulizobaini ni pamoja na ukopaji na utohozi, uambishaji, uambatishaji, ujenzi ghairi, ubadilishanaji wa silabi, tafsiri mkopo, unyumbuzi, upolisemia, ukatizaji, onomatopia, ubunifu wa leksimu, akronimu, na uhulutishaji. vile vile tulibaini kwamba ingawaje Sheng huijundia leksimu kwa kutumia mbinu hizi za kimofolojia, karibu maneno yote ya Sheng hutokana na ukopaji na utohozi. Yaani, leksimu nyingi za Sheng huwa zimeombwa au kukopwa kutoka lugha zingine hususan lugha ya kingereza, Kiswahili na

kikuyu. Leksimu asilia ambazo huwa za lugha ya Sheng huwa zile zinazotokana na ubunifu na mifano kadhaa ya onomatopia. Ni kutokana na uwezo huu wa kujiundia leksimu ambapo lugha hii ya Sheng huwa na uwezo wa kufanikisha mawasiliano mionganii mwa wanajamii lugha wake. Jamii lugha hii hujumuisha vijana waliosoma na wasiosoma, matajiri na maskini. Ni kutokana na sababu hizi ambapo Sheng huwa na leksimu za taaluma mbalimbali kama vile za kiufundi, kiteknolojia, kisayansi na hata kielemu. Vile vile jambo hili huchangia kuwepo kwa leksimu za Kiingereza, Kiswahili na lugha zingine za kienyeji katika Sheng.

Katika sura ya tatu, tumetalii jinsii ambavyo Sheng hutumia maneno mbalimbali iliyojiundia kwa kujiundia vifahiwa kadhaa. Vifahiwa hivi hutumiwa na wanajamii lugha hii kwa kujiundia sentenzi za viwango mablimbali vya kisintaksia na kisemantik. katika utafiti wetu ni pamoja na Haponimu, Sinonimu, Haponimu, Polisemia na Antonimia. Vifahiwa hivi tumevijadili kwa kina ili kuziweka bayana sifa zake pamoja na utenda kazi wake. Kila aina ya kifahiwa cha Sheng tumeambatisha na mifano kadha ya sentensi za Sheng. Pamoja na tafsiri kamili ya sentensi hizo. Tafsirizingine tumezisawiri katika Kiswahili sanifu.wanjamailugha hii ya Sheng huvitumia vifahiwa hivi pamoja na sentenzi hizo za Sheng katika kufanikisha mawasiliano mionganii mwao. Hivyo, wanajamii lugha hii huweza kujianisha, wakajitambulisha na kisha wakajilinganisha na makundi mengine katika jamii kwa kutumia lugha hii yao. Vile vile wao huitumia lugha hii katika kujieleza, na kuwasilisha maoni na mitazamo yao ya kijamii hasa kwa kutumia sanaa ya nyimbo na uimbaji.

Katika sura ya nne tumeangazia athari za Sheng zinazotokana na sanaa ya nyimbo na uimbaji. Nyimbo ambazo tumeangazia ni nyimbo za kidini zilizoimbwa katika Sheng. Hii ilitokana na sababu kwamba utafiti wetu ulikita katika kutathmini athari za Sheng katika dini ya Kikristo. Hivyo tumepata kubaini kwamba Sheng ina athari zake katika taasisi mbalimbali za kijamii na za kidini. Mifano ya taasisi na asasi hizi ni pamoja na makanisa ya awali na ya kisasa nchini Kenya, vyombo vya habari, taasisi za elimu, afya, sayansi na teknolojia. Mifano ya makanisa ya awali tuliyochanganua ni pamoja na kanisa la Katoliki, kanisa la S.D.A, kanisa la Anglikana, kanisa la P.C.E.A, na kanisa la A.C.K. Mifano ya makanisa ya kisasa ambayo tumeangazia ni pamoja na The “Holy Ghost Fire Ministry”, “Jesus is Alive Ministry”, “God’s Favour Ministry,” “The Harvest Center.”

Kati ya aina hizi mbili za makanisa, tumepata kubaini kwamba makanisa ya kisasa ndiyo ambayo yamekubalia matumizi ya Sheng kwa kiwango kikubwa katika kufanikisha taratibu za ibada. Athari za Sheng katika makanisa ya awali bado hazijaanza kuchipuza ingawaje dalili zipo. Asasi nyingine ya kijamii ambayo tuliweza kubaini kwamba athari za Sheng hujithirihisha kwayo ni asasi ya habari na mawasiliano. Katika asasi hii tuliweza kuangazia vyombo vyahabari kama vile redio, televisheni na sahani za santuri (CD ROM)

Matokeo ya utafiti wetu yamelingana na nadharia tete ambazo zilituongoza katika mchakato mzima wa utafiti wetu. Katika madhumuni ya utafiti wetu, tulilenga kubaini kama Sheng imezua leksimu ambazo henzieleweki na wanajamii wote wa dini ya Kikristo. Utafiti wetu ulibainisha kwamba Sheng imezua misamiati mingi sana ambayo haieleweki bayana na wafuasi wote wa dini ya Kikristo. Ingawaje vijana wengi wanaenzi kuhubiri injili ya dini ya kikristo kwa kutumia Sheng, ujumbe ambao huwa katika nyimbo hizo huwa haueleweki na wafuasi wote wa dini hii. Hivyo, wale wasioielelewa Sheng huwa wanafungiwa nje ya mahubiri hayo ya kiSheng. Hali hii hutokana na sababu kwamba jamii hii ya Sheng hutumia leksimu zisizoeleka bayana na watu wazima katika nyimbo hizo zao za kiinjili. Hivyo basi matumizi ya Sheng katika mahubiri ya Kikristo huzua upungufu Fulani katika malengo na makusudio ya dini ya Kikristo. Vile vile hadhi ya dini hii katika jamii huweza kuathiriwa kwa njia moja au nyingine.

Madhumuni ya pili ya utafiti wetu yalikuwa kubaini kama kweli matumizi ya Sheng katia dini ya Kikristo yanzeza athari hasi na chanya katika asasi hii. Utafiti wetu ulibainisha kwamba Sheng imesababisha athari hasi na chanya katika dini hii ya Kikristo. Athari chanya za Sheng zimejidhihirisha katika makanisa ya kisasa. Makanisa haya ya kisasa huwakubalia vijana (ambao ndio hupenda kutumia Sheng pakubwa) Kuitumia Sheng katika taratibu mbalimbali za kuendesha ibada. Matokeo yake yamekuwa kwamba makanisa haya yameishia kuwa na wafuasi wengi vijana ambao wamezihudhuria ibada zao. Kwa njia moja au nyingine wazazi wengi wa vijana hawa walikuwa washiriki wa makanisa ya awali kama vile katoliki. Anglikana, PCEA , SDA, The Quakers na ACK . lakini wengi wa vijana hawa wameasi ushirika wa makanisa hayo ya wazazi wao na wakajiunga na makanisa haya ya kisasa. Mojawapo ya sababu ambazo zimechangia vijana hawa kuyagura makanisa haya ya awali na kujiunga na makanisa haya ya kisasa ni ukubalifu wa matumizi ya Sheng katika makanisa haya ya kisasa. Yaani makani sa ya kisasa yamekubalia matumizi ya Sheng katika taratibu za ibada zao kinyume na ilivyo katika

makanisa ya awali au zamani. Athari hizi pia zinashuhudiwa katika asasi ya habari na mawasiliano. Yaani Sheng na utenda kazi wake ina ufuasi mkubwa sana katika jukwaa la vyombo vya habari. Vyombo hivi vya habari ni pamoja na redio, televisheni, matandao na sahani za santuri. Hapo awali (kabla ya matumizi ya Sheng kukita miziz katika jamii na asasi zake) wafuasi wa dini ya Kikristo walikuwa na vipindi vyao mahususi katika vyombo vya habari ambavyo walivitumia hasa kwa kuhubiri injili. Lugha iliyotumiwa katika vipindi hivi ilikuwa lugha ilijoja sajili za dini ya Kikristo. Lugha hii ilieleweka na ikaheshimika bayana na wafuasi wote wa dini hii.

Lakini leo hii, wafuasi wa dini hii ya Kikristo ambao ni wanajamii lugha ya Sheng, pia wana vipindi vyao vya kidini katika vyombo hivi vya habari. Katika vipindi hivi, jamii hii ya Sheng huwa na wawakilishi wao ambao pia huizungumza Sheng. Maongezi na nyimbo ambazo huimbwa katika vipindi hivyo hufanyika katika Sheng. Hivyo basi vijana wengi ambao hujainisha kama wanajamii lugha hii ya Sheng hujilinganisha na kujitambulisha na vipindi hivi ambavyo huletwa kwenye vyombo hivi vya habari. Michango yao katika vipindi hivi pia hushuhudiwa pakubwa.

Madhumuni ya tatu ya utafiti wetu yalikuwa kubaini kama kweli matumizi ya Sheng katika dini ya Kikristo yangesababisha mgogoro baina ya wapenda Sheng na wasiopenda Sheng na hivyo basi kuzua makundi mawili kinzani katika dini ya kikristo. Matokeo ya utafiti wetu yametubaishia kwamba Sheng imezua mgogoro katika asasi hii muhimu ya dini ya Kikristo. Kwa sasa mgogoro huu upo na unaendelea kushuhudiwa kati ya wanajamii wa lugha ya Sheng na wanajamii wa lugha ya dini ya kikristo. Mgogoro huu ndio ambao umepelekea kuzuka kwa makundi mawili kinzani katika asasi hii ya dini. Kwa upande mmoja, kuna kundi ambalo linaenzi matumizi ya Sheng katika kufanikisha taratibu za ibada za dini ya Kikristo. Kundi hili huitumia Sheng kwa sababu Sheng ni lugha yao na ndicho kitambulisho chao kama vijana. Kwa upande mwingine kuna kundi ambalo linapenda kuziendesha taratibu za ibada kwa kutumia lugha ya dini ya Kikristo iwe makanisani au kwenye vyombo vya habari. Mgogoro huu vile vile umesababisha dini ya Kikristo kupoteza hadhi, malengo na makusudio yake kwa wanajamii wake.

Madhumuni yetu ya nne yalihusu kutathmini kama matumizi ya Sheng katika dini ya kikristo yangelifilisha hadhi, malengo na makusudio ya dini ya kikristo na hivyo basi kuioanisha dini na taratibu za kidunia. Matokea ya utafiti wetu yametubainishia kwamba hadhi, malengo na makusudio ya dini ya kikristo yemeathiriwa pakubwa na matumizi ya Sheng katika taratibu za dini ya kikristo.

Nguzo na misingi ya dini ya kikristo ambayo hapo awali imekuwa ikiheshimiwa, kutiwa na kuzingatiwa sana, leo hii imelegezwa pakubwa. Kifaa ambacho kimetumiwakatika kulegeza nguzo na misingi hii ni Sheng. Nguzo na misingi ya dini ya kikristo hufafanuliwa na kuelezwu kupitia kwa rejista ya dini hii. Rejista hii hubeba maneno ya kale na yaliyo na makali ya kukosoa, kukemea, kuelekeza, kuahidi, kutahadharisha na kufundisha. Rejista hii ya dini ya kikristo ndiyo ambayo imevamiwa na Sheng. Wanajamii lugha hii ya Sheng wamepenyeza misamiati yao katika rejista hii. Misamiati hii ndiyo ambayo inatumika kwa kupunguza makali ya rejista ya dini ya Kikristo na hivyo basi kuifanya rejista hii kuwa kubalifu hasa kwa jamii ya Kikristo na ile isiyokuwa ya kikristo. Ni kutokana na sababu hii ambapo leo hutastaajabu ukisikia nyimbo za kinjili za Sheng zikichezwa kwenye mabaa na kumbi mbalimbali za burudani au kuwasikia wanamuziki wa nyimbo hizi za kiinjili wakialikwa kuimba katika maeneo kama haya. Vile vile, leo hii nyimbo za kiinjili huchanganywa na zile za kidunia kwenye sahani moja za santuri (CD ROM). Mitindo ya kuzicheza nyimbo hizi huwa sawa. Jambo hili lenye uajabu fulani pia hushughudiwa kwenye vyombo vya habari. Katika vyombo hivi, kuna vipindi ambavyo hucheza nyimbo za kidunia na zile za kiinjili (hasa zilizoimbwa katika Sheng) kwa pamoja. Jambo jingine ni kwamba, wasanii wengi wa sanaa hii ya uimbaji huweza kuimba nyimbo zote za kiinjili na za kidunia kwa pamoja. Kwa wasanii kama hawa, kwao wimbo ni wimbo tu na hakuna wimbo wa Mungu wala wa Shetani. Kulingana nao, nyimbo zote ni za Mungu.

5.1 Mambo Ibuka.

Kando na madhumuni na haipothesia ambazo zilituongoza katika utafiti wetu, kuna jambo moja ibuka ambalo lilijitokeza katika utafiti wetu. Jambo lenyewe ni kwamba vijana kadhaa katika sehemu hii ya Umoja pamoja na maeneo jirani, wameanza kuijainisha kama wanajamii lugha ya Sheng kwa kuijundia makundi ya kihalifu. Mojawapo ya makundi tuliyotajiwa katika utafiti wetu ni pamoja na kundi linalojulikana kama “gaza.” Kundi hili ni la wanajamii lugha ya Sheng

na uongozi wake vilevile unamilikiwa na vijana. Kundi hili huwa na lengo kuu moja tu ambalo ni kuwafundisha watoto kutowatii wazazi wao. Vijana wengi hasa wale wa shule za msingi na upili tayari wameanza kujitambulisha kwa kundi hili na hivyo basi kupitia kwalo wakawenza kujilinganisha na makundi mengine katika jamii. Vijana hawa wadogo, pia hufundishwa kuwa wanyang'anyi. Wao hasa huwanyang'anya watoto wa masrika yao bidhaa kama vile vitabu vyta shule, simu, saa na hata mavazi. Bidhaa hizo huwasilishwa kwa viongozi wa genge hili. Viongozi hawa baadaye huviuza bidhaa hizo kisha huwagawia wafuasi wote wa kikundi hiki pesa ambazo hupatikana kutokana na mauzo hayo kwa asilimia fulani. Kikundi hiki tayari kina mizizi yake katika mtaa huu wa Umoja pamoja na maeneo jirani kama vile Buruburu, Kaloleni, Bahati, Majengo, Kayole, Donholm, na Jericho

5.2 Mapendekezo ya Utafiti

Utafiti wetu ulilenga kutathmini athari za Sheng katika dini ya Kikristo: Mtaa wa Umoja. Hivyo basi tumeweza kubaini kwamba Sheng ina athari hasi na chanya katika dini hii hasa mtaani Umoja. Athari hizi za Sheng kama zinavyojidhihirisha katika mtaa huu wa Umoja huenda zikawa tofauti Katika mitaa mingine iliyoko Magharibi, Kusini, na Kaskazini mwa jiji la Nairobi. Vile vile utafiti wetu ulikita katika asasi ya dini ya Kikristo. Zipo asasi nyinginezo katika jamii ambazo utafiti huu haukuangazia. Mifano ya asazi hizi ni pamoja na asasi ya elimu, asasi ya afya, asasi ya sayansi na teknologia, asasi ya utamaduni na asasi ya Usalama wa taifa. Kwa jumla haya ndio maeneo ambayo kwa hakika tunapendekeza kuwa watafiti wa baadaye wapate kuyaangazia kwa kina katika tafiti zao. Hii ni kwa sababu, hatuna budi kudai kwamba athari za Sheng huenda zikajidhihirisha katika asasi hizi muhimu za taifa. Tusichokijua kwa sasa ni kina na kiwango cha athari hizi katika asasi hizo na katika jamii nzima kwa jumla.

HOJAJI

Mimi ni mwanafunzi wa somo la isimu ya Kiswahili (uzamili) katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Nafanya utafiti juu ya Sheng. Naomba uchukue muda wako kunijazia hojaji hii. Toa habari za kweli bila uwoga wowote na usiandike jina lako popote pale. Habari zote zitashughulikiwa kama siri.

Sehemu A (tia alama kwa jibu lako)

1. Umri wako unapatikana katika kategoria gani?

- a) 14-20
- b) 21-25
- c) 26-35
- d) 36-45
- e) 46- na zaidi

2. Jinsia

- a) Uume
- b) Uuke

3. Kiwango chako cha elimu kiko katika kategoria ipi?

- a) Elimu ya shule ya msingi
- b) Elimu ya shule ya upili

- c) Elimu ya chuo cha anuai
- d) Elimu ya chuo kikuu
- e) Nyingineyo bainishi...

4. Kazi yako?

- a) Mwanafunzi
- b) Umeajiriwa
- c) Umestaafu
- d) Mfanyi biashara
- e) Mwalimu
- f) Mwandishi wa habari
- g) Nyingine bainisha

5. Je uwezo wako wa kuzungumza Sheng ni wa kiwango gani?

- a) Mzuri sana
- b) Mzuri
- c) Kiasi
- d) Mbaya

Sehemu B

(Toa jibu lako kwa kutia alama aub kwa ufupi iwezekanavyo).

1. a) Je, Sheng ina misamiati kutoka kwa lugha zingine kama vile Kikuyu, Kiingereza, kifaransa, Kiswahili na kadhalika?

i. Ndio

ii. La

- b) Kama jibu lako ni ndio, taja mifano ya misamiati hii pamoja na maana zake katika Kiswahili

Neno

Maana

- | | | |
|------|-------|-------|
| i. | ----- | ----- |
| ii. | ----- | ----- |
| iii. | ----- | ----- |
| iv. | ----- | ----- |
| v. | ----- | ----- |
| vi. | ----- | ----- |

vii. ----- -----

2. (a) Je, Sheng huyapatia maneno ya Kiswahili maaana mpya kando na maana ya kawaida ya maneno hayo?

- i. Ndio
- ii.
- iii.
- iv. La

(b) kama jibu lako ni ndio taja mifano ya maneno hayo pamoja na maana yake mpya ya kiSheng.

Neno **maana**

- i. ----- -----
- ii. ----- -----
- iii. ----- -----
- iv. ----- -----

3. a) Je, Sheng hujiundia lekisimu kwa kubuni misamiati?

Ndio

La

b) Kama jibu lako ni ndio taja mifano kadhaa

Neno **maana**

- i. ----- -----
- ii. ----- -----
- iii. ----- -----

iv. -----
v. -----

4. a) Je, lugha ya Sheng hujiundia maneno ya kidini kando na maneno tuliyoyazoea?

Ndio

La

b) **Iwapo jibu lako ni ndio taja mifano kadhaa ya maneno haya.**

Neno maana

i. -----
ii. -----
iii. -----
iv. -----
v. -----

5. a) vijana katika jamii ya Sheng huwasiliana kwa maongezi. Hebu tunga sentensi mbili za Sheng katika muktadha wa dini au katika muktadha wa maongezi ya kawaida.

i. -----
ii. -----

6. Taja angalau majina kadhaa yanayomrejelea Mungu au Shetani katika lugha ya Sheng.

Mungu Shetani

a)------
b)------
c)------

7 kwa jumla taja mifano kadhaa ya leksimu za Sheng

Sheng	maana
a) -----	-----
b) -----	-----
c) -----	-----
d) -----	-----
e) -----	-----

Sehemu C

(Tao jibu lako kwa ufupi iwezekanavyo)

1. Taja mifano kadhaa ya wanamuziki wa kiinjili ambao wameimba katika Sheng.
a) -----
b) -----
c) -----
d) -----
2. Hebu andika kibwagizo angalau kimoja kinachotokana na nyimbo za waimbaji hawa.

Sheng

Tafsiri

a) Je wewe kama Mkristo huuelewa ujumbe ambao hupatikana katika nyimbo hizi.

Ndio

La

b) Toa sababu kwa jibu lako.

3. Kati ya nyimbo za kiinjili zilizoimbwa kwa Sheng na zile zilizoimbwa katika Kiswahili sanifu ni zipi ambazo hukuvutia sana?

b) Toa sababu kwa jibu lako.

Sehemu D

(Toa jibu lako kwa jibu na kwa ufasaha zaidi)

1. Una maoni gani kuhusu uimbaji wa nyimbo za kiinjili katika lugha ya Sheng kanisani mwenu?

2. Wapo waimbaji ambao huimba nyimbo za kidunia na za kiinjili kwa pamoja katika lugha ya Sheng. Je, una maoni gani kulihusu jambo hili?

3. a) Taja mifano ya vipindi vya kiinjili katika lugha ya Sheng ambyo huletwa kwenye vyombo vya habari.

Televisheni wakati redio wakati mtandaoni wakati

b) Taja mifano ya vipindi vya kiinjili kwa lugha ya Kiswahili sanifu ambavyo huletwa kwenye vyombo vya habari.

Televisheni wakati redio wakati mtandaoni wakati

c) kati ya vipindi hivi (vya Sheng na vya Kiswahili) ni vipindi vipi ambavyo huwa na sifa za kuzicheza nyimbo za kidunia na zile za kiinjili kwa pamoja?

4. a) Una maoni gani kuhusiana na swala la uchanganyaji na uchezaji wa Nyimbo za kiinjili na zile za kidunia kwa pamoja?

b) Toa mfano wa nyimbo ambazo hudaiwa kuwa za kiinjili lakini sio za kiinjili?

Marejleo

Abdulaziz, M. na K. Osinde, (1997), *Sheng and English in Nairobi: Development of Mixed Codes Among the Urban Youth in Kenya*. International Journal of the sociology of Language 125:43-63

Bosire, M. (2008), *Sheng. The Phonological, Morphological and Social Profile of an Urban Vernacular*. Tasnifu ya uzamifu ambayo haijachapishwa: University of Albany. State University of New York.

Githinji, P. (2008), *Language Attitudes: Nairobi People and Sheng*. Tasnifu ya Uzamili ambayo bado haijachapishwa, Michigan State University.

Hartmann R.K. na F.C. Stork, (1972), *Dictionary of Language and Linguistics*. London: Applied Science Publishers Ltd.

Hudson, R.A. (1996), *Sociolinguistics*. (2nd Edition) Combridge, C.U.P.

Iribi Mwangi, P.I. & A. Mukhwana, (2011), *Isimujamii*. Nairobi. Focus Publishers Ltd.

Karanja, M.N. (1993), *Miaka 50 Katika Jela*. Nairobi: Heineman Kenya.

Katie, W. (2001), *A Dictionary of Stylistics*. Longman: Halow.

Kembo-Sure, (1992), “*The Coming of Sheng*,” *English Today* 26-28

King’ei, G. K.(2001), Language and Identity. The challenge of Sheng in kenya. Paper presented at the Association of Third World Studies Conference, September 17-19,2001, Njoro, Egerton University: Kenya.

Makokha, W.O. (2010), Uchanganuzi wa Kiisumu wa Baadhi ya Matini za Kiswahili. Mtazamo wa Pragmatiki Leksika. Nairobi, Tasnifu ya Uzamili ambayo bado haijachapishwa.

Katamba, F. (1993), *Morphology*. Cambridge; Cambridge University Press.

Mathews, P.H. (1997), *A Concise Dictionary of Linguistics*. New York. Oxford University Press.

Mazrui, A.M. (1995), *Sheng and Code Switching*: The Case of Sheng in Kenya. Africanistisch Arbeitspapier 42:168-179

Mbaabu, I. na K. Nzuga, (2003), *Sheng-English Dictionary*: Deciphering East Africa’s Underworld Language. Dar es Salaam: TUKI.

Moga, j. na D. Fee, (1993), *Sheng Dictionary*. Nairobi: Ginsen publishers.

Momanyi, C. (2009), *The Effect of Sheng in the Teaching of Kiswahili in Kenyan Schools*. The Journal of Pan African studies, 12:127-138.

Mgalla, R.S. (1999), *Mtalaa wa Isimu,, Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mukhwana , A. (2008), *Language Attitude in Urban Kenya:A Case Study of Nairobi, Mombasa and Kisumu*. Tasnifu ya uzanifu ambayo bado haijachapishwa.

Mgesa, M. (2002), *And Sheng Lives on Profile*. East Asfrican Standard 16-22, Feb 2001.

Obuchi, S. M. na A. Mukhwana (2010), *Muundo wa Kiswahili; Ngazi na Vipengele*. Nairobi: Frame publishers.

Ogechi, N.O. (2002), *Codeswitching in Kenya Evidence from Ekegusi, Kiswahili, English and Sheng*. Tasnifu ya uzamifu ambayo haijachapishwa. Hamburg: University of Harmberg.

- Ogechi, N.O. (2005): *Lexicolization in Sheng*. Nordic Journal of African studies 14(3), 334-355.
- Osinde, K (1986), *Sheng; An Investigation into the Social and Structural Aspects of An Evolving Language*. Tasnifu ya B.A ambayo bado haijachapishwa. Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Richards et al, (1985), *Longman Dictionary of Applied Linguistics*. U.K, Longman Group.
- Samper, H. (2002), *Taking Sheng: The Role of Hibrid Language in the Constitution of Identity in Youth Culture in Nairobi, Kenya*. Tasnifu ya Uzamifu ambayo bado haijachapishwa. University of Pennsylvania.
- Saussure, F. (1916), *Course in General Linguistics*. London: Duckworth.
- Shitemi, N.L. (2002), *Pidginization Sheng, The Melting-pot of the Kenyan Language and an Anti- Babel Development* . Kiswahili 64: 1-15
- Spyropoulos, M. (1987), *Sheng: Some Preliminary Investigation into a Recently Emerged Nairobi Street Language*. Journal of the Anthropological Society at Oxford,18 (18) 125-136.
- Trudgill, P. (1974), *Sociolinguistics: An Introduction to Language and Society*. England: Penguin books.
- Ullmann, S. (1957) *The principles of Semantics*: Great Britain: Britain: Blackwell and Mott.
- Ullmann, S. (1962), *Semantics. An Introduction to Science of Meaning*. Great Britain: Blackwell and Mott.
- Willson, D. na D. Sperber, ((2002), *Truthfulness and Relevance*. Mind. 111. 3-6